**29 AGOSTI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Agosti, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuweka Mezani Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024)*.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya kujibu maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na matukio ambayo yanaashiria uvunjifu wa haki za binadamu. Matukio haya ni pamoja na mauaji, utekaji lakini pia utekaji na uuaji wa watoto. Matukio haya yamekuwa na sura tofauti tofauti ikiwepo wivu wa kimapenzi, lakini pia ushirikina na matukio mengine ya kutekwa na kupotea kwa watu yanahusishwa na vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua mkakati wa Serikali, moja kuzuia matendo haya, lakini kuondoa taharuki ambayo inajitokeza kwenye jamii. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, najiuliza hilo swali ni la Mheshimiwa Waziri Mkuu au ni la kisekta. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pengine unaweza kutoa maelezo kidogo siyo kwa maana ya kujibu swali, kwa nini? Kwa sababu juzi mtakumbuka hapa alisimama Mheshimiwa Aida Khenani, mambo hayo ambayo yanahitaji uchunguzi ukiyasema kwa ujumla kwa haya maneno, utekaji, mauaji.

Leo asubuhi nimesoma kuna mganga sijui amezika watu sijui kumi na ngapi. Sasa wale ni Polisi, ni vyombo vya dola, huyu mganga ambaye watu wameuawa na wamezikwa kwake. Sasa unajua haya mambo yakiwa yanasemwa kwa hisia yanaleta picha fulani hivi. Kwa hiyo, mtu mwingine anaweza kuwa anahisi labda kuna mtu ana roho mbaya mahali hajali. Kila mtu anajali, kila binadamu ana haki ya kuishi lakini tusiweke yale mazingira ya kuonesha kwamba kila anayepotea.

Kuna watoto ambao, si kuna mabasi kule wanapanda kule chini, akidondoka huko njiani nyumbani si wanamtafuta? Utasema ni chombo cha dola kimemchukua? Yaani sisi wote lazima tufanye hii kazi kama viongozi. Ukichukua mihemko, ukitumia mihemko hutoi nafasi kwa Serikali kufanya kazi yake, wakati huo huo hutoi nafasi kwa jamii kuendelea kushiriki hili zoezi kwa sababu na wao wanawaza kuna mahali watu wapo, lakini kumbe hawapo mahali, mganga kawazika mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, labda utoe maelezo tu ya jumla kuhusu jambo hilo, lakini kwa maana ya swali, sisi wote humu ndani ni viongozi na kwa kweli tunawakilisha wananchi na tungependa wananchi wawe salama. Sasa ukisema mambo ya jumla jumla na wewe chukua nafasi ya uongozi unaweza kutoa ushauri, lakini usinyooshe vidole kwa sababu huna hakika na wengine wanahama nchi. Mwingine anaenda, si tunakamata hapa wahamiaji haramu kila siku na wenyewe huko kwao wanatafutwa, watasema ni chombo cha dola kimewachukua kimewapeleka sijui wapi, lakini kumbe alifika hapa Tanzania mazingira yakawa magumu amekamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuanza na ufafanuzi huo ili Watanzania waweze kujua. Nataka nieleze tu kwamba tunapoilinda nchi ni wajibu wetu Watanzania wote kwa kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyombo vya ulinzi na usalama nchini vyenye jukumu la kupokea taarifa mbalimbali zinazoonesha

uvunjifu wa amani popote pale kadri taarifa zinavyokuja pale kwenye meza za vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Jukumu lao hawa wakishapokea taarifa ni kuhakikisha kwanza wanafanya uchunguzi na uchunguzi utakapobaini waliotenda makosa wanachukuliwa hatua kwa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kujikita kusimamia misingi ya amani katika nchi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi. Pia tumeendelea kujikita kwenye misingi yetu ya amani na ulinzi kwa gharama yoyote ile kuhakikisha kwamba mipaka yetu, raia wetu lakini na mali zao zinabaki kuwa salama na hiyo ndiyo inayoleta amani katika nchi. Kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kwamba suala la ulinzi na usalama bado lipo mikononi mwetu pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunasaidia vyombo vya ulinzi kwa kutoa taarifa zozote zile ambazo zinaleta tishio la amani katika nchi ili kuvisaidia vyombo vyetu viweze kuchukua tahadhari na hatua stahiki ili kuwabaini wale wote ambao wanasababisha kutokuwepo kwa amani kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe wito kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea na wajibu wao wa kuhakikisha kwamba kila taarifa inayopatikana lazima ifanyiwe uchunguzi, lakini pia na kubaini wale wote ambao wanahusika kama wanapatikana wachukuliwe hatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nashukuru sana kwa maelezo yako ya msingi ya awali ili kuondoa upotoshaji ambao unaweza kuwa unaendelea na kufanya vyombo vyetu vishindwe kufanya kazi yake halafu tukawavunja moyo hawa watu ambao wanafanya kazi masaa 24 kwa ajili ya ulinzi ambao leo unatufanya hapa tubaki salama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu inaamini katika uongozi wa kisheria na utawala bora ili kujenga umoja, mshikamano na upendo baina ya wananchi na Serikali yao, lakini kumekuwa kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya wateuliwa wa Mheshimiwa Rais, Wakuu wa Mikoa na baadhi ya Wakuu wa Wilaya kwa kutumia nguvu na mamlaka yao vibaya kukamata viongozi na wananchi na kuwatupa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwanza jambo hili moja, limetengeneza chuki kubwa baina ya wananchi na Serikali yao, lakini pili, linafifisha jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais za kuhubiri *4R*. Linatengeneza chuki kubwa, mwisho wa siku hili jambo linakuwa halileti mantiki. Nataka kujua kauli ya Serikali ni ipi katika kukemea jambo hili ambalo linatengeneza chuki kubwa baina ya Watanzania na Serikali yao. Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa hawa watawala ambao wanatumia mamlaka yao vibaya kutesa na kuwanyanyasa wananchi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili analoliuliza Mheshimiwa Mbunge ni lile ambalo jana Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Ifakara eneo la Mlimba aliliuliza jana na Mheshimiwa Spika, alitupa kazi Serikali kulifanyia kazi. Tutakapokamilisha tutatoa majibu kwa Mheshimiwa Mbunge na naamini kwa majibu hayo pia tutamjibu na Mheshimiwa Fiyao.

Mheshimiwa Spika, kwa utangulizi ni kwamba ni kweli baadhi ya watawala kwenye maeneo yao wanazo sheria ambazo zinawaruhusu kuhakikisha kwamba hali ya utulivu na ulinzi wa usalama kwenye maeneo yao inaimarika na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba baadhi ya wateuliwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie wale waliotamkwa jana, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao pia ipo sheria wanaitumia. Jana ulisimama ukafafanua vizuri na nataka kuungana na wewe kuuhakikishia umma wa Tanzania kwamba sheria ile inayomruhusu Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya kumkamata mwananchi au yeyote yule kumweka ndani haikulenga kama ambavyo baadhi wanaitumia. Lengo ni katika kuhakikisha kwamba mazingira hayo kusitokee uvunjifu wa amani mkubwa na kwa hiyo anaweza akatumia sheria hiyo kumhifadhi mahali ili hali itulie na baadaye aweze kutoka na kuendelea na majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anaweza kuwa tishio lipo kwa Mkuu wa Wilaya mwenyewe au Mkuu wa Mkoa mwenyewe anaweza kutumia nafasi hiyo ili kulinda, inaweza kuwa jambo hilo ni hatari kwa wananchi anaweza kuitumia nafasi hiyo kulinda usalama wa raia wale lakini pia hata huyo huyo mwananchi ambaye analeta hiyo hoja kulinda usalama wake, basi sheria inaweza kutumika kwa yeye kumwondoa eneo lile na kumhifadhi mahali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeshazungumzwa mara kadhaa hapa Bungeni, jambo hili tumeshatoa ufafanuzi mara kadhaa hapa Bungeni na tulitaka tuchukue hatua. Nataka nikuhakikishie kwamba wiki mbili, tatu zilizopita Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wote waliitwa hapa Mkoani Dodoma kwa semina katika maeneo mbalimbali. Eneo hili la sheria hii limezungumzwa sana na wameelimishwa sana na tunaamini sasa watakuwa wanaelewa namna ya kuitumia sheria ile bila kuleta madhara, bila kuleta chuki miongoni mwao na wananchi na bila kuleta mtafaruku katika jamii ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata kama anatumia sheria hii mashariti yake ni kwa masaa 24 ambayo baada ya masaa 24 anatakiwa

kutoa taarifa ya kwa nini yule aliyepo ndani kawekwa na kuwezesha chombo husika kuchukua hatua. Kama hana jambo lolote anatakiwa baada ya masaa 24 yule aliyeingizwa polisi anatakiwa aondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana tumefuatilia kule Kilombero tumeona wale watuhumiwa wote wameshapelekwa Mahakamani. Kwa hiyo jambo lile hatuwezi kulizungumza tena kwa sababu tayari hatua zimeshachukuliwa na sasa hivi wapo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tutaendelea pia kuelimisha wateule wote wenye sheria hizi ili waweze kuzitumia kwa weledi, lakini kwa uaminifu na uadilifu kuzingatia sheria na taratibu za nchi ili pia kuleta amani katika jamii bila kuleta msuguano, migongano isiyokuwa muhimu ili kuwezesha kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo ya msingi kwa awali. Tutakavyopata taarifa zilizokamili ya tukio hili lilikuwaje ili tuweze kuhusisha swali la Mheshimiwa, hoja ya Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Stella Fiyao, wote Waheshimiwa Wabunge tutawapa taarifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kumekuwa na changamoto ya watoto wenye ulemavu kutokupata huduma za kunyooshwa na kurekebishwa viungo katika maeneo mbalimbali nchini. Sasa hii inapelekea ongezeko kubwa la watoto wenye ulemavu na ongezeko la watu wenye ulemavu. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wanaweka vituo katika kila mkoa ili mtoto pale anapozaliwa aweze kupata huduma hii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kadija Taya, maarufu Keysha, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya afya hapa nchini kwa sasa yameimarishwa sana na uwekezaji mkubwa umefanywa. Kwa mujibu wa tafiti zetu ndani ya Wizara ya Afya imeelezwa kwamba hatua mbalimbali za mama mjamzito kabla hajajifungua zinaweza kubaini aina ya ulemavu wa mtoto alionao na uwezekano wa kupunguza ulemavu kwa zaidi ya 80% inawezekana. Kwa maana hiyo kwa uwekezaji ambao sasa Serikali umeufanya kutoka ngazi ya zahanati, vituo vya afya lakini hospitali za wilaya, hospitali za mkoa, kanda na kitaifa; siyo tu kuamua hospitali moja katika mkoa ndiyo iwe inashughulika na kutoa huduma kwa walemavu, ni vituo vyote vinavyotolea huduma vinatakiwa kupata vifaa na vifaa vimeshapatikana na sasa kila eneo huduma hii inaweza kutolewa ya kupunguza uwezekano wa mtoto kuwa na ulemavu kama nilivyosema ulemavu huu unaweza kuepushwa kwa zaidi ya 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huduma hizi zinapatikana sasa kuanzia vituo vya afya mpaka huko juu kwa kutoa wito kwa wamama wajawazito kuhudhuria kliniki ambayo itasaidia kupata elimu, lakini na uchunguzi wa mara kwa mara mpaka anapojifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoto anapobainika amezaliwa ana ulemavu bado wataalam wetu wa afya kupitia vituo vyote vya utoaji huduma wanaweza kulifanyia kazi hilo kutoka umri mdogo wa mtoto mpaka umri ambao ulemavu huu unaweza ukapunguzwa kwa zaidi ya 80%. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili halihitaji ku-*specialize* hospitali moja kwenye eneo, kwenye mkoa ni kila eneo la utoaji huduma kuanzia zahanati na kuendelea. Pale ambapo mama anahudhuria kliniki tunaweza kubaini na tunaweza tukaanza kazi ya kuokoa ulemavu huo kwa zaidi ya 80%. Hayo ndiyo majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo James, Mbunge wa Buchosa. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Uchumi wa dunia sasa unabadilika na unajielekeza kwenye *digital economy,* kwa maana ya uchumi wa kidigitali. Katika hili vijana wengi wa Kitanzania wamekuja na ubunifu wa aina mbalimbali. Wapo waliobuni mifumo ya kufanya kazi mbalimbali, wapo hata waliotengeneza umeme. Changamoto kubwa ya vijana wetu inakuwa ni mtaji wa kukuza ubunifu wao kuwa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, sasa zipo nchi mbalimbali zimeanzisha mifuko ya ubunifu *(innovation funds)* ikiwemo Kenya na Ethiopia. Je, nchi yangu ipo tayari sasa kuanzisha Mfuko huu kwa ajili ya kuwasaidia vijana wa Kitanzania wenye ubunifu kupata mitaji ili kuendeleza ubunifu wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric Shigongo, Mwandishi wa Magaziti pendwa, Mbunge wa Buchosa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake linahitaji kujua, kwamba Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mfuko ambao utawasaidia wabunifu ndani ya nchi kuendelea na majukumu yao. Ametoa mifano kutoka katika nchi nyingine. Nataka nimhakikishie kwamba Serikali ilikwishaanza mkakati huu muda mrefu wa kuhakikisha kwamba kwanza tunawatambua wabunifu kwa kuanzisha maonesho mbalimbali ya wabunifu mbalimbali kuwaleta pamoja kuja kuonesha kazi. Hili linasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo kwa miaka sita sasa inakuwa na maonesho kila mwaka ya kuwaleta wabunifu pamoja ili kuonesha kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeshaanzisha Mifuko inayoweza kusaidia wabunifu hawa kufanya kazi yao kwa uhakika

zaidi. Moja, Tume ya Ubunifu *(COSTECH)*. Tume ile inayo pia Mifuko miwili; Mfuko wa kwanza ni wa utafiti wa wabunifu. Watafiti wote wanaobuni kazi zao Mfuko ule una fursa nao ya kwenda kupata msukumo wa kuendelea na utafiti wao. Sasa upo ule Mfuko wa jumla wa wabunifu ambao pia baada ya kuwa umebuni kazi yako unataka kuiendeleza, ukienda pale *COSTECH* unakuta kuna dirisha linaweza kutoa mitaji ya kuendeleza ubunifu ulioubuni.

Mheshimiwa Spika, hatujaishia hapo, pia Wizara ya Elimu yenyewe inao Mfuko ambao unawawezesha wabunifu kufanya kazi zao. Miaka yote hii inaposimamia maonesho ya ubunifu Wizara ya Elimu inachangia sana ubunifu huu kukua. Vijana wengi sasa waliopo shuleni kwenye shule zetu za msingi, sekondari wameweza kunufaika na Mfuko huu kwa ajili ya kuandaa ubunifu wao na kwenda kuuonesha kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kadhaa ikiwemo na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Wasanii wabunifu wanao Mfuko wao, Mfuko wa Ubunifu wa Sanaa na Utamaduni ambao pia upo kwenye Wizara hiyo na Mifuko mingine ambayo inaweza kuwezesha wabunifu hawa kupata mitaji ya kuendeleza ubunifu wao, hiyo ipo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imefungua milango ya kwenda kuzungumza na *private sector,* taasisi za fedha ili ziweke dirisha na dirisha tayari lipo, lipo *CRDB, NMB, AZANIA, NBC* na Benki nyingine. Kama Mwanga hapa Dodoma nayo pia imefungua dirisha linalowaruhusu wabunifu kwenda kupata mtaji na kubuni kazi zao.

Mheshimiwa Spika, sasa Mifuko hii niseme tu kwamba tumepata wazo zuri na ushauri mzuri na Mheshimiwa Eric Shigongo tutahakikisha kwamba kwanza inabidi tuutangaze na kujua namna hatua ya kupata mitaji hiyo ili itoe fursa ya wabunifu wote sasa kwenda kupata mitaji hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kushauri haya nataka nikuhakikishie kwamba tutalifanyia kazi kwa sababu sasa Serikali

imeweka msisitizo wa ubunifu kwa Watanzania na tumeona mafaniko yake makubwa. Nataka ubunifu huu uendelee na utengeneze kazi waingie kwenye masoko na iwasaidie wabunifu kupata masoko ya kazi yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhani Abeid Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla ya kuuliza swali nitoe pole kwa wananchi wenzangu wa Singida Kaskazini ambao walipatwa na kadhia ya yale mauaji ya yule mshirikina. Nilifika kule jana nimejionea na kuwapa pole.

Mheshimiwa Spika, hapa nikupe wewe pongezi kwa maelezo uliyoyatoa ya kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kuhakikisha wanachukua hatua ya kudhibiti jambo lile na kumkamata yule mtu na kuhakikisha anatoa ushirikiano mpaka yamepatikana mauaji ya miili mingine nane katika Wilaya ya Chemba, Kijiji cha Mialo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika msimu huu wa mavuno kumeanzishwa mfumo mpya wa kuuza mazao ya mikunde kunde hasa dengu na mbaazi katika baadhi ya maeneo hapa nchini, ambapo Serikali imeelekeza kutumika kwa mfumo mpya wa stakabadhi ghalani ambao pia hapa niipongeze Serikali kwa sababu imewasaidia wananchi kuuza moja kwa moja kati ya wakulima na wanunuzi na kuwaondoa wachuuzi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umeanzishwa katika mikoa hii na mpya, wananchi wengi hawauelewi. Sasa kumetokea changamoto kadhaa ikiwemo kucheleweshewa malipo, lakini pia wananchi kutembea mbali mrefu kupeleka mazao ghalani na tatu, baadhi ya maghala hayajasajiliwa na mengine hayana bima. Je, Serikali sasa imejipangaje ili kuhakikisha kwamba inatoa elimu kwa wakulima pamoja na wadau wote wanaohusika na zao hili au ununuzi kwa mfumo huu, ili kuhakikisha wakulima

wanapata bei nzuri, pamoja na kutatua hizi changamoto ambazo zimejitokeza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ili upate majibu ya uhakika nadhani swali linatakiwa lijibiwe na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, yupo hapa sijui kama leo ana swali, kama hana swali nitampa nafasi ili akujibu saa ya maswali itakapofika. Kama analo swali atakaposimama hapa utasimama nitakupa hiyo nafasi ya kumuuliza.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Ulanga.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa nchi yetu imejipambanua sana kwenye uwekezaji na wawekezaji wengi wamekuwa wakiingia kwa ajili ya uwekezaji, lakini kumekuwa na hali duni katika maeneo ya barabara pamoja na huduma za afya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaboresha huduma hizo ili kuwezesha uwekezaji zaidi katika nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim, Mbunge wa Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kujibu swali hili kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Salim yeye ni mwekezaji mkubwa hapa nchini. Amewekeza kwenye madini, lakini pia na viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwenye mazao ya kilimo. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji nchini limepata msukumo mkubwa baada ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuonesha dhamira ya dhati nchini ya kupanua wigo wa uwekezaji kwa kuwashawishi Watanzania kuwekeza, lakini pia na mataifa ya nje kuwekeza nchini. Alipokuwa anatoa msukumo huu tayari Serikali ilishakuwa na mwelekeo mzuri.

Kwanza kisiasa, siasa yetu inaruhusu uwekezaji hapa nchini; mbili, tuliimarisha Sera ya Uwekezaji ambapo tumetoa fursa kwa Watanzania na mataifa ya nje kuingia nchini kuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweka sheria na kanuni nzuri tu ambazo zinaruhusu uwekezaji na kumletea faida mwekezaji, yeye mwenyewe ni shahidi kwa sababu yeye ni mwekezaji. Kwenye eneo hili Serikali ilishapunguza hata gharama ya uwekezaji kwa Watanzania kutoka dola 100,000 mpaka dola 50,000, ambayo tayari una uwezo wa kuwekeza na wale wa nje tuliwapunguzia kutoka dola 200,000 mpaka dola 100,000. Hii inaruhusu wawekezaji wengi kuingia nchini. Tunataka tuone uzalishaji unakuwa mkubwa ndani ya nchi ili tupeleke bidhaa zetu nje.

Mheshimiwa Spika, pia, tunapotoa wito wa uwekezaji Serikali imejiimarisha katika kutoa huduma muhimu kwa wawekezaji. Moja, nishati ya umeme ya kuendesha viwanda, sasa hivi tuna umeme mwingi wa kutosha na bado Bwawa la Mwalimu Nyerere linaendelea kufunguliwa milango ya kuzalisha umeme. Sasa hivi tupo mlango wa tatu na kila mlango unatoa megawati 235; na tunaendelea mpaka milango yote tisa. Hii nchi tutakuwa tupo mbali sana, tutakuwa na umeme mwingi wa kutosha na unaopatikana kwa uhakika, hilo hatuna mashaka nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la usafirishaji, ili mwekezaji aweze kusafiri yeye mwenyewe na bidhaa zake Watanzania wote mnajua tuna *network* yetu nzuri tu ya barabara nchini. Kila Mkoa unafikika kwa barabara ya lami na kule vijijini tunaimarisha barabara za vumbi. Pia, kwenye maji tuna meli, tumeshajenga Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa. Wote mnajua kwamba Ziwa Nyasa, sasa meli inakwenda mpaka Malawi, Ziwa Tanganyika tunajenga meli na bandari tumeziimarisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la huduma ya afya kama alivyosema, mwenyewe na Watanzania wanajua kwamba tuna zahanati ambazo zimeimarika na tunaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya Hospitali za Wilaya na Halmashauri mpaka ngazi ya Kitaifa. Kwa hiyo, mwekezaji akija nchini hatuna mashaka na

huduma zinazoweza kumwezesha yeye kuishi ndani ya nchi lakini pia kupata huduma pale anapopata tatizo yeye na wafanyakazi wake kwa sababu Serikali imejiimarisha kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa niendelee kutoa wito kwa wawekezaji wote wa ndani kwa Watanzania na walioko nje ya Tanzania kuja Tanzania, kuja kuwekeza kwa sababu tuna rasilimali za kutosha ambazo pia na sisi wenyewe tunazitumia hapa ndani na zinafaa pia kuja kuwekeza ili tuweze kuzalisha bidhaa nyingi na tuzipeleke nje ya nchi tuweze kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Salim, kwamba uwekezaji wake hatapata hasara na wawekezaji wengine wote hawatapata hasara. Serikali ipo pamoja na wao pale wanapopata tatizo wasisite kutuona ili tuweze kutatua tatizo la uwekezaji hapa nchini. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu sote kwamba vijana ni kundi muhimu sana katika ukuzaji wa uchumi wa nchi yetu. Hivi karibuni kumeibuka wimbi kubwa la vijana kulewa sana wakati wa kazi wakati wa mchana na hii ni kutokana na uingizwaji wa vilevi vikali sana kutoka nje ya nchi, lakini vilevi ambavyo vinapatikana kila mahali kiasi kwamba kijana anaweza kwenda gengeni akamiminiwa kakinywaji kidogo baada ya hapo analewa kabisa na kushindwa kuendelea na kazi. Je, Serikali ina kauli gani juu ya udhibiti wa vileo hivi vikali ambavyo vinaathiri uchumi wa vijana na vinaathiri ujenzi wa uchumi wa nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inao utaratibu unaowezesha kutambua uzalishaji, uuzaji lakini pia kudhibiti bidhaa ya vileo inayoingia hapa nchini. Vileo hivi vinaendelea kusambaa kwa wateja kwa utaratibu uliowekwa wa wanaopata vibali vya biashara na kuendesha biashara za vileo. Serikali yetu inaendelea kutoa elimu kwa jamii yetu, ile ya kuelekeza au kuonesha madhara ya ulevi uliopitiliza, ikiwemo na hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, kwamba vijana wengi wanalewa wanakosa uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili siachi kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amefanya kazi kubwa ya kuhamasisha vijana kujiunga pamoja na kutengeneza makundi yanayoweza kufanya shughuli za ujasiriamali. Vipo vikundi vya ujasiriamali vya mtu mmoja mmoja pamoja na vya pamoja wanaofanya biashara kwa siku zima na vinawapatia mapato. Utaratibu huu umesaidia sana vijana wetu kupata pato linaloendesha yeye na jamii yake.

Mheshimiwa Spika, tumeona hapa Dodoma *Machinga Complex* vijana wa kawaida wapo pale wanafanya biashara zao. Tumeona kila Wilaya waendesha bodaboda, bajaji, wafanyabiashara za kawaida na machinga. Hii yote ni jitihada za Mheshimiwa Rais katika kuhamasisha kwamba wanakaa pamoja na kutafuta shughuli ya ujasiriamali. Sasa hivi tunaendelea kuwahamasisha nchini kwa vijana wote kuingia kwenye shughuli ambazo zinawazalishia mali kuliko kuingia kwenye makundi ambayo hayana tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kinafanyika; ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii hii kuhakikisha kwamba wanaingia zaidi kwenye shughuli za uzalishaji mali huku pia tukiimarisha sheria kwa wazalishaji wanaoingiza bidhaa za vilevi ndani ya nchi, wauzaji na watumiaji, hasa kwenye maeneo yale ya wanaokiuka sheria maana tunazo sheria zetu. Kwa hiyo wale wanaokiuka sheria huwa tunawachukulia hatua. Hii inasaidia kupunguza kuingiza kwa pombe ambayo ni kali kupitiliza kiasi. Malengo yetu ni kwamba kila aina ya kileo kinachoingia nchini kinakidhi mahitaji ya afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jamii itusaidie kutambua uingizaji na utengenezaji wa bidhaa usiokuwa rasmi ambao haujapata vibali. Hawa ndio wanaotengeneza bidhaa hiyo ambayo ni kali kupita kiasi bila kutambuliwa na wale wote ambao wana leseni wanatengeneza bidhaa ambayo nayo imepimwa na inakidhi mahitaji ya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa taasisi zote zinazofanya shughuli za vijana kuendelea kuwaelimisha vijana hawa maadili mema na pia kuendelea kutoa elimu stadi za maisha kwa vijana hawa. Muhimu zaidi kutoa elimu ya ujasiriamali kwa lengo la kuwaonesha kwamba njia nzuri sahihi ni hii ambayo utakuwa unajishughulisha, unapata pato kuliko njia hii ya kuendelea kula viroba ambavyo baadaye vitamlaza siku zima; hana mtaji hawezi kupata mafao, hawezi kupata kujikimu kwenye familia. Huu ndio mpango mkakati ambao Serikali tunao, wa kuhakikisha kwamba vijana wetu tunawapa fursa za kushiriki kwenye ujasiriamali ili waachane na shughuli nyingine waendelee kwenye ujasiriamali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Elimu uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika shule za sekondari na shule za msingi na shule mpya nyingi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga nyumba za walimu kuziba upungufu au ombwe la nyumba za walimu katika shule zote za sekondari na msingi nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Maige, Mbunge wa Tabora, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye Sekta ya Elimu. Tumejenga miundombinu mbalimbali kwenye Kurugenzi ya Msingi, lakini pia miundombinu mbalimbali kwenye Kurugenzi ya Sekondari. Tunaendelea kubaini mahitaji ili tuweze kujenga miundombinu mingine ikiwemo na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze mkakati wa Serikali unaenda kwa awamu, tulianza na ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na matundu ya vyoo kuruhusu wanafunzi kwenda shuleni. Kwa upande wa sekondari tumeendelea kujenga maabara ili waweze kusoma masomo ya sayansi, tumejenga majengo ya utawala ili walimu wapate nafasi ya kukaa na kusimamia shughuli za masomo na sasa tunaingia kwenye *phase* ya ujenzi wa nyumba za walimu ili walimu waweze kuishi maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote mnatambua bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI mliyopitisha kipindi kilichopita, sasa tunaingia kwenye awamu ya ujenzi wa nyumba za walimu. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati ambao Serikali unao wa ujenzi wa nyumba za walimu kupitia bajeti hii. Migawo itakapoanza, Waheshimiwa Wabunge mtashuhudia kwenye maeneo yenu na tunaomba msaidie kusimamia fedha hizo, kusimamia ujenzi, ili walimu waweze kupata nyumba za kuishi kwenye maeneo hayo. Huo ndiyo mkakati wa Serikali kwa sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu muda wetu umekwisha, lakini nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa CHADEMA, kwa hivyo nimwombe radhi kwa sababu sio yeye aliyekuwa ameomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimejulishwa hapa kwamba kulikuwa na makosa ya uchapaji. Aliyekuwa ameomba alikuwa ni Mheshimiwa Esther Malleko, Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi, Mbunge wa Viti Maalum. Sasa muulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wanawake wengi wamekuwa wakijihusisha na biashara za

mazao ya kilimo kandokando ya barabara kuu hapa nchini. Je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha kwamba wanawake hawa wanatengenezewa mazingira bora ikiwa ni kujengewa mabanda ili waweze kufanya biashara zao katika hali nzuri zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Malleko Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeshuhudia akinamama sasa hivi wamekuwa na mwamko mzuri tu wa kufanya shughuli za ujasiriamali na kufanya biashara kando kando ya barabara zetu. Unapokwenda Dar es Salaam tunawakuta hapo Gairo, lakini pale mbele kidogo Dumila hata Mikese unakuta wamejipanga wanafanya biashara zao na barabara zote nchini utakuta akinamama wengi na vijana wengine wa kiume wakifanya biashara zao. Zipo baadhi ya halmashauri zimekuwa na maono na zimeendelea kusimamia wajasiriamali hawa kwa kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya biashara zao kwa kuwajengea vibanda vya kibiashara kama pale Dumila palivyo, lakini na eneo la Mikese kwa Halmashauri ya Morogoro Vijijini. Mheshimiwa Taletale ameshiriki pia kuwajengea vibanda wafanyabiashara, wananchi wake eneo la Mikese, Mbunge wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu huu ni utaratibu ambao unawahamasisha hawa wafanyabiashara kufanya biashara zao vizuri, lakini pia wanakingwa na mvua na jua wanapofika kwenye msimu huo wakiwa wanaendelea kufanya biashara zao, lakini hata bidhaa inayouzwa inabaki kuwa salama na inafaa kwa kuendelea kuliwa pale ambapo inakaa kwenye kivuli na mahali sahihi pa kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua mipango ya Serikali, nitoe maelekezo kwa halmashauri zote nchini zihakikishe zinaendelea kutambua wajasariamali wanawake na vijana wanaouza biashara zao kandokando ya barabara kwa ajili ya wasafiri wanaosafiri ili

watengenezewe mazingira mazuri ya kufanya biashara hiyo kwa kuwajengea vibanda vinavyowakinga na jua na mvua, lakini vinavyokinga pia bidhaa zile kwa jua na mvua ili bado mlaji apate bidhaa iliyo safi na salama ambayo bado ina mng'aro unaovutia kununuliwa. Hili litasaidia sana wajasiriamali hawa kupata kipato chao kwa uhakika na kufanya biashara kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunalichukua hili na kama ambavyo nimeiagiza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia halmashauri zote wasimamie jambo hili ili wajasiriamali hawa wafanye biashara kwenye maeneo haya na wapate manufaa ya biashara zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Kuharakisha Malipo ya Wastaafu Nchini**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha malipo ya wastaafu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali uliopo kwa sasa ni pamoja na mipango ifuatayo katika kuhakikisha kwamba mafao yanalipwa kwa wakati:-

(i) Kuharakisha malipo kwa kupunguza muda wa kuchakata malipo hayo ambapo kwa sasa malipo yanalipwa chini ya siku 60 na imetungwa kabisa sheria ya kuweza kuhakikisha ndani ya siku 60 malipo yanafanyika;

(ii) Kutumia mfumo wa TEHAMA mfano *PSSF* Kiganjani ambapo mtumishi anapata taarifa za muda wote na hivyo kujua hali ya michango yake; na

(iii) Kupunguza mrundikano wa madai kwa kulipa madeni ya zamani mfano yale ya kabla ya mwaka 1999 ambapo mwaka 2012 Serikali ililipa zaidi ya trilioni mbili na pia michango ya wanachama kulipwa moja kwa moja kupitia Hazina kwenda katika Mfuko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, marekebisho ya sheria mbalimbali yamefanyika yakiwemo sheria ambayo tutaiwasilisha hapa Bungeni kwa siku ya leo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa vile bado kuna wimbi kubwa la watumishi ambao wamestaafu lakini hawajapata malipo yao ya kimsingi kwa maana ya kiinua mgongo. Je, Serikali haioni sasa kubadilisha sheria ili watumishi wa Serikali waendelee kubaki katika utumishi

wao hadi pale taratibu za malipo zitakapokuwa zimekamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kwa sasa kwa sababu tayari tumekwishatungia sheria na inataka ndani ya siku 60 mafao yawe yamekwishalipwa. Kwa mfano, kama ana kesi mahususi yeye ya wastaafu ambao hawajaweza kupata, niipate kwa sababu, mpaka sasa hivi kwa Mfuko wa *PSSSF* kwa mwaka wa fedha 2023/2024, wastaafu walioomba wote kwa ujumla walikuwa 8,957, kati ya hao 5,016 wamekwishalipwa ndani ya siku 60, ambao ni sawa na 54% kwa *PSSSF*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeendelea kuhakikisha kwa wale 3,941 ambao wana changamoto pengine labda kutokana na waajiri wao kutokupeleka michango au mapungufu ya kinyaraka na mazingira mengine ambayo yanasababisha pengine kuna changamoto za kumbukumbu yameendelea kushughulikiwa na yanapofikishwa mwisho ndani ya wiki mbili anakuwa amelipwa mafao yake. Kwa upande wa Mfuko wa *NSSF* kwa *private sector,* nakumbuka tulikuwa na maombi zaidi ya 3,344 ya wastaafu ambao walikuwa wanahitaji kulipwa. Kati ya hao zaidi ya 3,325 tayari wamekwishalipwa na hii ni sawa na zaidi ya 90% ya ulipaji ndani ya siku 60.

Mheshimiwa Spika, kuna wale 16 tu ambao bado kwa *NSSF* nao pia ni kwa sababu waajiri hawajapeleka michango na kuna kesi zipo mahakamani na tumeendelea kuchukua hatua. Kwa hiyo, sasa hivi hakuna mstaafu ambaye anachelewa kupata mafao yake au kulipwa pensheni yake ndani ya siku 60 kwa mujibu wa sheria, tunalitekeleza hilo na kama kuna hizo kesi muda wote tumeendelea kuomba waweze kutufikishia ofisini kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, wazee wengi waliostaafu kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia pensheni wanayopewa kila mwezi kwamba ni kiasi kidogo ambacho hakikidhi mahitaji yao. Je, ni lini Serikali itapitia upya ili kuweza kuongeza kiasi hicho wanachowapa kwa sasa ambacho ni 100,000 tu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nenda moja kwa moja tu kumjibu Mbunge bila kumtaja kwa sababu mimi nilishamtaja, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa kuna malalamiko, hivyo tayari ni zilipendwa kwa sasa kwa sababu baada ya mabadiliko haya ya kulipa ndani ya siku 60 na ambayo ipo ndani ya sheria, malalamiko kwa kweli kwa sasa hayapo ofisini na kama yapo mahususi kama ninavyosisitiza tuweze kuyalipa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pensheni ambayo ilikuwa ina changamoto kwa maana ya kwamba kulikuwa kuna malipo ya mkupuo na yale malipo ya pensheni ya kila mwezi, mwaka 2018 tulikuwa tunalipa 25%, lakini baada ya mjadala mkubwa wa Serikali pamoja na vyama vya wafanyakazi kupitia *TUCTA*, Shirikisho la Vyama vya Wafanyazi lakini pia waajiri *ATE (Association of Tanzania Employers)* walikubaliana na kufikia muafaka na Serikali wa kutoka 25% mpaka 33% na sasa tumetoka 33% kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumefika 40% na tunaendelea kuhakikisha kwenye mkupuo pia tutoke ile 50% kwenda 67% na sasa kuna maboresho tena ya asilimia nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aamini tu kwamba Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda sana wafanyakazi na inatambua mchango wao wa utumishi na tutaendelea kuboresha kila wakati kwa sababu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge nimekuona, lakini ulipaswa kusimama anaposimama yule mwenye swali lake sasa umesimama baadaye. Kwa hiyo, utatafuta fursa nyingine itakapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali imeshapiga hatua kubwa kwa kweli, siku hizi wastaafu wengi wanalipwa mafao kwa wakati lakini hii ya miezi miwili kwa nini? Kwa sababu huyu alikuwa mfanyakazi kwa hivyo alikuwa anategemea mshahara mwisho wa mwezi, hii miezi miwili anayochelewa kulipwa anakuwa anaishije? Kwa sababu yeye anasubiri. Lengo la mafao ni kwamba inachukua ile nafasi ya mshahara. Kwa hiyo, mshahara unapokata ile tarehe aliyokuwa anapokea mshahara anapaswa kupokea mafao na kwa sababu kustaafu sio dharura, anakuwa ameshajua na ninyi mmepewa taarifa miezi kadhaa nyuma. Kwa hiyo, badala ya mwajiri, sasa anapelekwa huku ilipoenda michango na hili ulilolisema la changamoto ya michango ya mwajiri tulilisemea hapa ndani na tumaini ni mojawapo ya marekebisho mnayoleta.

Kwa kweli sio kazi ya mfanyakazi kufuatilia michango kama mwajiri anapeleka au hapeleki, kwa sababu yeye hana uwezo wa kujua, hana uwezo wa kumfuatilia huyu mwajiri la sivyo atafukuzwa kazi. Kwa hiyo, hili nalo muangalie namna ya kulifanyia kazi kwa kweli. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Karibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, hilo la siku 60 ambazo tumeziweka kisheria ukweli ni kwamba hata siku moja kama nyaraka zake na taarifa zote zipo sahihi na wanalipwa wapo wengine siku tatu, siku nne. Hizo 60 tumeweka tu *threshold* ambayo ndani ya kipindi hicho mstaafu

huyo asiweze kupata shida. kwa hiyo, analipwa wakati wowote anapostaafu.

Mheshimiwa Spika, la pili la kuhusiana na zile asilimia, ni Bunge lako Tukufu liliamua kwamba tuweke *interest* kwa yule ambaye anachelewesha michango na tumekwishafanya hivyo kwenye sheria zinazohusiana na watumishi wa umma, lakini pia kwa upande wa *private sector;* na moja ya sehemu ya marekebisho ni pamoja na huu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ambao tunauleta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kuna hatua kali pia ambazo tunaendelea kuzichukua za kuwafikisha mahakamani, pia kutakuwa na pendekezo la kuhakikisha kwamba yule ambaye hata akipelekwa mahakamani maamuzi yafanyike kwa *summary procedure* na zaidi ya hapo alipe kwanza fedha ndipo aweze kusikilizwa ili kulinda hali ya wanachama wetu huko. Zamani ilikuwa wanatafuta sana *procedure* ya kupata ruhusa ya mahakama ili aweze kusikilizwa wakati mwanachama wetu anazidi kuumia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa Tarime Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Susuni Tarime Vijijini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Susuni, Jimbo la Tarime Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Susuni iliyopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ina jumla ya Vijiji vitano (5) vya Matamankwe, Kiongera, Keroti, Kikomili na Nyabilongo. Kati ya vijiji hivyo, Vijiji viwili vya Matamankwe na Kiongera vina zahanati.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuipandisha hadhi Zahanati ya Kiongera kuwa Kituo cha Afya, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepeleka fedha shilingi milioni 207 kwenye zahanati ya Kiongera kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi lenye huduma ya upasuaji wa dharura na jengo la maabara.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri itatenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu iliyosalia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la kufulia, jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* na jengo la wodi ya kulaza wagonjwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; hii Kata ya Susuni, Kijiji cha Kiongera ndiyo eneo ambalo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alitoa fomu humu ndani Wabunge wote tukajaza kuomba vituo vya afya. Nikaenda kwenye kata hii nikafanya mkutano wa hadhara nikawaahidi kwamba sasa Serikali inajenga kituo cha afya hapa. Sasa nataka nijue kwamba kwa majibu haya huo mpango haupo kabisa, tukawaambie kwamba hicho kituo hakijengwi au kutakuwa na majibu mengine katika swali hili hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba mwaka wa fedha ujao 2025/2026 halmashauri itapeleka milioni 150 katika eneo hili. Lakini anasema wataboresha

jengo la kufulia, jengo la *OPD* na wodi, jengo la kufulia linachukuwa mpaka milioni 187, *OPD* milioni 180 mpaka 187, wodi ni milioni 250. Je, Serikali wapo tayari kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime *DC* kupitia mapato ya ndani apeleke fedha zote hizi ili kituo cha afya kijengwe Kiongera kwa sababu katika eneo hilo hakuna huduma ya afya na amesema mwenyewe kata ina vijiji vitano…

**SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nimeshauliza eeh?

**SPIKA:** Umeshauliza maswali mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, ni kweli baada ya Serikali kuweka dhamira ya kujenga vituo vya afya kwenye kila Jimbo Mheshimiwa Mbunge alileta mapendekezo ya Kata hii ya Susuni na sisi kama Serikali tayari tumeshaiweka kwenye orodha ya kata ambazo zitapata fedha kwa ajili ya kujenga kituo hiki cha afya. Kwa hiyo, kwanza mpango wa kujenga kituo cha afya hiki kupitia kituo cha afya kila jimbo upo pale pale. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba kituo cha afya kinahitaji majengo mengi zaidi na shilingi milioni 150 haitatosha kukamilisha majengo yote, lakini safari ni hatua tumeanza na majengo haya, tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha majengo mengine.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumsisitiza pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime Vijijini kwamba kadri mapato ya ndani yanapopatikana tunaweza kuongeza fedha

kutoka milioni 150 na kupeleka fedha zaidi kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hiki. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kata ya Nanda, Kata ya Nyakafuru hazina vituo vya afya. Natambua Serikali ina mpango kila Mbunge kutupa kituo cha afya, sasa swali langu lini Serikali itatoa pesa ili kusudi vituo hivyo viweze kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Kata hii ya Nanda na kata nyingine ambayo Mheshimiwa Maganga ameitaja katika Jimbo la Mbogwe ni miongoni mwa kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Pia, Kata ya Nanda ni miongoni mwa kata ambazo zimeorodheshwa kwa ajili ya kupata fedha baada ya Mheshimiwa Mbunge kuainisha kwamba, ni kata ya kipaumbele. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua uhitaji wa vituo vya afya na Wananchi wa Mbogwe wawe na imani kwamba, Serikali inatafuta fedha, kwa ajili ya kwenda kujenga vituo hivyo kwa awamu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majibu kwa maswali kwa kifupi na moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya kwenye Kata ya Bubiki, Wilaya ya Kishapu, kata hii ambayo ina vijiji vinne na watu takribani 15,000? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata ya Bubiki katika Jimbo la Kishapu ni moja ya kata ambazo zina idadi kubwa ya wananchi, zaidi ya 15,000 na Mheshimiwa Mbunge alifanya mkutano wa hadhara wiki moja iliyopita na akatoa hoja hiyo. Namhakikishia tu kwamba, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeshapokea hoja hiyo na tunaelekea kutafuta fedha, kwa ajili ya utekelezaji, ili kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum pamoja na Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa jimbo hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kituo cha Afya Mwandoya ni kikubwa sana, lakini hakina uzio. Je, ni lini Serikali itajenga uzio katika kituo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Mwandoya ni miongoni mwa vituo vya afya ambavyo vimepokea fedha, kwa ajili ya kuboresha miundombinu. Serikali iliweka kipaumbele kwanza kwa kukamilisha majengo ya huduma za afya kwa wananchi ambapo wodi na majengo mengine kwa kiasi kikubwa yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, sasa awamu inayofuata, tutaendelea kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya kujenga uzio katika kituo kile. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya cha Kata ya Ukumbi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kata ya Ukumbi kimepokea fedha awamu ya kwanza na kinaendelea na ujenzi na nafahamu kwamba, kinahitaji fedha nyingine takriban shilingi milioni 250, kwa ajili ya ukamilishaji na Mheshimiwa Nyamoga amefuatilia mara kwa mara. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipo kwenye mpango wa vituo ambavyo vinahitaji fedha, kwa ajili ya ukamilishaji na mara fedha zikipatikana tutahakikisha tunapeleka ili kituo kile kiweze kukamilishwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, je, nini mpango wa Serikali wa kupeleka fedha kwa haraka Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili wakajenge Kituo cha Afya katika Kata ya Likawage?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya katika kata mbalimbali zikiwemo kata katika Jimbo na Wilaya ya Kilwa, lakini nafahamu kwamba, kuna uhitaji wa vituo vya afya katika kata ambazo pia, Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Namhakikishia tu kwamba, Serikali inaendelea kujenga vituo hivi kwa awamu na mara fedha zikipatikana tutahakikisha pia, tunapeleka katika Kata hiyo ya Likawage ili tuweze kujenga hicho kituo cha afya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, je, nini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka fedha, shilingi milioni 200 kwenye Kata ya Bungu ili kukamilisha kile kituo cha afya? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, vituo vyote vya afya ambavyo vilipokea fedha chini ya shilingi milioni 500, vimewekwa kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu 2024/2025, lakini vipo ambavyo vitawekwa kwenye Bajeti ya 2025/2026 ikiwemo Kata ya Bungu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Zahanati zetu nchini, nyingi sana hazina vifaa vya maabara. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha zahanati zetu zinakuwa na vifaa vya maabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imepeleka zaidi ya shilingi bilioni 250 katika Sekta ya Afya ya Msingi, kwa ajili ya kununua vifaa tiba na hivi leo halmashauri zote 184 zimepokea kati ya shilingi milioni 700 hadi shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, bado kuna mahitaji ya vifaa tiba kwenye baadhi ya zahanati. Hii imetokana na kasi ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na hospitali mpya zimekuwa nyingi, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwenye bajeti ya mwaka huu imetengwa zaidi ya shilingi bilioni 55, kwa ajili ya vifaa tiba na tutahakikisha zahanati zote, vituo vyote na hospitali za halmashauri zenye upungufu wa vifaa tiba zinapewa kipaumbele kupewa fedha hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Tenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN SELEMAN MTENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatupa fedha za kujenga jengo la Manispaa ya Mtwara Mjini ambalo limejengwa takriban miaka ya 60 iliyopita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, jengo la Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ni kongwe na tayari Mheshimiwa Mbunge alishaleta taarifa hiyo na halmashauri walishawasilisha gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo. Namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, kwenye bajeti ambazo tunaendelea kutenga kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutatoa kipaumbele, kwa ajili ya jengo la Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali linalofuata ni la kwako au ni la Naibu Mwingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Ni la Mheshimiwa Katimba.

Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Ujenzi wa Daraja la Mafusi Kata ya Itenka – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mafunsi, Kata ya Itenka – Nsimbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa ujenzi wa Daraja la Mafunsi, Kata ya Itenka – Nsimbo. Mwaka 2023/2024 daraja hili lilifanyiwa usanifu ambapo gharama zinazohitajika zilikuwa ni shilingi bilioni 2.3.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua za mwaka 2023/2024, Wakala unapitia usanifu uliofanyika ili kujiridhisha kutokana na hali ya wingi wa maji uliobainika kwenye kipindi cha mvua za *El-Nino*. Kazi ya kupitia usanifu inaendelea kukamilishwa na inatarajia kukamilika mwezi wa Septemba, 2024 na mara itakapokamilika taratibu za ujenzi zitafuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri, lakini nina maswali ya nyongeza.  Swali la kwanza; kwa kuwa, daraja hili ni muhimu sana kwa wananchi wa Kata ya Itenka. Mashamba na shughuli zao zote za kijamii ziko ng'ambo ya mto na kipindi cha masika hakuna watoto wala wananchi wanaokwenda kufanya shughuli zao za kijamii. Je, ni lini Serikali itajenga daraja hili ili wananchi wa Itenka waweze kupata maisha mazuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, je, yuko tayari Bunge hili likiisha twende naye Itenka ili akaone uhalisia na shida ya wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maana anapigania maslahi mapana ya wananchi wake. Naomba nimhakikishie kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa daraja hili kuichumi na kijamii. Ndiyo maana Serikali imechukua hatua ya kufanya mapitio ya usanifu ili daraja litakapojengwa liwe la kudumu na liwe lina ubora ambao utakuwa ni wa muda mrefu zaidi na utawasaidia wananchi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara

baada ya mapitio ya usanifu kukamilika, Mwezi wa Tisa, taratibu za ujenzi zitaanza. Kwa hiyo, katika mwaka huu wa fedha, daraja hili litajengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Tayari tulishanong'ona na ameshaniomba niweze kwenda kutembelea katika jimbo lake, niweze kwenda kujionea uhalisia katika eneo hili la Kata ya Itenka. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nipo tayari, tutakaa na tutakubaliana ratiba ili niweze kufika katika eneo hili.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali kwa kifupi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Kigogwe katika Kata ya Munzeze? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa sana wa madaraja haya na hasa kwa maslahi mapana ya wananchi kiuchumi na kijamii, Serikali tayari imeshaanza jitihada mbalimbali za kuhakikisha inajenga madaraja haya ili wananchi waweze kuyatumia. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kuleta fedha ili kuhakikisha daraja hili ulilolitaja katika Kata ya Munzeze liweze kujengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali kwa kifupi.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Daraja linalounganisha Barabara ya Mwamanyili na Mwamkala litakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombimu na hasa ya barabara zetu katika ngazi za Wilaya, yaani kwa maana barabara zinazosimamiwa na *TARURA*. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuleta fedha, kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hii ikiwemo daraja hili alilolitaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Madeni ya Wazabuni Wanaotoa Huduma za Vyakula Mashuleni**

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa madeni ya Wazabuni wanaotoa huduma za vyakula kwenye shule mbalimbali tangu Mwaka 2023 hadi 2024? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipokea madeni mbalimbali ya wazabuni wa chakula kwa shule za msingi na sekondari za Serikali kutoka katika halmashauri zote. Madeni hayo yamekuwa yakilipwa baada ya uhakiki na kadri ya upatikanaji wa fedha. Mwaka wa Fedha 2020/2021 – 2022/2023, Serikali imelipa wazabuni wa chakula shuleni kiasi cha shilingi bilioni 26.3.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekusanya madeni ya wazabuni wa chakula katika shule za msingi na sekondari yenye jumla ya shilingi bilioni

21.7 (shule za msingi shilingi milioni 761.8 na shule za sekondari shilingi bilioni 20.9). Madeni haya yamewasilishwa Hazina, kwa ajili ya taratibu za uhakiki na malipo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; fedha inayotengwa kumlisha mwanafunzi kwa siku ambayo ni shilingi 1,500 na zaidi kidogo haitoshi kuweza kumpa milo mitatu, kwa maana ya mlo kamili *(balanced diet)*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza hicho kiasi ili kusudi kiweze kulingana na hali halisi ya maisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kiasi ambacho kilishalipwa, lakini madeni ya wazabuni wa vyakula mashuleni bado ni makubwa na mengine bado yako kwenye halmashauri, hayajafika hata Wizarani. Je, Serikali mna mpango gani wa kuhakikisha kwamba, sasa wanaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, hayo madeni yanalipwa kila mwezi ili yasiendelee kurundikana kule? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ambaye ameuliza maswali mazuri kabisa haya kwamba, kiwango cha fedha, kwa ajili ya kununua chakula cha wanafunzi katika shule kimepandishwa, kimeboreshwa kutoka shilingi 1,500 kwa mwanafunzi mmoja mpaka shilingi 2,000. Kwa hiyo, Serikali itakuwa inahakikisha inafanya mapitio ya gharama hii ili kuweza kuiboresha zaidi kwa kadri muda unavyozidi kwenda na kwa kadri bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, pia, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Fedha itaendelea kuhakikisha kwamba, fedha zote zile ambazo zinakuwa zimetengwa zinatolewa zote kulingana na

idadi ya wanafunzi wa bweni walioko katika shule zetu hizi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imefanya mapitio ya gharama hizo na itaendelea kufanya mapitio zaidi, ili kuendelea kuboresha kiwango.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba, inalipa wazabuni. Kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 mpaka 2022/2023, Serikali tayari imelipa wazabuni wa chakula shuleni kiasi cha shilingi bilioni 26.3. Kwa muktadha wa swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kutoa maagizo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote ambazo zina shule za bweni wafanye uhakiki wa madeni yote ya wazabuni wa chakula na waweze kuyawasilisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuweze kuyawasilisha Wizara ya Fedha, kwa ajili ya taratibu za malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali kwa kifupi.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Shule nyingi za Sekondari Mkoani Tanga zina maeneo makubwa yanayofaa kwa kilimo ambayo yangesaidia kupata chakula cha mchana kwa wanafunzi. Je, ni lini Serikali itatoa waraka maalum kwa walimu wa Mkoani Tanga, ili maeneo hayo yatumike vizuri, kwa ajili ya chakula cha mchana kwa wanafunzi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, nani anayepaswa kulima kati ya wanafunzi na walimu ili niwe nimeelewa swali lako vizuri?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi la kwenye hili swali Namba 43 linazungumzia chakula ambacho...

**SPIKA:** Hilo limeeleweka, yaani muktadha wa swali lako, umesema walimu waelekezwe ili yale maeneo yatumike vizuri;

kwa maana ya kutafuta wakulima wa kulima? Ama yale maeneo walime walimu ama walime wanafunzi?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, vyovyote iwavyo, lakini maeneo yatumike vizuri. Yanakuwa ni kama vile sehemu ya elimu ya kujitegemea, lakini pia, shule ziwe na miradi ili kuepusha huu mzigo wa Serikali kuwalipa wazabuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa lishe na hasa katika ustawi wa wanafunzi wetu. Kwa hiyo, kwa muktadha wa swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nichukue nafasi hii kuendelea kuwahamasisha Wakuu wa Shule waweze kuwa wabunifu, kuanzisha vibustani vidogo vya matunda, mbogamboga na mazao madogo ili waweze kuchangia katika lishe za wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge dhamira yake ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, shule zetu hizi na zenyewe kwenye maeneo yao wanaweza kuwa wabunifu na kuanzisha vimiradi vidogo ambavyo vitasaidia katika lishe za watoto ambazo ni muhimu sana katika makuzi yao katika kupata afya ambayo itawawezesha kupokea masomo vizuri.

**SPIKA:** Yeye amezungumzia mashamba makubwa, kwa maana ya kwamba, hizo shule zilizoko Mkoa wa Tanga zina mashamba makubwa. Hii ya kulipa wazabuni ni kwa sababu, yale mashamba kwa swali lake yeye hayatumiki, maana yake yapo tu. Si ndiyo Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge? Nimekuelewa vizuri? Yale mashamba kwa sasa hayalimwi, yaani hayazalishi chochote?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ni sawa. Mheshimiwa Waziri ameliweka vizuri zaidi swali langu.

Mantiki halisi ni hiyo aliyoisema. Nimesema maeneo makubwa, lakini hayatumiki vizuri walau kuondoa changamoto ya chakula.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha ngoja tuelewane vizuri. Maeneo makubwa halafu bustani ndogo? *(Kicheko)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, maeneo hayo makubwa yanaweza pia, yakawa na bustani ndogondogo nyingi. Inawezekana pia.

**SPIKA:** Nimeuliza hapa, ili nani alime? Ndiyo nadhani mwanzoni hamkunielewa vizuri kwa nini nilikuwa nafafanua nani alime?

Maana kuna watu tumesoma shule za kulima mashamba. Sasa kama unataka Mheshimiwa Waziri aseme walimu wasimamie wanafunzi walime, Mbunge uwe wazi ili Mheshimiwa Waziri ajue anatoa maelekezo gani. Ndiyo maana na yeye kajielekeza kwenye bustani ndogo, walimu wasimamie, maana sisi tena tunataka tuwape kazi walimu ya kusimamia mashamba makubwa ambayo watakuwa wanalima wanafunzi. Ndiyo maana nilitaka kuelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, ulikusudia mashamba madogomadogo walime bustani au yale mashamba makubwa walime, kwa ajili ya hawa wazabuni ambao wewe mwenyewe umewasema, kwamba, wazabuni hawa si wanaleta mahindi, unga na maharage, sasa hayo yanalimwa kwenye bustani kweli? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mantiki halisi ni kwamba, *whether* ni mashamba madogomadogo au ni mashamba makubwa, lakini walime. Mimi nimesoma *Tanga School* na ni mjini na tulikuwa tunaweza kutoa magunia 100, lakini utashangaa unakwenda Maramba, vijijini ambako wanasema watoto wanakosa chakula cha mchana na wana maeneo makubwa ya kuweza kupata chakula. *Those are logics behind my question. (Makofi)*

**SPIKA:** Sasa utaelewa, ndiyo maana nilikwambia unazungumzia mashamba makubwa. Maana hapa umeshasema unaenda kijijini wana mashamba makubwa. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani umeielewa hoja?

Ninyi mchukue hiyo hoja yake mkaichakate. Shule ambazo zina mashamba makubwa kama yatakodishwa, yaani yafanye kazi badala ya kukaa tu halafu wanafunzi wanakuwa pengine chakula hakitoshelezi ama kama kinaweza kutosheleza basi chote ni cha kununua. Kama kitatoka kwenye mashamba yao maana yake kitakuwa bei rahisi, lakini hoja ya wanafunzi kurejea kule tulikokuwa sisi kwenye kulima wanafunzi kwenye mashamba makubwa, sasa hiyo itakuwa ni hoja nyingine tofauti. Tusije tukachanganya mambo hapa. Ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri, uichukue hiyo hoja mkaichakate vizuri muone namna bora ya kuendesha yale mashamba.

Tunaendelea, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Uwiano wa Mwalimu na Mwanafunzi Nchini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, upi uwiano wa mwalimu na mwanafunzi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, uwiano wa mwalimu na wanafunzi kwa shule za msingi mwaka 2024 ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 64 (1:64). Aidha, kwa upande wa shule za sekondari mahitaji ya walimu yanazingatia idadi ya masomo yaliyopo katika shule husika ambapo mwalimu anatakiwa kufundisha masomo

yasiyozidi mawili na vipindi visivyozidi thelathini kwa wiki katika mkondo mmoja wenye wanafunzi 40.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shule za sekondari hakuna uwiano halisi wa jumla kwa mwalimu na wanafunzi kwa masomo yote kwa kuwa kila somo lina idadi ya vipindi tofauti na somo lingine. Serikali imekuwa ikifanya jitihada kuajiri walimu wa elimu ya msingi na sekondari ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba uwiano wa walimu nchini upo chini ya kiwango kinachostahili, je, Serikali sasa ipo tayari kuchukua suala hili kuwa kipaumbele maalum cha Taifa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa yapo maeneo ambapo shule zetu za sekondari hazina kabisa walimu wa kike, je, Serikali ipo tayari sasa kuweka kipaumbele katika ajira za walimu kwa wanawake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua upungufu wa walimu na imekuwa ikifanya jitihada za kuajiri walimu kila mwaka. Mathalani mwaka huu kuna ajira tayari zimetangazwa 11,015 za walimu na Serikali inachukua jitihada mbalimbali ikiwemo pia matumizi ya TEHAMA katika kufundishia kwa maana kutumia *smart classes*. Pia kutumia walimu wa kujitolea pamoja na kuwatumia walimu wale ambao wapo kwenye mafunzo kazini (wale wanaofanya *internship)* ambao mwaka wao mmoja wa masomo wanatakiwa wafanye mafunzo, sasa waanze kuingia katika shule wakifanya mafunzo kwa vitendo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa na inaweka kipaumbele

katika kuhakikisha inapata walimu na inapunguza ukali wa upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge naomba nichukue nafasi hii kuwahamasisha waombaji wa ajira hizi za ualimu ambao ni wanawake wajitokeze kwa wingi waombe ajira hizi kwa sababu ajira za walimu ni kwa ajili ya wanawake lakini wanaume. Kwa hiyo wanawake wajitokeze na waombe nafasi hizi za ualimu ili tuweze kupata wanawake wengi zaidi katika nafasi za walimu pia. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nadhani tukiendelea kuwahamasisha wanawake wakajitokeza kwa wingi wakaomba nafasi tutaweza kuongeza idadi ya walimu wanawake ambao tunawahitaji pia.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Ndulane, swali kwa kifupi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto ya uhaba mkubwa wa walimu katika Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali tayari imeshatangaza ajira mpya za walimu katika mwaka huu ajira 11,015, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mgawo wa walimu hawa na yeye atapata walimu hawa katika jimbo lake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu Wilaya ya Nyasa imekuwa na matokeo mabaya sana ya kidato cha nne katika yale masuala ya upimaji na changamoto kubwa ni walimu wengi wanahama kuliko ambao wanabakia kwenye maeneo. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti wa kina kwenye hizi wilaya za vijijini ili kupata

mkakati maalum wa kuhakikisha watoto wa maeneo hayo nao wananufaika na elimu ya Tanzania kuliko hali ilivyo sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza Ofisi ya Rais, Utumishi imeshatoa mwongozo kwamba mtumishi anapopangiwa kituo cha kazi haruhusiwi kuhama kwenye kituo hicho cha kazi mpaka awe ametimiza angalau miaka mitatu. Kwa hiyo hiyo ni jitihada moja ambayo inafanywa na Serikali kuhakikisha maeneo ya pembezoni hayapati changamoto kubwa ya walimu au watumishi kuhama.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kuchukua jitihada ya kuboresha mazingira ya kufundishia na hasa katika maeneo ya pembezoni ili kupunguza ile changamoto ya watumishi kuhama na kwa muktadha wa swali lako yaani walimu kuhama katika maeneo ya pembezoni kwenda kutafuta mazingira bora zaidi ya kufanya kazi. Kwa hiyo Serikali inatambua changamoto ya ukosefu au kuhama kwa watumishi na hasa walimu kutoka katika maeneo ya pembezoni na tayari Serikali inachukua jitihada mbalimbali ili kuhakikisha maeneo hayo hayapati upungufu huo kwa kutengeneza mazingira ambayo watumishi na walimu wataweza kuendelea kubaki kuwafundisha watoto wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kaa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge hapa mbele nikawa nakumbuka jana liliulizwa swali na Mheshimiwa Mbunge mwingine (Mheshimiwa Kamani) kuhusu waajiriwa kutunza ndoa kitu kama hicho na yalikuwepo maswali ya nyongeza yakipelekea huko. Leo linaulizwa swali kwamba kuna maeneo watu wanahama.

Mimi nafikiri jambo hili Ofisi ya Rais, Utumishi na TAMISEMI siku moja mkajipange vizuri tuje tukae tujadili jambo hili sisi kama Taifa tunataka nini. Kwa sababu huyu anayehama kwenda kumfuata mwenza wake ile nafasi yake Serikalini bado imejaa kule hatafutiwi mtu mwingine wa kwenda na wakati huo huo huduma

kule inahitajika. Sasa tunataka nini sisi kama wawakilishi wa wananchi, tunataka watu wakae pamoja tulinde maadili, tunataka watu wapate huduma kule ambapo huyu amepangiwa kazi ama tunataka nini? Kwa sababu na sisi pia tunaivuta Serikali upande huu, upande huu, kwa hiyo majibu wanatupa kwa kadri tunavyouliza maswali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo hili jambo walichukue kwa mapana hayo kwa sababu la si hivyo tutaendelea kuuliza. Leo tutauliza mume wangu yupo mbali, mke wangu yupo mbali, familia inavunjika na ndoa zinavunjika. Mwingine atakuja kusema walimu kwake hakuna, watumishi wa afya hakuna sijui nani kahama kwa hiyo tutajichanganya sisi wenyewe. Nafikiri ni jambo ambalo tunaweza kulijadili kwa pamoja kama wawakilishi wa wananchi ili tutoe sasa mawazo yetu kwa Serikali namna ya kwenda nalo kwa sababu hata hili la miaka mitatu halitoshelezi kwa kweli. Wilaya kama huko Nyasa hata akikaa miaka mitatu ukamwondoa sasa yeye kule atabaki na nani, kwa hiyo na yenyewe haimfanyi yeye awe na watumishi wa kutosha. Kwa hiyo nafikiri ni jambo kidogo ambalo limekuwa likijitokeza na sisi wenyewe tunajichanganya tunataka nini hatueleweki.

Kwa msingi huo, niwaombe sana upande wa Serikali Ofisi ya Rais, TAMISEMI mkae pamoja na Utumishi ili sisi Waheshimiwa Wabunge tukae pamoja mtuelezee ya kwenu kuhusu kuhama, mtueleze ya kwenu kuhusu ajira halafu tutoe ushauri wa jumla ili haya maswali yasiwe yanajitokeza kila wakati.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo ya vijijini au pembezoni hali ni mbaya zaidi ambapo unakuta mwalimu mmoja ana uwiano wa wanafunzi 90 mpaka 120 kinyume na Sera ya Elimu ambao inasema wanafunzi 40 kwa mwalimu mmoja na maeneo ya mjini uwiano walau ni mzuri kidogo; na kwa kuwa Serikali ina *program* ya TEHAMA, je, ni kwa nini sasa isichukue walimu kutoka mijini iwapeleke vijijini maeneo ya pembezoni ili kuweza ku-*balance* kuhakikisha watoto wote

wanapata elimu sawa kwa sababu huku mjini wanaweza wakatumia TEHAMA kuweza kufundisha wanafunzi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu katika jibu la msingi ni kwamba Serikali inafanya jitihada kuhakikisha inapunguza upungufu wa walimu na inatumia jitihada tofauti tofauti kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge kwamba pia kuna matumizi ya TEHAMA. Tayari tumeshaanza kufanya majaribio katika baadhi ya maeneo Mkoa wa Dodoma kwa hiyo tutaendelea kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia kama hizi yaani *smart classes*.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu pia tunaendelea kuzikumbusha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza pia kutumia namna ya kuchukua walimu wale wa kujitolea ambao wanapewa posho kidogo kwa hiyo wanaweza kuwafundisha wanafunzi wetu na kupunguza kwa kweli ukali wa upungufu wa walimu. Pia nimesema tunatumia njia nyingine ya walimu ambao wapo katika mafunzo kwa vitendo *(internship)*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua upungufu na hasa katika maeneo haya ya pembezoni na inachukua hatua hizi mbalimbali. Kwa hiyo nimhakikishie hata katika maeneo yake ya utawala anapowakilisha katika mkoa wake tutaendelea kuwafikia kwa awamu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest.

Na. 45

**Mkataba wa Gesi Asilia Kuwasilishwa Bungeni**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, lini Mkataba kati ya Tanzania na Wawekezaji wa Gesi Asilia wenye thamani zaidi ya shilingi trilioni 70 utaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Kampuni za Nishati za Kimataifa *(International Energy Companies)* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG)*. Kwa kuwa majadiliano bado yanaendelea, yakikamilika tutaendelea na hatua inayofuata.  Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Majibu yanasema Serikali inaendelea na majadiliano, hivyo niiombe Serikali kutoa *commitment* kwa kuwa imeshatangaza kusitisha matumizi ya kuni na hasa kwenye taasisi na matumizi ya Gesi ya *LPG* ni gharama. Tungetaka kauli ya Serikali itakamilika lini kwa sababu ilivyo kwa sasa inaweza kuchukua muda mwingi na sijui hatima yake.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa matumizi ya gesi nchi nzima kwa sasa wananchi wengi wanatumia *LPG, LPG* ni gesi ambayo ni ghali na Serikali haitumii Mfumo wa *Bulk Procurement*. Nataka kauli ya Serikali juu ya kutumia mfumo huu ambao utaweza kusaidia ku-*regulate price* tofauti na ilivyo leo

ambapo wauzaji ndiyo wanaoweza ku-*determine price* tofauti na ilivyo kwenye bidhaa nyingine ya petroli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, moja kuhusiana na lini majadiliano haya ya Mradi wa *LNG* yatakamilika, mradi huu ni mradi wenye manufaa makubwa sana kwa Taifa letu. Majadiliano haya ni muhimu kwa sababu ndiyo ambayo yanaweka msingi wa kodi, mirabaha pamoja na ulinzi wa vigezo vya sisi kunufaika kiuchumi. Kwa hiyo nataka niwahakikishie suala la Mradi wa *LNG* ni kipaumbele katika Serikali na majadiliano haya yanaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ni lini? Nitashindwa kusema tarehe mahususi, lakini nataka niwahakikishie ni kipaumbele na tunafanya kazi hii kwa weledi mkubwa sana kuhakikisha majadiliano yanaendelea vizuri, yanakamilika na mradi unaenda kutekelezwa. Nataka niwahakikishie suala hili Mheshimiwa Mbunge kwa kweli tumejizatiti kuhakikisha tunafanya majadiliano ya maslahi kwa Taifa na mwisho wa siku yanakamilika na mradi kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili la kuagiza gesi ya *LPG* kwa Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja *(Bulk Procurement System - BPS)*. Kwa kweli ni wazo zuri na sisi tunalichakata, lakini unafuu wa bei ama uuzaji wa bei kwa kweli *EWURA* wanachokifanya soko halipo huru, hivyo ni tunahakikisha soko linakuwa himilivu ili kuhakikisha bidhaa inaweza kusambaa na inapatikana kwa urahisi. Suala la *BPS* lina vigezo mbalimbali ikiwemo kwa sasa hivi tunaenda kujenga gati ambalo litatuwezesha kuleta meli kubwa za *LPG*. Kwa hiyo tutaendelea tathmini kadri ambavyo tunaendelea kuwekeza kwenye kuleta gesi hii ili kuhakikisha tunaenda kutumia Mfumo huu wa *BPS* lakini ni wazo ambalo tunalichakata na tutaenda kulifanyia kazi

kulingana na mahitaji ya soko, lakini kwa kadri vile tunavyoenda kuboresha miundombinu ya kuleta gesi nchini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Barabara ya Mchepuko – Babati**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi wa Babati waliopisha ujenzi wa barabara za mchepuko takribani miaka minne iliyopita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, baada ya usanifu wa kina na uthamini wa mali zitakazoathiriwa na Mradi wa Barabara ya Mchepuo wa Mji wa Babati *(Babati Bypass)*, tathmini ilionesha kwamba barabara pendekezwa ya *Babati Bypass* yenye urefu wa kilometa 27 inapita katika maeneo ya Mji wa Babati yenye nyumba nyingi na kusababisha gharama ya fidia kuwa kubwa kiasi cha shilingi bilioni 9.05. Kutokana na hali hiyo, Serikali imemwelekeza Mhandisi Mshauri kupendekeza njia nyingine mbadala ambayo itapita nje ya Mji. Hivyo, fidia kwa njia ya awali imesitishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul kumbe umeketi huna swali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yana ukakasi barua aliyoiandikia *TANROADS* Mkoa wa Manyara alimwandikia meneja kwamba kwa kuwa wananchi hawa wamekaa zaidi ya miaka mitano wakipisha eneo hilo wale wanaodhani wameathirika na wanahitaji fidia wapeleke majina yao ili wazingatiwe katika fidia, leo ananiambia fidia hii imesitishwa, imesitishwa lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa jambo hili limegusa nusu nzima ya wananchi wa Jimbo la Babati Mjini maana yake ni mchepuo wa Singida, Dodoma na Arusha, lile jimbo lote. Naomba busara yake kwa nini yeye au Mheshimiwa Waziri wasiwatembelee wananchi wa Jimbo la Babati Mjini ili jambo hili liishe kwa amani?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majibu Kanuni huwa zinataka majibu yawe ni ya kutosheleza. Mheshimiwa Gekul wakati ukianza kuuliza maswali yako ya nyongeza umesema majibu yana ukakasi nataka kujua yana ukakasi kwamba hayajajibu swali lako ili nianze kushughulika na hilo kwanza kabla sijampa nafasi ya kujibu maswali yako ya nyongeza, yaani kwamba swali ulilouliza na kilichojibiwa ni vitu viwili tofauti.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kwa sababu majibu ambayo sisi tumeletewa kwenye Mkoa ni kwamba *TANROADS* waendelee kuwaita wale wananchi walioathirika ili Serikali iangalie namna ya kuwafidia. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema fidia hii imesitishwa, ndiyo maana nikasema majibu yana ukakasi, kwa nini asirudi tu ndani kuangalia majibu yake ya awali ili tumalize jambo hili.

**SPIKA:** Sawa, sasa tuelewane vizuri. Hapa kwenye swali linasomeka je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi halafu linaendelea. Serikali inasema imemwelekeza Mhandisi Mshauri kupendekeza njia nyingine mbadala ambayo itapita nje ya mji maana yake inawakwepa hawa watu, hivyo fidia kwa ajia ya awali imesitishwa, kwa sababu huku juu wewe

uliuliza Serikali ina mpango gani kwa hiyo mpango wake imesitisha kupitisha hapo barabara.

Sasa nielezee mimi ni namna gani hili swali halijajibiwa ili lijibiwe ndiyo uulize swali ya nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni Sheria zetu za nchi hii kwa masuala ya fidia zipo wazi. unapo-*acquire* eneo la mtu hata kwa miezi sita mpaka miaka mitano wananchi wamesubiri na waliandikiwa barua za kusitishiwa maeneo hayo wasiendeleze. Fidia ninayozungumzia na wananchi hawa wanaozungumzia baada ya Serikali kuona kwamba shilingi bilioni tisa hawawezi kufidia, sheria inasemaje sasa waweze kuangalia kwa kupisha maeneo yao kwa miaka mitano?

**SPIKA:** Sawa, sasa ili taarifa zetu za Bunge zikae vizuri kama hiyo ndiyo lilikuwa lengo lako siyo kwamba majibu waliyotoa Serikali hayajibu swali lako yanajibu isipokuwa wewe una maswali yako ya nyongeza kwamba hawa watu nyinyi huu ndiyo mpango wenu wa kusitisha, lakini wamewasubiri kwa muda mrefu, mna mpango gani? Ndiyo swali lako la nyongeza la kwanza.

Swali la pili ni hilo sasa ulilouliza. Ukishaanza na ukakasi maana yake tuanze kwanza kushughulika na jibu lipo ama halipo. Kwa hiyo kwa sasa tukubaliane jibu hili lipo sawasawa, sasa wewe una maswali yako hayo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, njia iliyokuwa imependekezwa kwa kuwa imesitishwa, lakini kama alivyosema Mbunge, Sheria ya Utoaji Ardhi, Sura ya 118(19)(1) kimeelezea taratibu za namna ya ku-*deal* na suala kama hili pale ambapo wale uliokuwa umewasimamishia ama

umewasababishia usumbufu unatakiwa ufanye. Kwa hiyo taratibu hizo zimeainishwa kwenye hiyo sheria na zitafuatwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara kutembelea tuko tayari kwenda kuangalia, lakini pia nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali siyo kutoa usumbufu kwa wananchi, nia ya Serikali kimsingi ni kuwapelekea maendeleo, kuwatengenezea miundombinu bora. Ndiyo maana baada ya kuona tutavunja nyumba nyingi, lakini pia kwa mji ulivyopanuka, barabara iliyokuwa imependekezwa ni kama inaenda sambamba na barabara iliyopo, kwa hiyo tunaona tufanye jambo kubwa zaidi kuliko hili ambalo lipo. Kwa hiyo, nia si kuwasumbua na kama watu watakuwa na haki kwa kutumia hii sheria haki yao watapewa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bunda na Majimbo mengine ya Mkoa wa Mara kuna barabara kuu ambazo watu wameongeza kwenda mita 30 na *TANROADS* imeshaweka vigingi na vile vigingi wananchi hawajalipwa. Ahsante.

**SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Je, ni lini sasa wale watu watafidiwa kwenye barabara zilizoongezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baada ya mabadiliko ya sheria kutoka mita 45 kwenda mita 60 kumekuwa na ongezeko la mita 7.5 kila upande na tulishaweka alama kuonesha *corridor* ama ushoroba wa barabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini kama Wizara imeonekana kwamba gharama ya kulipa fidia ni kubwa sana ambayo ni zaidi ya shilingi trilioni saba. Wizara tumeshaanza kufanya kazi ya kufanya tathmini kama kweli hizo shoroba zote zinahitajika na tunaweza tukazilipa kwa wakati, kazi hiyo inaendelea ili tuweze kupeleka Serikalini, tuwe na tamko kwamba yale maeneo ambayo kweli tutayahitaji ndiyo ambayo tuweze kuyafidia kwa mita 60 na yale ambayo tunadhani, kwa mfano barabara hizo za mikoani ambazo tuna uhakika hata kama unataka corridor yaani *carriage way* ya njia mbili mbili bado mita 45 tutaweza, baada ya kukamilisha hiyo tathmini Serikali tutatoa tamko kuhusu namna ya kutoa fidia kwenye hayo maeneo ambayo yameongezeka kutoka mita 45 kwenda mita 6o na hii itakuwa ni kwa nchi nzima. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopitiwa kwenye mashamba yao pale Uvinza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu moja kwa moja kwa sababu Mheshimiwa Mbunge nilishamtaja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, fidia hiyo italipwa. Tayari tumeshapeleka taarifa kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha baada ya kufanya tathmini na tutakapopewa fedha hizo zitalipwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Newala hadi Masasi unaenda sambamba na ujenzi wa miradi ya kijamii. Kwa kuwa barabara hiyo ujenzi umeshaanza, je miradi hiyo ya kijamiii itaanza kujengwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi hiyo barabara ya kilometa 160 tayari tuko tunafanya tathmini ikiwa ni pamoja na kusanifu hiyo miradi ili ianze kujengwa sambamba na hiyo Barabara.  Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Muharami Shaban Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Ujenzi wa Chuo cha VETA- Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Halmashauri ya Bagamoyo kwa kuwa imekamilisha vigezo vyote muhimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inaendelea kutekeleza azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 64 ikiwemo chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Bagamoyo kinachojengwa katika Halamshauri ya Mji wa Chalinze. Ujenzi huo unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutekeleza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi,  katika Mwaka wa Fedha 2024/2025,

Serikali imeanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa Shule za Sekondari za ufundi 100 ambazo zitajengwa katika Halmashauri ambazo hazina Vyuo vya *VETA* pamoja na maeneo mengine yenye uhitaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi. Halmashauri ya Bagamoyo ni miongoni mwa Halmashauri zitakazojengewa Sekondari ya Ufundi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tunatambua kwamba Serikali ina mpango wa kujenga Shule za Ufundi katika Halmashauri zote ambazo hazijapata vyuo vya *VETA*. Je, ujenzi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Chuo cha *VETA* kinachojengwa katika Wilaya ya Bagamoyo Halmashauri ya Chalinze mpaka sasa kinasuasua ujenzi wake na hatujui hatma yake ni lini kitamalizika. Je, Serikali ina kauli gani kumaliza chuo hiki ili wananchi wa Bagamoyo na wananchi wa Chalinze, wanafunzi wetu na vijana wetu wapate kusoma katika vyuo hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake muhimu kwa Wanabagamoyo na Chalinze kwa ujumla na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 87 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule hizi za amali kwa awamu. Kwa hiyo, katika kipindi hiki kwanza katika mwaka huu wa fedha tutajenga shule hizo 100, lakini ujenzi huu utaanza kwa awamu. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge tayari

hivi sasa tumeshaanza kupeleka fedha ambazo ni kati ya shilingi milioni mia tano na ishirini na nane *plus* katika kila Halmashauri ambayo inataka kujengewa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu ndani ya *quarter* hii ya kwanza ya mwaka huu ujenzi huu wa shule hizi za sekondari za amali katika maeneo haya niliyoyataja uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili, katika Chuo chetu cha *VETA* pale Chalinze na bahati nzuri na nilifanya ziara pale nimetembelea eneo lile kulikuwa na changamoto za *design* pamoja na wajenzi wetu wale tukajaribu kutatua. Nimwondoe hofu tayari tumeshazungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tulipokea mwanzoni shilingi bilioni 49 bado shilingi bilioni 51 hatujazipokea kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na Wizara ya Fedha ndani ya *quarter* hii ya kwanza tutahakikisha kwamba fedha zile shilingi bilioni 51 tumezipata ili kuendelea na ujenzi katika maeneo yote ya Wilaya hizi 64 ili kuhakikisha kwamba ujenzi huu unakamilika ndani ya mwaka huu ili mwakani vijana wetu waanze kupata mafunzo katika maeneo haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya yangu ya Nanyumbu kwenye Kijiji cha Maneme umesimama kwa kipindi kirefu. Je, ni lini ujenzi huo utaendelea? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza katika maelezo yangu ya jibu la mwanzo kwamba tunatarajia ndani ya *quarter* hii yaani mwezi huu Agosti na mpaka kufika mwezi Septemba tuweze kupata fedha hizi shilingi bilioni 51 ili ujenzi ule uweze kuendelea katika maeneo yote, katika Wilaya 64 na kile kimoja cha Mkoa wa Songwe, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Serikali imekamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Geita, lakini kimejengwa *very substandard*. Sasa nataka kujua ni lini Wizara itapeleka Mkaguzi pale kuangalia kazi ilivyofanyika chini ya kiwango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kanyasu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeshafika Geita, Vyuo hivi vinne vya Mikoa ambavyo mwanzoni vilikuwa vinajengwa kwa ufadhili wa Benki ya *FDB* na baadaye mkopo ule ulisitishwa, Serikali ilikwenda kukamilisha ujenzi ule kupitia fedha za UVIKO-19 ambapo tulifanya ujenzi ule kwa njia ya *force account,* ujenzi umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Mbunge anazungumza kwamba umekwenda *substandard,* nitamwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie baada ya Bunge hili tuweze kufanya ziara sote kwa pamoja, mimi na yeye twende tukabaini hayo maeneo ambayo anadhani kwa namna moja au nyingine labda yamejengwa kwa *substandard* ili tuweze kufanya maboresho na marekebisho, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kile chuo chetu cha Musoma Mjini cha *VETA* ndicho chuo kinachohudumia vyuo vinavyoanzishwa vya Mkoani Mara kama Butiama pamoja na kule Rorya. Je, ni lini sasa chuo hicho kitapewa hadhi Mkoa pamoja na *facilities* zote kwa maana ya miundombinu inayolingana na hadhi ya Mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu dogo la Mheshimiwa Manyinyi. Nashukuru kwa maswali yake ya msingi, Mheshimiwa Manyinyi nitaomba na yeye vilevile aridhie baada ya Bunge hili labda tuweze kufanya ziara, twende pale tukafanye tathmini ya kuangalia mahitaji na mapungufu yaliyopo ili Serikali iweze kuyafanyia kazi tuweze kuongeza hiyo miundombinu ambayo inapungua ili kukipa hadhi chuo hiki kuwa Chuo cha Mkoa. Nashukuru sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Ukarabati Skimu za Umwagiliaji Kata ya Bahi**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji zilizopo Kata ya Bahi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu zilizopo katika Bonde la Bahi. Bonde hilo lina jumla ya hekta 5,000 na linajumuisha Skimu za Nguvumali, Bahi Sokoni, Mtazamo, Matajila na Welela. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa skimu hizo umekamilika na skimu hizo zipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za Mkakatika na Makulu katika Bonde la Bahi ili kuongeza eneo la umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ili hatua ya manunuzi kuanza inatakiwa kwamba kazi iwe imeshatangazwa kwenye hatua za manunuzi, lakini bado haijatangazwa. Swali langu linabaki pale pale, ni lini Serikali inaanza ukarabati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; Umoja wa Wakulima pale Bahi walikopa Benki - *NMB* na bahati mbaya yakatokea mafuriko na deni lile limekuwa likiongezeka na Wizara ilionesha *interest* ya kumaliza mkwamo wa deni lile. Je, ni lini deni hili linaenda kumalizwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kama tulivyojibu katika jibu la msingi ni kwamba tayari *feasibility study* imeshafanyika na sasa tuko katika hatua ya manunuzi ya kumpata mkandarasi na nimthibitishie tu katika mwaka huu wa fedha jambo hili litakuwa limekamilika na tutamkabidhi mkandarasi *site* baada ya kumaliza hizi hatua za manunuzi. Kwa hiyo, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko kazini na hili jambo litaenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni ni kwamba tunashosubiria sisi ni fedha tu na baada ya hapo tutalipa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunalifahamu jambo hili na ndiyo maana Serikali tumekuwa tukilifuatilia kila wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati akijibu maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna swali la Mheshimiwa Ighondo Ramadhani nilisema utapata nafasi ya kulijibu, lakini baada ya

kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge kadhaa wameniletea ujumbe hapa kwamba watahitaji kuuliza maswali ya nyongeza kwa sababu wana hoja kama hizo kwenye maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hili swali Serikali ikatafute majibu kama swali la msingi ili lije liulizwe ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kuja kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ighondo swali lako litajibiwa kama swali la msingi kwa hiyo litaletewa majibu na Serikali, hivyo Wabunge wengine watapata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.*( Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Abdull Yussuf Maalim, Mbunge wa Amani, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Tathmini ya Changamoto za *ZFF* na *TFF***

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM** aliuliza:-

Je, tathmini ipoje juu ya utatuzi wa changamoto zitokanazo na Mashirikiano yaliyopo kati ya *ZFF* na *TFF?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa sasa mashirikiano kati ya *ZFF* na TFF hayana changamoto zozote kwani kazi zinaendelea kwa pamoja kwa manufaa ya pande zote za Muungano kwa maendeleo ya mpira wetu. Mathalani mashirikisho haya yanashirikiana katika kuendesha soka la vijana, mashindano yote ya kitaifa ya vijana *under 15* na *under 17*. Aidha, katika

mashindano ya *CAF* na *FIFA* wawakilishi wetu *Taifa Stars, Twiga Stars*, na *Serengeti Boys* hushirikisha wachezaji kutoka katika pande zote mbili za Muungano kulingana na vigezo vya Mwalimu katika uteuzi wa wachezaji husika.

*TFF* na *ZFF* pia wamekuwa wakishirikiana vema katika kuendesha mafunzo ya waamuzi pamoja na walimu wa soka kwa kozi zote za *CAF* na *FIFA* zinazoendeshwa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, fauka ya hayo, mashirikisho haya yameendelea katika uandaaji wa mashindano ya kimataifa mathalani mashindano ya *African Schools Football Championship* ambayo yalifanyika mwezi Mei mwaka 2024 katika uwanja wa *Amaan Complex,* Visiwani Zanzibar na timu ya wavulana ya Taifa kuchukua ubingwa.

Mheshimiwa Spika, *TFF* kwa kushirikiana na *ZFF* zimekuwa zikipeleka mashindano mbalimbali Visiwani Zanzibar. Pia fainali za kombe la Shirikisho *(FA Cup)* kati ya Yanga dhidi ya *Azam FC* na nusu fainali ya Kombe la Ngao ya Jamii mwaka 2024, mchezo kati ya *Coastal Union* dhidi ya *Azam FC* yote ilifanyika katika uwanja wa Amaan. Hali kadhalika, misafara mingi ya Timu ya Taifa ya Tanzania - *Taifa Stars* imekuwa ikiongozwa na Rais wa *ZFF* kama Mkuu wa msafara, kuonesha ushirikiano mkubwa uliopo kwa sasa baina ya *TFF* na *ZFF*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Naomba kuuliza masuala madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa muktadha wa mabadiliko ya Katiba ya *TFF* hususan kipengele Na.2. Je, ni vipi *ZFF* itanufaika na mabadiliko ya Katiba hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kiasi gani itasaidia kuinua viwango vya ubora wa waamuzi kutoka Zanzibar kuelekea kimataifa ukizingatia Zanzibar tuna upungufu wa waamuzi wa kimataifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na mabadiliko ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasema kwenye Katiba ya *TFF,* Zanzibar bado itakuwa inaendelea kunufaika na programu zote za maendeleo ya mpira wa miguu zinazofanywa na *TFF,* zikiwemo programu zinazoendeshwa kupitia *CAF* na *FIFA* kama ambavyo imekuwa ikitokea huko nyuma. Hakuna chochote ambacho kinakwenda kubadilika kwenye programu za maendeleo ya michezo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Zanzibar itaendelea kunufaika.

Mheshimiwa Spika, hali kama hiyo pia inakwenda mpaka kwenye suala la waamuzi, kwa vile *course* zote za waamuzi ikiwemo mitihani ya kupata beji ya *FIFA* ambazo zinaendeshwa na *TFF* zinahusisha pia upande wa waamuzi kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, fursa ya kufanya mitihani kwa ajili ya kupata beji ya *FIFA* bado itaendelea kuwepo kama ambavyo imekuwa ikitokea kama nyakati zote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninalo tangazo la wageni hapa, lakini kabla ya tangazo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna ujumbe nimeupokea hapa.

Kuna Mbunge anauliza, maagizo ambayo huwa yanatolewa kwa Wakuu wa Taasisi, Viongozi mbalimbali walioko nje ya Bunge hili yanayotolewa na Waheshimiwa Mawaziri wanapojibu hapa maswali, utaratibu wa utekelezaji wa hayo maagizo ukoje?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa sisi upande wa Bunge huwa tunao utaratibu, nimekutaja Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini tunao utaratibu, yale mambo yote yanayotokea huku Bungeni huwa yanaandikwa na zile ahadi zilizotolewa na mambo kama hayo huwa tunazipeleka Serikalini, lakini na wao pia Serikali kipindi hiki cha maswali kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali wanao Maafisa wa Serikali ambao ni kazi yao kufuatilia haya majibu ili wawafikishie wale ambao wamepewa maelekezo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ikitokea kwamba Mheshimiwa Mbunge uliuliza swali, Serikali ikatoa maelekezo kupitia Naibu Waziri ama Mawaziri ama Waziri Mkuu, huko jambo likawa halijafanyika, sasa ni kazi yako kwa sababu wewe ndiyo mwakilishi wa wananchi kufuatilia, aidha kwa hapa Bungeni ama kufuatilia kwa Waziri husika kwamba jambo hili ulilitolea maelekezo na halijafanyiwa kazi, lakini utaratibu upo wa namna hiyo, kwa maana ya kwamba maelekezo yanayotolewa hapa Bungeni huwa kuna maafisa ambao wanafuatilia ili wayapeleke kwa wale wanaohusika, pia upande wa Bunge huwa yanaandikwa hayo yote kila mwisho wa Bunge na kuipelekea Serikali na Serikali huwa inaleta taarifa kila baada ya muda kuleta utekelezaji wa yale yote ambayo yaliagizwa hapa Bungeni, kwa hiyo huo ndiyo utaratibu.

Jambo la pili Mheshimiwa Waziri Mkuu nimeletewa hapa taarifa ambazo kama mambo mengine huko nyuma nilivyowahi kutoa maamuzi kwamba, jambo ambalo sina taarifa nazo za kutosha, inaniwia ngumu kulitoa kwa Bunge ili Bunge liweze kujadili ama kulitolea maelekezo kwa Serikali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeletewaa taarifa hapa kwamba, wale watu ambao aliwasemea Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba kwamba wamekamatwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya sasa wamefunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hili jambo jana kwa sababu tulilizungumza hapa na tukakuomba ukalifanyie kazi, lakini pia leo wakati wa maswali Mheshimiwa Stella Fiyao alipoliuliza ukasema

kwamba, unaendelea kulifanyia kazi kwa yale maelekezo yaliyokuwa yametoka jana. Basi hili jambo lifuatiliwe kwa haraka kwa sababu hatuna uwezo wa kujua ni mazingira gani uhujumu uchumi ulikuwepo kabla akatumwa *DC* kwenda kuwakamata ama haukuwepo umekuja baada ya *DC* kutoa maelekezo na Mbunge kusema humu ndani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa nimeona niliseme kwa sura hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana yake sasa linakwenda kuchukua sura nyingine mpya. Sasa likichukua hiyo sura mpya tena, lisije likatupeleka sisi kuanza kulijadili hapa ndani wakati hatuna taarifa za kutosha. Vilevile, kama kuna na watu watakuwa wamepata athari ambazo Mheshimiwa Mbunge wa eneo hilo amekwishazisema hapa ndani mara kadhaa, tutalazimika kulijadili hilo jambo kwa sura ambayo pengine haitapendeza kwa sababu kama tayari imeshatajwa hapa uhujumu uchumi, maana yake tayari kesi iko Mahakamani na Mbunge akisimama hapa itaonekana tunajadili jambo ambalo liko Mahakamani.

Kwa hiyo, lifuatiliwe katika kipindi hiki cha mwanzo ili Bunge tusije tukajikuta tunajadili jambo. Kama limefika kweli Mahakamani, limefika kwa sura gani? Hiyo ya kisiasa aliyokuwa anaisema Mbunge ama lilikuwepo kabla? Kwa sababu tusije tukajikuta tunaanza kuvutana hii Mihimili kwa sura ambayo haitapendeza.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la wageni walioko Bungeni na tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula kutoka Taasisi ya *Msichana Initiative* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Rebecca Gyumi ambaye ni Mkurugenzi wa *Msichana Initiative* na Mwenyekiti Mwenza wa Jukwaa la Wanawake na Uongozi Afrika kwa upande wa Tanzania. Ameongozana na Anande Nko ambaye ni Mkurugenzi *Girls Livelihood and Mentorship Initiative (GLAMI);* Ndugu Lineth Masala - Meneja Miradi *Flaviana Matata Foundation* na, ameongozana na Ndugu Steven Kiboko ambaye ni Afisa Miradi *Msichana Initiative*, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wenu Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbongwe. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni ndugu zake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi ambao ni Katibu wake Ndugu Emmanuel Mapunda na dereva wake Ndugu Ali. *(Makofi)*

Wageni 43 wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambao ni Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Jimbo la Same Mashariki kutoka Wilaya ya Same pamoja na Ndugu Paul William ambaye ni Mwandishi wa Habari, Gazeti la Uhuru, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Mawaziri mnazungumza na mimi nimesimama.

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni Wenyeviti Kata wa Chama Cha Mapinduzi…

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na huyo uliyekaa naye hapo jirani nimesimama bado, ahsante sana.

Wageni 25 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni Wenyeviti kata wa Chama Cha Mapinduzi kutoka kata zote za Wilaya ya Kilolo, Iringa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Yahaya Ally Mhata, ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Tairo. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikano wa Afrika Mashariki, hawa ni wanafunzi 75 na walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *The Glory,* wakiongozwa na Meneja wa Shule Ndugu Mathew Levi Alexna kutoka Mafinga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 55 na walimu wanne wa Shule ya Sekondari ya Adventista Wasabato kutoka Mbeya, karibuni sana wageni wetu na karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 76 kwa jambo ambalo limejitokeza mapema leo Bungeni. Awali wakati wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mafuwe aliuliza swali kwa Waziri Mkuu akizungumzia juu ya pombe kali ambazo vijana kwa sasa wanatumia kwa wingi na kupelekea kutofanya kazi na kupata athari za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri Mkuu lakini kiuhalisia pombe hizi zina madhara makubwa zaidi nje ya uchumi. Tumeshuhudia vijana wengi na hata wengine wenye rika zaidi ya miaka 45 na 50, baada ya kutumia hizi pombe kali ambazo zinauzwa kiholela hata kwenye maduka ya vyakula, nyingine zinauzwa kwa maduka ambayo hayana leseni, zinauzwa mpaka shilingi 2,000 mpaka shilingi 3,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanatumia na wanapata mpaka madhara ya kiafya. Mathalani, wanapata madhara ya figo, wanaharibika ini, lakini hata wanafunzi wetu wa wengine wa sekondari wanakwenda wananunua hizi pombe wanaathirika macho, wanapata matatizo ya kuona. Ukipata madhara ya kiafya, maana yake unapelekea mzigo mkubwa kwa Serikali kufanya *dialysis* ya figo lakini hata familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi pombe pia zina madhara hata hata ya kijamii kwa maana ya kwamba, wakishatumia hizi pombe wanadhoofika na hata vijana wetu wanashindwa kuanzisha familia. Kwa hiyo, hii nayo inapelekea mapungufu kwenye nguvu kazi ya Taifa kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ukiniruhusu kufanya rejea naweza nikataja hata baadhi ya hizi pombe ili sasa mwongozo wangu ninapokwenda kuulekeza….

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, baadhi ya hizi pombe ambazo zinauzwa shilingi 2,000 na kuna kipindi tulichangia hapa wakati wa bajeti; kuna pombe inaitwa *Kuka* ziko kama kumi hivi…

**SPIKA:** Sasa huko kwenye kuzitaja kwa sababu linaweza kuwa ni jambo la kibiashara, maliza hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Nimeomba mwongozo kwako kuweza kujua kwa nini Serikali isifanye tafiti ya madhara makubwa ya pombe ambayo wanapata Watanzania baada ya kutumia hizi pombe ambazo kwa kweli ziko kwa wingi mtaani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa nini Serikali inaruhusu watu wauze kiholela wakati kuna leseni ambayo inatakiwa zitolewe *proper* kwenye haya maduka? Pia, zinauzwa muda wote ule. Ukiona kijana ameshikilia *Energy drink,* hajashikilia *Energy drink*; pale ameweka shimuhaa, ameweka hizi pombe ambazo umesema nisizitaje.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kwa nini Serikali isifanye tafiti za kina kuweza kujua madhara makubwa ambayo wanapata Watanzania baada ya kutumia hizi pombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa nakumbuka hapa michango ya Mheshimiwa Mbunge wa Momba. Mheshimiwa *Chief Whip* geuza kiti huku mbele Spika ameshasimama.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Esther Matiko hapa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 76 akiomba Mwongozo wa Spika, juu ya swali ambalo lilijitokeza leo wakati wa kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu lililoulizwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kuhusu pombe kali ambazo ziko chini ya kiwango ambazo zina madhara kwa binadamu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa majibu hapa. Kwa namna swali lilivyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishalijibu.

Hata hivyo, Mheshimiwa Esther Matiko ameomba Mwongozo kupitia Kanuni ya 76 kwa maelezo hayo aliyoyatoa na hapo mwishoni akauliza swali kwamba, kwa nini Serikali isifanye hicho ambacho amekisema.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 76 pamoja na kwamba inataka jambo liwe limetokea hapa ndani, lakini ili utumie Kanuni hii ni kwamba unataka kusema kama hilo jambo linaruhusiwa au haliruhusiwi kusemwa ama kutendwa hapa ndani. Kwa maana kwamba, swali lililoulizwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu limeshaisha na hakuna mwongozo juu ya hilo, swali liko vizuri.

Hata hivyo, madhara aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge hapa kwa kweli ni madhara makubwa kwa Taifa letu ukiacha hilo eneo la kiuchumi ameeleza na madhara mengine. Pia, pengine yatakuwepo madhara makubwa zaidi. Kwa sababu kama ni makubwa kwa namna hiyo maana yake mwingine akizidisha hicho kiwango, anaweza hata kupoteza uhai wake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amesema anayo orodha ya hizo aina ya hizo pombe au baadhi ya aina ya hizo pombe, ataikabidhi Serikali ili waweze kufuatilia zinaingia kutoka wapi na ni za nchi gani? Je, zinatengenezwa hapa nchini?

Pia na kujaribu kuona namna ambavyo yale maeneo yaliyoathirika Serikali inaweza kuchukua hatua gani.

Sasa kwa hatua hii siwezi kutoa mwongozo wowote, lakini hoja ya msingi imesikika. Upande wa Serikali lichukueni jambo hili na mlifanyie kazi kwa sababu tutakuwa tunawapoteza vijana na pengine siyo vijana tu; wengine wanaweza kuwa wanatumia pombe hizi na wasijue madhara na huenda ndio maana namba zinazidi kuongezeka za magonjwa haya tunayosema yamezidi sana.

Naona Mbunge wa Iringa Mjini pale ananitazama kuashiria kwamba, aliyoyasema Mheshimiwa Esther Matiko yuko sahihi kwa sababu yeye ni mtetezi wa familia. Hata hivyo, jambo limesikika na limeeleweka Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, halitatolewa mwongozo lakini Serikali ilichukue jambo hili na kulifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendment Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye anashughulikia masuala ya Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na pia Mifuko hii kwa maana ya marekebisho ya Sheria hizi yako chini yake, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendments Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya pekee naomba nianze kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia mimi kupitia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuniteua kuwa Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mungu, nataka kuendelea kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu na kutuamini mimi na wenzangu kuendelea kuhudumu katika Wizara hii. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu wote kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu. Kwa hakika uongozi wao na usaidizi wao kwa uongozi wetu ni ushuhuda wa dhati kuwa timu imara inaleta matokeo imara. Hongera sana kwa viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge na mwalimu wangu, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa

Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Afya; Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo- Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Cosato David Chumi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyadhifa mbalimbali wanazozitumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mkurugenzi wa *WHO,* Kanda ya Afrika. Uchaguzi huu ni kielelezo cha kukubalika kwa Nchi yetu ya Tanzania katika dunia. Hii ni tafsiri ya juhudi zinazofanywa na Rais wetu katika kuunganisha Tanzania na dunia kwa upande mwingine. Hongera Rais wetu, hongera Watanzania, hongera *Comrade* Ndugulile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala mbalimbali ndani ya Bunge lako kwa umahiri mkubwa. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia shukrani, kwa upekee kabisa nataka kuishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wetu Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaotupatia katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu wakiongozwa na Naibu Waziri wangu *Comrade* Patrobas Katambi, Mbunge mahiri, bingwa, hodari na mwenye weledi, kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya ya kuendelea kunisaidia pamoja na wenzangu wote. Pamoja naye, pia nimpongeze Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu wetu, Naibu Katibu Mkuu Zuhura Yunus Abdallah pamoja na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza kwa weledi majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ahadi yangu kwako, Watanzania na hasa Mheshimiwa Rais kuwa, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upekee nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Hamza Johari na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana Samweli Maneno, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pili, kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza vizuri majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, hapa nataka kumshukuru sana Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bwana Onorius Njole kwa kuandaa Muswada huu na kwa usimamizi wake wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize salamu zangu za shukrani kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwa ushirikiano na ushauri wanaotupatia wakati wa kupitia Miswada hii ndani ya Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa sana na nzuri ya kuchambua Miswada hii kwa umakini na maoni yao yaliwasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hii yamezingatiwa. Naomba kuishukuru Kamati kwa kuisadia Serikali kuboresha Muswada huu pia. Serikali imezingatia

ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024, kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50, (*The National Social Security Fund Act, Cap. 50);*

(ii) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371, *(The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371*); na

(iii) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263, *(The Workers' Compensation Act, Cap. 263)*.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne ambapo katika Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997 kwa lengo la kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na kuweka muundo na usimamizi wa Mfuko na masuala mengine yanayohusiana nayo. Tangu ilipotungwa sheria hii imerekebishwa mara kadhaa. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga kutatua changamoto katika usimamizi wa Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho ya jumla kwa kufuta msamiati "*insured person*" mahali popote katika sheria inapoonekana na badala yake kutumia msamiati "*member.*" Lengo la marekebisho haya ni kutumia msamiati ambao unaakisi tasnia ya hifadhi za jamii. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha

baadhi ya tafsiri ya maneno ili kuweka tafsiri sahihi ya misamiati hiyo. Vilevile, kifungu kimerekebishwa kwa kuongeza misamiati mipya inayotumika katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kufanya masharti yaliyoainishwa katika sheria yaeleweke kirahisi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta rejea ya Jedwali la Kwanza kwa kuwa masharti yote yamejumuishwa katika kifungu cha 12 cha sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya sheria kuhusu michango ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti ya kumtaka mwajiri kutunza rejesta, kumbukumbu na taarifa nyinginezo za mwajiriwa. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha usahihi wa kumbukumbu za mwanachama na kuongeza ufanisi katika ulipaji wa mafao. Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa kwa mwajiri kuweka cheti cha usajili mahali pa kazi katika sehemu inayoonekana kwa urahisi. Marekebisho haya yanalenga kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu kipya cha 11A kinapendekezwa kuongezwa ili kuwezesha watu waliojiajiri wenyewe katika sekta binafsi kujiunga na kufaidika na mafao ya hifadhi ya jamii katika mpango wa uchangiaji kwa mujibu wa sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii kwa watu waliojiajiri.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12(1) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha asilimia ya kiwango cha uchangiaji kinachopaswa kuwasilishwa na mwajiri kwenye Mfuko. Kifungu cha 12(3) kinapendekezwa kufutwa ili kuruhusu mwajiri kuchangia kwa kiasi kikubwa au kiasi chote. Kifungu cha 12(5) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha namna ya uchangiaji kwa wanachama waliojiajiri.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12A kinapendekezwa kuongezwa ili kuruhusu mfanyakazi aliyeajiriwa na mwajiri zaidi ya mmoja kuchangiwa na waajiri wote kwa ridhaa yake. Lengo la

marekebisho haya ni kumpa mwanachama uhuru wa kuchangiwa na zaidi ya mwajiri mmoja. Aidha, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutumia neno *"remitted"* badala ya neno *"paid."*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14(3) kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza adhabu ya tozo kutoka asilimia tano hadi 12.5% inayotozwa na Mfuko kwa mwajiri kwa kuchelewa kuwasilisha michango ya mfanyakazi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha kiasi stahiki kwa faini na kupunguza gharama za uendeshaji kwa mwaajiri na kuweka tozo rafiki na zinazolipika.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha bodi kuondoa michango ya ziada iliyoainishwa chini ya sheria baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana na hifadhi ya jamii. Lengo la marekebisho haya ni kutoa nafuu kwa taasisi zilizoonesha nia ya kutekeleza masharti ya sheria lakini zinashindwa kulipa adhabu za faini kutokana na changamoto za kifedha.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka wajibu wa Mkurugenzi Mkuu kuhakikisha kuwa hesabu ya kiwango chote imewekwa kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii hata kama kiwango hicho kilikatwa na mwajiri na hakikuwasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kulinda maslahi ya wanufaika wa mafao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kubainisha kwa ufasaha masharti yanayohusiana na malipo yaliyofanyika kimakosa. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usimamizi wa michango inayopokelewa kimakosa kwenye Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa kwenye kifungu cha 74A. Kifungu cha 20(3) kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yanakinzana na taratibu za mfumo wa pensheni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuruhusu michango iliyowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi kufika miaka sabini kuzingatiwa katika ukokotoaji wa malipo ya mafao ya pensheni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa mafao ya pensheni kwa mwanachama ambaye amefikisha umri wa kustaafu lakini hajakidhi vigezo vya pensheni na amekuwa akichangia umri wa miaka 61 mpaka 70.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha mafao ya ulemavu kwa mwanachama ambaye wana ulemavu wa kudumu kutokana na majeraha au ugonjwa usiotokana na kazi aliyoajiriwa. Kifungu cha 28A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Mkurugenzi Mkuu kuteua jopo la madaktari ili kuthibitisha iwapo mwanachama amepata ulemavu wa kudumu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa mafao yanatolewa kwa mnufaika anayestahili.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno *thirty three* na kuweka neno *thirty six*. Lengo la marekebisho haya ni kuweka idadi ya sahihi ya miezi inayokusudiwa ambayo ni miezi 36 kuongeza kiwango kinacholipwa kwa wategemezi pale ambapo mwanachama atakuwa amefariki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 43 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo kwa vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya ambavyo Bodi inaweza kuingia navyo makubaliano ili kutoa huduma za afya kwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 52 na 76 vinapendekezwa kurekebishwa ili kumruhusu mwanachama ambaye hajafikia umri wa kustaafu kutumia sehemu ya mafao yake kama dhamana kwa mkopo wa nyumba. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi kwa kuwa vifungu hivyo vinazuia matumizi ya mafao kama dhamana ya mkopo isipokuwa kwa mkopo wa nyumba kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 20.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 61 na 71 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa hitaji la Bodi kuwa na akaunti ya akiba. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa matumizi ya misamiati ambayo haitumiki kwenye tasnia ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 72 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza makosa mapya kwa mwajiri anayekataa kujiandikisha na mtu yeyote anayemzuia mkaguzi wakati wa kutekeleza majukumu yake. Aidha, kifungu kidogo cha tatu cha kifungu hicho pia kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka au Afisa wa Mfuko aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua kesi yoyote ya jinai chini ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utekelezaji na usimamizi bora wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 74 kinapendekezwa kurekebishwa na kuiondolea Bodi jukumu la kuteua afisa kwa ajili ya kufungua shauri la kudai michango. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha shughuli za kila siku za mfuko zinatekelezwa na Maafisa wa Mfuko chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 74A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuwekwa masharti yanayomtaka mdaiwa kuweka dhamana ya gharama anapoomba ruhusa ya kujitetea katika kesi za kurejesha michango. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha upatikanaji wa michango ya wanachama shauri dhidi ya mwajiri linapomalizika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufafanua masharti ya mgawanyo wa mapato yanayotokana na kuuzwa kwa mali za mwajiri.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 79 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiondolea Bodi majukumu ya kila siku ya uendeshaji wa Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 87 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha mamlaka ya mkaguzi kwa madhumuni

ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria. Aidha, Kifungu cha 87A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuitisha taarifa au nyaraka ambazo zipo kwenye himaya ya mtu au taasisi husika. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Mfuko unakua na uwezo wa kupata nyaraka yoyote muhimu au taarifa kadri itakavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 90 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuyajumuisha mafao yanayolipwa chini ya sheria hii katika orodha ya masuala yasiyotakiwa kutozwa kodi kama ilivyoorodheshwa katika kifungu hiki. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utozaji wa kodi mara mbili kwenye mafao yanayolipwa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza linapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa katika kifungu cha 12.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371. Sheria hii ilitungwa mwaka 2018 kwa lengo la kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, kuweka uchangiaji na malipo ya mafao ya hifadhi ya jamii kuhusiana na wafanyakazi katika utumishi wa umma na kuweka masuala mengine yanayohusiana na hayo. Tangu ilipotungwa sheria hii imerekebishwa mara moja. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha tatu ili kuboresha tafsiri ya baadhi ya misamiati inayotumika katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati inayotumika kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kichwa cha habari cha Sehemu ya Pili ya sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno *Pension*. Lengo la marekebisho haya ni kufanya kichwa cha habari kiendane na maudhui ya sehemu hiyo. Aidha, kifungu cha 5(2)

kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwamba waajiriwa wa kampuni ambayo Serikali inamiliki angalau 30% ya hisa ni lazima wasajiliwe kwenye Mfuko huu. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utendaji kazi wa Mfuko na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti yanayohusiana na usajili wa wanachama wa Mfuko. Aidha, mapendekezo ya marekebisho yanalenga kumwondolea mwajiri majukumu ya kuwasilisha ripoti ya fedha kwenye Mfuko na badala yake kuhakikisha mwajiri anatunza kumbukumbu za waajiriwa wake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayobainisha afisa mwenye wajibu wa kuwasilisha michango kwenye Mfuko, kuhusiana na waajiriwa wa taasisi ambao mishahara yao hailipwi na Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiwezesha bodi kuondoa michango ya ziada inayoainishwa chini ya sheria baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana na hifadhi ya jamii. Lengo likiwa ni kufanya marekebisho ili kutoa unafuu kwa taasisi zilizoonesha nia ya kutekeleza masharti ya sheria, lakini zinashindwa kulipa adhabu za faini kutokana na changamoto za kifedha.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti yanayohusiana na kumbukumbu za michango ya mwajiriwa pindi zitakapohitajika. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha mwanachama kupata historia ya uchangiaji wake kwenye Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 kinapendekezwa kufutwa. Lengo la marekebisho haya ni kuondokana na dhana iliyojengwa katika kifungu hicho inayoruhusu mwanachama kutoa kiasi cha

mchango wake katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kuondolewa uanachama inakinzana na kanuni za hifadhi ya jamii kutokana na dhana ya kifungu hicho kutotumika kwenye Mfuko wa Akiba na siyo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwamba mnufaika wa mafao ambaye kwa kipindi husika anatumikia kifungo anaweza kuridhia kwa maandishi kwamba mafao yake au sehemu yote ya mafao yake ilipwe kwa mnufaika aliyetajwa. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ushiriki wa mtu anayetumikia kifungo katika utoaji wa mafao yake kwa mnufaika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 47 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti yanayohusiana na kutokuhamishika kwa mafao ya mwanachama. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi, kulinda ustawi wa wanachama na mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa dhana ya mafao yasiyodaiwa haitumiki katika kanuni ya msingi za hifadhi ya jamii. Aidha, lengo la marekebisho haya ni kumwezesha mnufaika kudai mafao yake pasipo na ukomo wa muda.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 51 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuwianisha na masharti yanayohusu upitishwaji na uwasilishwaji wa makadirio ya bajeti. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha ufafanuzi na mfanano kwa masharti yanayoendana. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa dhana ya akaunti ya akiba haitumiki kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 58 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuboresha masharti yanayohusiana na utekelezaji wa mapendekezo ya uthaminishaji wa ustahimilivu wa Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 59 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuuwezesha Mfuko, kwa ridhaa ya Bodi kufungua na kuendesha akaunti zaidi ya moja ya benki.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi, Sura ya 263. Sheria hii ilitungwa 2008 kwa lengo la kuweka masharti ya fidia kwa wafanyakazi kutokana na kifo au ulemavu wa kudumu unaosababishwa na majeraha au magonjwa yanayotokana na utekelezaji wa majukumu ya mfanyakazi mahali pa kazi. Tangu ilipotungwa sheria hii imerekebishwa mara tatu. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, muswada huu unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 14 ili kuiwezesha Bodi kubadili na kuondoa sharti lolote linalohusiana na malipo ya mafao chini ya sheria pale ambapo kuna sababu za msingi za kufanya hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Bodi kuruhusu malipo ya mafao endapo mnufaika atashindwa kukidhi masharti na sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha matumizi ya ukomo wa muda kuanza kuhesabiwa kuanzia tarehe ya kutokea kwa ugonjwa husika. Vilevile, kifungu tajwa kinapendekezwa kurekebishwa ili kumruhusu Mkurugenzi Mkuu kuzingatia madai ya fidia pale ambapo taarifa iliyowasilishwa na mwajiriwa ndani ya muda japokuwa mwajiri aliwasilisha madai hayo nje ya muda.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42(3) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu vyama vya wafanyakazi au mtu yeyote kuwawakilisha waajiriwa katika madai ya fidia katika Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia mgongano wa maslahi kwa kuwa Maafisa Kazi na Wauguzi au Maafisa wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi ni sehemu ya watu wanaotekeleza Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48(6) kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha mwajiriwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu kuendelea kupokea pensheni hata baada ya kurejea kazini au kupokea mafao ya uzeeni. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kati ya wanufaika ambao wanapokea mafao kwa mkupuo na wanaopokea pensheni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 58(2) kinapendekezwa kufutwa ili kutojumuisha motisha katika mishahara inayotumika kwenye ukokotoaji wa fidia ili kuweka usawa kwa wanufaika katika malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 73 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa masharti yanayowalazimisha waajiri kuwasilisha taarifa ya mapato ya mwaka katika Mfuko kila ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka, kwa kuwa taarifa zinazowasilishwa na waajiri wanawasilisha michango ya kila mwezi husika. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Mkurugenzi Mkuu kuitisha taarifa hizo wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 75(2) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "*interest*" na badala yake kuweka maneno "*additional assessment.*" Lengo la marekebisho haya ni kutumia maneno sahihi yanayoakisi utekelezwaji wa Sheria. Aidha, kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha mfuko kurejesha michango ya waajiri iliyolipwa kwa ziada au kimakosa. Kifungu cha 82 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondokana na matakwa ya lazima ya kuwa na akaunti ya akiba na kuondoa jukumu la kufungua akaunti kwa Waziri na kuweka jukumu hilo kwa Bodi ya Wadhamini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 85 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu Mfuko kuwasilisha kwa Bodi ndani ya miezi sita taarifa ya mwaka kuhusu shughuli za Mfuko katika mwaka wa fedha na taarifa ya fedha iliyokaguliwa ndani ya mwezi mmoja baada ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kumaliza ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, miswada hii yote inalenga kutatua changamoto ambazo kwa upande mmoja, wanachama wanapata wanapofika katika kipindi cha kufaidi matunda ya utumishi wao. Miswada hii imefafanua kipengele kwa kipengele na kueleza nia ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutatua changamoto ikiwemo ile ya mkwamo wanaoupata watumishi punde wanapostaafu na kukutana na kizingiti cha waajiri wasiowasilisha michango kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, miswada hii inalenga pia kuongeza makusanyo kwa mifuko yetu, kuondoa uonevu wakati wa kuwapatia haki wafanyakazi walioumia kazini na anayepaswa kutoa taarifa anapochelewa kutoa ndani ya muda, malipo yasiyo ya lazima na kulinda watumishi katika stahiki zao, pamoja na hilo pia ni kuwasaidia waajiri kupata ulinzi wa taarifa na kuwajengea mazingira wachangiaji wapate nafuu katika malipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendments) Bill, 2024)* na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**29 AGOSTI, 2024**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE, WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU AKIWASILISHA MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA HIFADHI YA JAMII WA MWAKA 2024 (THE SOCIAL SECURITY LAWS (AMENDMENTS) BILL, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 (The Social Security Laws Amendments) Bill, 2024).

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuingoza Nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu na kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dotto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Jenister Joackim Mhagama (Mb), Waziri wa Afya , Mhe.

Balozi, Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Jerry William Slaa (Mb), Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Balozi Mahamoud Thabit Kombo (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki , Mhe. Cosato David Chumi (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Denis Lazaro Londo (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyadhifa wanazozitumikia. Kwa upekee, napenda kumpongeza Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.) kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika. Uchaguzi wake ni kielelezo cha kukubalika Nchi yetu ya Tanzania katika Dunia. Hii ni tafsiri ya juhudi zinazofanywa na Rais wetu katika kuunganisha Tanzania na Dunia kwa upande mwingine. Hongera Rais wetu, Hongera Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ninaishukuru pia Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (Ndc) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaotupatia katika ujenzi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu wakiongozwa na Naibu Waziri, Mhe. Paschal Katambi Patrobas, (Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini), Katibu

Mkuu, Mary Ngelela Maganga na Naibu Katibu Mkuu Zuhura Yunus Abdallah pamoja na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza kwa weledi majukumu yao. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

**Mweshimiwa Spika,** aidha, kwa upekee nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bw. Hamza Johari na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Samweli Maneno, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mbunge waViti Maalum) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Athumani Almas Maige (Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo. Aidha, kwa kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024, kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50, (The National Social Security Fund Act, Cap. 50);

2. Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371, (The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371); na

3. Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263, (The Workers' Compensation Act, Cap. 263).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997 kwa lengo la kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na kuweka muuundo na usimamizi wa Mfuko na masuala mengine yanayohusiana nayo. Tangu ilipotungwa Sheria hii imerekebishwa mara kadhaa. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto katika usimamizi wa Mfuko.

Muswada unapendekeza kufanya marekebisho ya jumla kwa kufuta msamiati "*insured person*" mahali popote katika Sheria unapoonekana na badala yake kutumia msamiati "*member*". Lengo la marekebisho haya ni kutumia msamiati ambao unaakisi tasnia ya Hifadhi za Jami. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha baadhi ya tafsiri ya maneno ili kuweka tafsiri sahihi ya misamiati hiyo. Vilevile, kifungu kimerekebishwa kwa kuongeza misamiati mipya iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kufanya masharti yaliyoainishwa katika Sheria yaeleweke kwa urahisi zaidi.

Kifungu cha 5A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta rejea ya Jedwali la Kwanza kwa kuwa masharti yake yamejumuishwa kwenye kifungu cha 12 cha Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya Sheria kuhusu michango ya kisheria.

Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti ya kumtaka mwajiri kutunza rejesta, kumbukumbu na taarifa nyingine za mwajiriwa. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha usahihi wa kumbukumbu za mwanachama na kuongeza ufanisi katika ulipaji wa mafao. Kifungu cha 11

kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa kwa mwajiri kuweka cheti cha usajili mahali pa kazi katika sehemu inayoonekana kwa urahisi. Marekebisho haya yanalenga kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile kifungu kipya cha 11A kinapendekezwa kuongezwa ili kuwezesha watu waliojiajiri wenyewe katika sekta binafsi kujiunga na kufaidika na mafao ya Hifadhi ya Jamii katika mpango wa uchangiaji kwa mujibu wa Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa Hifadhi ya Jamii kwa watu waliojiajiri.

Kifungu cha 12(1) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha asilimia za kiwango cha uchangiaji kinachopaswa kuwasilishwa na mwajiri kwenye Mfuko. Kifungu cha 12(3) kinapendekezwa kufutwa ili kuruhusu mwajiri kuchangia kwa kiasi kikubwa au kiasi chote. Kifungu cha 12(5) kinapendekezwa kurekebishwa kuainisha namna ya uchangiaji kwa wanachama waliojiajiri.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 12A kinapendekezwa kuongezwa ili kuruhusu mfanyakazi aliyeajiriwa na mwajiri zaidi ya mmoja kuchangiwa na waajiri wote kwa ridhaa yake. Lengo la marekebisho haya ni kumpa mwanachama uhuru wa kuchangiwa na zaidi ya mwajiri mmoja. Aidha, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutumia neno "remitted" badala ya neno "paid". Kifungu cha 14(3) kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza adhabu ya tozo kutoka asilimia tano (5) hadi asilimia mbili na nusu (2.5) inayotozwa na Mfuko kwa mwajiri kwa kuchelewa kuwasilisha michango ya mfanyakazi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha kiasi stahiki cha faini na kupunguza gharama za uendeshaji kwa waajiri na kuweka tozo rafiki na zinazolipika. Vilevile kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Bodi kuondoa michango ya ziada iliyoainishwa chini ya Sheria baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana na Hifadhi ya Jamii. Lengo la marekebisho haya ni kutoa nafuu kwa taasisi zilizoonesha nia ya kutekeleza masharti ya Sheria lakini zinashindwa kulipa adhabu za faini kutokana na changamoto za kifedha.

Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka wajibu kwa Mkurugenzi Mkuu kuhakikisha kuwa hesabu ya kiwango chote imewekwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hata kama kiwango hicho kilikatwa na mwajiri na hakikuwasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Lengo la marekebisho haya ni kulinda maslahi ya wanufaika wa mafao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kubainisha kwa ufasaha masharti yanayohusiana na malipo yaliyofanyika kimakosa. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usimamizi wa michango iliyopokelewa kimakosa kwenye Mfuko. Kifungu cha 18 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa kwenye kifungu cha 74A. Kifungu cha 20(3) kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yanakinzana na taratibu za mfumo wa pensheni.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 23 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuruhusu michango iliyowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi kufikia miaka sabini kuzingatiwa katika ukokotoaji wa malipo ya mafao ya pensheni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa mafao ya pensheni kwa mwanachama ambaye amefikisha umri wa kustaafu lakini hajakidhi vigezo vya kupata pensheni na amekuwa akichangia kuanzia umri wa miaka 61 mpaka 70. Kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha mafao ya ulemavu kwa wanachama ambao wana ulemavu wa kudumu kutokana na majeraha au ugonjwa usiotokana na kazi. Kifungu cha 28A kinapendekezwa kuongezwa ili kumuwezesha Mkurugenzi Mkuu kuteua jopo la madaktari ili kuthibitisha iwapo mwanachama amepata ulemavu wa kudumu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa mafao yanatolewa kwa mnufaika anayestahili.

Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "*thirty three*" na kuweka neno "*thirty six*". Lengo la marekebisho haya ni kuongeza kiwango kinacholipwa kwa wategemezi pale ambapo mwanachama atakuwa amefariki. Kifungu cha 43 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo kwa vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya ambavyo Bodi inaweza

kuingia navyo makubaliano ili kutoa huduma za afya kwa wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 52 na 76 vinapendekezwa kurekebishwa ili kumruhusu mwanachama ambaye hajafikia umri wa kustaafu kutumia sehemu ya mafao yake kama dhamana kwa mkopo wa nyumba. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi kwa kuwa vifungu hivyo vinazuia matumizi ya mafao kama dhamana ya mkopo isipokuwa kwa mkopo wa nyumba kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 20.

Vifungu vya 61 na 71 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa hitaji la Bodi kuwa na akaunti ya akiba. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa matumizi ya misamiati ambayo haitumiki kwenye tasnia ya hifadhi ya jamii. Kifungu cha 72 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza makosa mapya kwa mwajiri anayekataa kujiandikisha na mtu yeyote anayemzuia mkaguzi wakati wa kutekeleza majukumu yake. Aidha, kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hicho pia kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka au afisa wa Mfuko aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua kesi yoyote ya jinai chini ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utekelezaji na usimamizi bora wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 74 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiondolea Bodi jukumu la kuteua afisa kwa ajili ya kufungua shauri la kudai michango. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha shughuli za kila siku za Mfuko zinatekelezwa na maafisa wa Mfuko chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha 74A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka mdaiwa kuweka dhamana ya gharama anapoomba ruhusa ya kujitetea katika kesi za kurejesha michango. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha upatikanaji wa michango ya wanachama shauri dhidi ya mwajiri linapomalizika.

Kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufafanua masharti ya mgawanyo wa mapato yatokanayo na kuuzwa kwa mali ya mwajiri. Kifungu cha 79 kinapendekezwa kurekebishwa ili

kuiondolea Bodi majukumu ya kila siku ya uendeshaji wa Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mfuko.

Kifungu cha 87 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha mamlaka ya mkaguzi kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Aidha, kifungu cha 87A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuitisha taarifa au nyaraka ambazo zipo kwenye himaya ya mtu au taasisi husika. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Mfuko unakua na uwezo wa kupata nyaraka yoyote muhimu au taarifa kadiri itakavyohitajika. Kifungu cha 90 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuyajumuisha mafao yanayolipwa chini ya Sheria hii katika orodha ya masuala yasiyotakiwa kutozwa kodi kama ilivyoorodheshwa katika kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utozaji wa kodi mara mbili kwenye mafao yanayolipwa chini ya Sheria.

Jedwali la Kwanza linapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa katika kifungu cha 12.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371. Sheria hii ilitungwa mwaka 2018 kwa lengo la kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, kuweka uchangiaji na malipo ya mafao ya hifadhi ya jamii kuhusiana na wafanyakazi katika utumishi wa umma na kuweka masuala mengine yanayohusiana na hayo. Tangu ilipotungwa Sheria hii imerekebishwa mara moja. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 3 ili kuboresha tafsiri ya baadhi ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati iliyotumika kwenye Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kichwa cha habari cha Sehemu ya Pili ya Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "PENSION". Lengo la marekebisho haya ni kufanya kichwa cha habari kiendane na maudhui ya Sehemu hiyo. Aidha, kifungu cha 5(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwamba waajiriwa wa kampuni ambayo Serikali inamiliki angalau asilimia thelathini ya hisa ni lazima wasajiliwe kwenye Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utendaji kazi wa Mfuko na kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria.

Kifungu cha 17 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti yanayohusiana na usajili wa wanachama wa Mfuko. Aidha, mapendekezo ya marekebisho yanalenga kumuondolea mwajiri majukumu ya kuwasilisha ripoti ya fedha kwenye Mfuko na badala yake kuhakikisha mwajiri anatunza kumbukumbu za waajiriwa wake. Kifungu cha 18 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayobainisha afisa mwenye wajibu wa kuwasilisha michango kwenye Mfuko kuhusiana na waajiriwa wa taasisi ambao mishahara yao hailipwi na Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya Sheria.

Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiwezesha Bodi kuondoa michango ya ziada iliyoainishwa chini ya Sheria baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana na Hifadhi ya Jamii Lengo la marekebisho haya ni kutoa nafuu kwa taasisi zilizoonesha nia ya kutekeleza masharti ya Sheria lakini zinashindwa kulipa adhabu za faini kutokana na changamoto za kifedha. Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti yanayohusiana na kumbukumbu za michango ya mwajiriwa pindi itakapohitajika. Lengo la marekebisho haya ni kumuwezesha mwanachama kupata historia ya uchangiaji wake kwenye Mfuko.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 24 kinapendekezwa kufutwa. Lengo la marekebisho haya ni kuondokana na dhana iliyojengwa katika kifungu hicho inayoruhusu mwanachama kutoa kiasi cha mchango wake katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kuondolewa

uanachama inakinzana na kanuni za Hifadhi ya Jamii kutokana na dhana ya kifungu hicho kutumiwa kwenye Mfuko wa Akiba na siyo katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwamba mnufaika wa mafao ambaye kwa kipindi husika anatumikia kifungo anaweza kuridhia kwa maandishi kwamba mafao yake au sehemu yoyote ya mafao yake ilipwe kwa mnufaika atakayetajwa. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ushiriki wa mtu anayetumikia kifungo katika utoaji wa mafao yake kwa mnufaika.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 47 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti yanayohusiana na kutokuhamishika kwa mafao ya wanachama. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi, kulinda ustawi wa wanachama na mafao yao. Kifungu cha 48 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa dhana ya mafao yasiyodaiwa haitumiki katika kanuni za msingi za hifadhi ya jamii. Aidha, lengo la marekebisho haya ni kumuwezesha mnufaika kudai mafao yake pasipo na ukomo wa muda.

Kifungu cha 51 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuwianisha na masharti yanayohusu upitishwaji na uwasilishwaji wa makadirio ya bajeti. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha ufafanuzi na mfanano kwa masharti yanayoendana. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa dhana ya akaunti ya akiba haitumiki kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii.

Kifungu cha 58 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuboresha masharti yanayohusiana na utekelezaji wa mapendekezo ya uthaminishaji wa ustahimilivu wa Mfuko. Kifungu cha 59 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuuwezesha Mfuko, kwa ridhaa ya Bodi kufungua na kuendesha zaidi ya akaunti moja ya benki.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263. Sheria hii ilitungwa mwaka 2008 kwa lengo la kuweka masharti ya fidia kwa wafanyakazi kutokana na kifo au ulemavu wa kudumu unaosababishwa na majeraha au magonjwa yanayotokana na

utekelezaji wa majukumu ya mfanyakazi mahali pa kazi. Tangu ilipotungwa Sheria hii imerekebishwa mara tatu. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 14 ili kuiwezesha Bodi kubadili au kuondoa sharti lolote linalohusiana na malipo ya mafao chini ya Sheria pale ambapo kuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Bodi kuruhusu malipo ya mafao endapo mnufaika atashindwa kukidhi masharti kwa sababu za  msingi.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha matumizi ya ukomo wa muda kuanza kuhesabiwa kuanzia tarehe ya kutokea kwa ugonjwa husika. Vilevile, kifungu tajwa kinapendekezwa kurekebishwa ili kumruhusu Mkurugenzi Mkuu kuzingatia madai ya fidia pale ambapo taarifa iliwasilishwa na mwajiriwa ndani ya muda japokuwa mwajiri aliwasilisha madai hayo nje ya muda.

Kifungu cha 42(3) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu vyama vya wafanyakazi au mtu mwingine yeyote kuwawakilisha waajiriwa katika madai ya fidia katika Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia mgongano wa maslahi kwa kuwa maafisa Kazi  na Wakaguzi wa wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi ni sehemu ya watu wanaotekeleza Sheria hii.

Kifungu cha 48(6) kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha mwajiriwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu kuendelea kupokea pensheni hata baada ya kurejea kazini au kupokea mafao ya uzeeni. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kati ya wanufaika ambao wanapokea mafao kwa mkupuo na wanaopokea pensheni.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 58(2) kinapendekezwa kufutwa ili kutojumuisha motisha katika mshahara unaotumika kwenye

ukokotoaji wa fidia ili kuweka usawa kwa wanufaika katika malipo ya fidia.

Kifungu cha 73 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa masharti yanayowalazimisha waajiri kuwasilisha taarifa ya mapato ya mwaka katika Mfuko kila ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka kwa kuwataarifa zinawasilishwa na waajiri wanapowasilisha michango ya kila mwezi husika. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Mkurugenzi Mkuu kuitisha taarifa hizo wakati wowote.

Kifungu cha 75(2) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "interest" na badala yake kuweka neno "additional assessment". Lengo la marekebisho haya ni kutumia maneno sahihi yanayoakisi utekelezwaji wa Sheria. Aidha, kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Mfuko kurejesha michango ya waajiri iliyolipwa kwa ziada au kimakosa. Kifungu cha 82 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondokana na matakwa ya lazima ya kuwa na akaunti ya akiba na kuondoa jukumu la kufungua akaunti kwa Waziri na kuweka jukumu hilo kwa Bodi ya Wadhamini.

Kifungu cha 85 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu Mfuko kuwasilisha kwa Bodi ndani ya miezi 6 taarifa ya mwaka kuhusu shughuli za Mfuko katika mwaka wa fedha na taarifa ya fedha iliyokaguliwa ndani ya mwezi mmoja baada ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kumaliza ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, Miswada hii yote inalenga kutatua changamoto ambazo kwa upande mmoja, wanachama wetu wanapata wanapofikia katika kipindi cha kufaidi matunda ya utumishi wao. Miswada hii imefafanuliwa vizuri kwa vipengele vyake na kueleza nia ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutatua changamoto ikiwemo ile ya mkwamo wanaoupata watumishi wanapostaafu na kukutana na kizingiti cha Waajiri kutowasilisha michango kwa wakati kwenda kwenye Mifuko na kuongeza makusanyo; uonevu wakati wa kuwapatia haki wafanyakazi wanaoumia makazini na anayepaswa kutoa taarifa

anaposhindwa kutoa taarifa ndani ya muda; malipo yasiyo ya lazima na kulinda watumishi katika stahiki zao; kwa Waajiri kuwapa ulinzi wa taarifa, na kuwajengea mazingira wachangie na kuwapa nafuu katika malipo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 (The Social Security Laws Amendments) Bill, 2024) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA.

Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
**29 Agosti 2024**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, kwenye Taarifa yako Mheshimiwa Waziri wakati ukiishukuru Kamati ulimtaja Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kama Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Nimeletewa Taarifa hapa Makamu Mwenyekiti ni Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida.

Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge zitarekebishwa pia, na kwenye Taarifa yako urekebishe. Sasa namwita Mheshimiwa

Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024),* kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024 ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Nne, Kikao cha Kumi na Tatu kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 15 Februari, 2024, kwa mujibu wa Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuufanya Muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa Muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 24(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing)* tarehe 15 na 16 Agosti, ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

(i) Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*);

(ii) Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA);*

(iii) *Congress of Tanzania Trade Unions (COTTU);*

(iv) *Institute Social Work;* na

(v) Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Agosti, 2024, Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya

marekebisho katika ibara zinazoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2024)* ukiwa umegawanyika katika sehemu nne na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii, Sura ya 50 *(The National Social Security Fund Act, Cap. 50);*

(b) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 *(The Public Service Social Security Fund Act, Cap.371);* na

(c) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *(The Workers Compensation Act. 263)*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya 1 inayohusu jina fupi na Ibara ya 2 inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu unaofanya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Hifadhi ya Jamii. Kwa kiasi kikubwa Kamati imeridhishwa na maudhui ya Muswada huu kwa kuwa yamezingatia maslahi mapana ya wanachama wa mifuko hii, na hivyo kuleta chachu ya maendeleo ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, ni wito wa Kamati kwa Serikali kuendelea kufanya maboresho ya Sheria kwa mtazamo wa kuongeza tija na ukuaji wa sekta mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii, Sura ya 50 *(The National Social Security Fund Act, Cap. 50)* Sehemu hii inahusu Ibara ya 3 hadi ya 35 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya misamiati mahususi katika tasnia ya hifadhi za jamii, kumwongezea mwajiri wajibu wa kutunza kumbukumbu za mwajiriwa, kuruhusu watu waliojiajiri katika sekta binafsi kuchangia kwenye mifuko ya hifadhi za jamii na kumpa Waziri mwenye dhamana wajibu wa kutunga Kanuni zitakazoanisha utaratibu wa uchangiaji na viwango kwa watu waliojiajiri katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyojitokeza katika mapendekezo ni utaratibu wa mtu aliyeajiriwa na zaidi ya mwajiri mmoja kuchangiwa kwenye mfuko na waajiri wote. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kupunguza faini kwa mwajiri anayechelewa kuwasilisha michango ya mwajiriwa katika mfuko kutoka faini ya 5% hadi 2.5%. Halikadhalika Bodi imepewa mamlaka ya kusamehe faini kwa mwajiri aliyechelewa kuwasilisha michango ya mwanachama kwenye mfuko.

Mheshimiwa Spika, pia, limejitokeza suala la kumpa Mkurugenzi Mkuu wajibu wa kuhesabu kwamba kiwango cha michango ya mwajiriwa kimekamilika hata kama mwajiri alimkata mwajiriwa lakini hajawasilisha kwenye mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mwanachama kulipwa mafao

yake hata kama mwajiri hajawasilisha michango yake kwenye mfuko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ruhusa kwa michango inayowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi miaka 70 kuzingatiwa katika ukokotoaji wa malipo ya mafao ya pensheni kwa mwanachama ambaye amefikisha umri wa kustaafu lakini hajakidhi vigezo vya kupata pensheni. Mengine zaidi ni ongezeko la kiwango cha malipo wanayolipwa wategemezi pale ambapo mwanachama anafariki na ruhusa ya mwanachama kutumia sehemu ya mafao yake kuweka dhamana kwa mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 *(The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 36 hadi 54 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kubadilika na marekebisho ya sheria inayopendekezwa. Mambo hayo ni pamoja na kuongeza Maafisa Masuuli wa Taasisi ambazo mishahara yao hailipwi na Hazina kuwa na wajibu wa kuwasilisha michango kwenye mfuko, kuipa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko uwezo wa kuondoa au kupunguza faini za michango iliyochelewa kutoka kwa mwajiri.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni kuweka utaratibu wa mamlaka za idhini za Menejimenti, Bodi na Waziri katika kuandaa, kupitisha na kuridhia bajeti ya mwaka ya mfuko. Pia kuweka masharti kuhusu utekelezaji wa matokeo ya tathmini katika urejeshwaji wa hali ya uhimilivu wa mfuko katika kulipa mafao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 262 *(The Workers Compensation Act, Cap. 263)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 55 hadi 64 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga kuipa Bodi ya Wadhamini mamlaka ya kusamehe baadhi ya masharti ya kulipa fidia ili kulinda haki ya fidia kwa wanachama, kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kupokea madai yaliyowasilishwa na mwajiriwa ndani ya muda.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni ukomo wa miezi 12 wa kuwasilisha madai yanayotokana na kifo kilichotokea nje ya nchi ihesabiwe kuanzia tarehe ya kifo, kuondoa ukomo wa malipo ya pensheni kwa mwajiriwa aliyerejea kazini au kwa aliyeanza kupokea malipo ya pensheni ya uzeeni na kuweka masharti ya kuwezesha mfuko kurejesha kwa waajiri michango iliyolipwa kimakosa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Isipokuwa baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha Muswada kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii, Sura ya 50 *(The National Social Security Fund Act, Cap. 50)*, Ibara ya 5 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 kinachohusu tafsiri ya maneno. Muswada unapendekeza kufanya tafsiri ya neno '*member*', ambapo tafsiri hii limetumika neno '*employee*' na '*worker*'. Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka kuwa neno *worker* lifutwe kwenye tafsiri ya neno '*member*' kwa kuwa neno '*worker*' halijatolewa maana katika sheria na halitofautiani na neno '*employee*'. Aidha, Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini na Sheria ya Taasisi za Kazi hazijatoa ufafanuzi wa neno '*worker*'. Maboresho haya yanalenga kuondoa mkanganyiko katika kufanya tafsiri ya neno hilo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 11(A) kinachohusu usajili wa watu waliojiajiri. Mapendekezo haya yanalenga kuweka masharti kuwa mtu aliyejiajiri akitaka kuwa mwanachama wa mfuko atatakiwa

kuchangia kila mwezi na endapo atashindwa kuchangia kwa miezi sita mfululizo bila kueleza sababu ya msingi, basi Mkurugenzi Mkuu atathibitisha uanachama wake na atabadilishwa kuwa mwanachama wa Mfuko wa Ziada *(Supplementary Scheme)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu hiki kimempa mamlaka Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni zitakazoweka utaratibu wa kuchangia na viwango. Kamati ilishauriana na Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya watu waliojiajiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Kanuni zitakazotungwa na Waziri zimruhusu mwanachama kuchangia kwa mkupuo, lakini mchango wake uweze kufidia miezi ya mbele kwa kugawa kulingana na uchangiaji wake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu waliojiajiri vipato vyao vinabadilika na pia hutegemea msimu hivyo utaratibu huu utamsaidia mwanachama kumudu uchangiaji kwa masharti yaliyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na Kamati na kueleza kuwa Kanuni zitakazotungwa na Waziri zitaainisha mazingira ambayo yatamfanya mtu aliyejiajiri kutolazimika kuchangia kwa mfululizo iwapo uchumi wake utabadilika kwa sababu zitakazotajwa kwenye Kanuni na kulipa kulingana na malimbikizo anayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12(c) inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14(3) cha sheria kinachohusu mamlaka ya Bodi kusamehe faini. Muswada unapendekeza kuipa Bodi ya Wadhamini mamlaka ya kuondoa au kupunguza faini zinazotokana na michango iliyocheleweshwa na mwajiri kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Kamati ilishauri kuwa, bodi kabla ya kusamehe faini ipate idhini ya Waziri mwenye dhamana. Lengo ni kumfanya Waziri kuwa sehemu ya mchakato wa kusamehe tozo kwa kuwa mamlaka yake ndiyo yatakayotekeleza uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 74(a) kinachohusu haki ya kufanya utetezi wa mashauri ya madai ya michango ya wanachama.

Kifungu hiki kinaweka masharti yanayomtaka mdaiwa kuweka dhamana Mahakamani ya kiwango cha michango anayodaiwa pindi anapoomba ruhusa ya kujitetea katika Kesi ya Michango Mahakamani. Kamati ilishauri kifungu hiki kiboreshwe kwa kuanzia na maneno *"Notwithstanding with the provision of Order XXXV Rule 3,"* ili kuonesha ulazima wa malipo ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanalenga kuondoa mgongano wa Vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai na Sheria hii. Tunaipongeza sana Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kufanya maboresho katika Kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32(b) inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 87(4) cha Sheria kinachohusu watu watakaohusika katika ukaguzi. Kifungu hiki kinalenga kumpa mamlaka mkaguzi kushirikiana na Maafisa wa Taasisi nyingine za Serikali katika kufanya ukaguzi ambapo Afisa wa Polisi ni miongoni mwa Maafisa hao. Katika mahojiano baina ya Kamati na Serikali ilikubaliana kumfuta Afisa wa Polisi. Lengo la ushauri huu lilikuwa ni kuondoa uhasama utakaoweza kujitokeza baina ya mfuko na waajiri ikiwa mchakato ungemhusisha Afisa wa Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 *(The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371);* Ibara ya 43(b) inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 19 cha Sheria kinachohusu Mamlaka ya Bodi ya Wadhamini kusamehe faini.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kuipa Bodi ya Wadhamini mamlaka ya kuondoa au kupunguza faini zinazotokana na michango iliyocheleweshwa na mwajiri kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Kamati ilishauri kuwa, kabla ya kusamehe faini, Bodi ipate idhini ya Waziri mwenye dhamana. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *(The Workers Compensation Act, Cap. 263)*; Sehemu hii inahusu ibara ya 55 hadi 64 ya Muswada. Ibara ya 62(b) ya Muswada inaweka sharti la mfuko kuweza kurejesha kwa waajiri michango iliyolipwa kimakosa. Kifungu kinarekebishwa kwa kutumia neno "*may*". Katika majadiliano na Serikali, Kamati ilishauri neno "*may*" liondolewe na badala yake liwekwe neno "*shall*", ili kulazimisha malipo yaliyolipwa kimakosa yarudishwe kwa mwajiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kulingana na mapendekezo ya Kamati. Lengo la ushauri huu ni kulinda fedha ya mwajiri iliyolipwa kimakosa ili iweze kumsaidia kufanya shughuli nyingine za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni na ushauri wa ujumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na Hifadhi za Jamii nchini, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ihakikishe inalinda maslahi mapana ya mwanachama pindi itakapotunga Kanuni kwenye vifungu ambavyo Waziri amepewa dhamana kwa ajili ya uendeshaji kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa.

(b) Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii *(NSSF)* uhakikishe unaweka mpango wa motisha mbalimbali ili kuwavutia wananchi waliojiajiri kwenye sekta binafsi kujiunga kwa wingi kwenye mfuko.

(c) Kuna umuhimu wa Bodi ya Wadhamini kuzingatia sababu za msingi za kufuta faini kwa waajiri waliochelewesha michango ili kuhakikisha kuwa waajiri wanazingatia sheria na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

(d) Serikali ihakikishe inaboresha Mfumo wa TEHAMA ili wanachama waweze kupata taarifa za michango yao kutoka kwa waajiri kila mwezi kwenye simu zao za kiganjani ili kuondoa tatizo la wanachama kutolipwa mafao kwa wakati kutokana na kutopelekwa kwa michango yao kwenye mfuko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndugu Onorius Njole pamoja na Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kufanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**29 AGOSTI, 2024**

**MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA HIFADHI YA JAMII 2024 *[THE SOCIAL SECURITY LAWS (AMENDMENTS) BILL, 2024]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 *Maelezo ya Awali*

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadihi ya Jamii ya Mwaka 2024 (*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024*), kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023,

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na Kumi na Nne, Kikao cha Kumi na Tatu kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 15 Februari, 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 *Namna Uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika*

**Mheshimiwa Spika**, hatua za kuufanya muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwaajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa muswada ulifanywa na kuwasilishwa

kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 24(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 15 na 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo:-

1. Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*);

2. Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA);*

3. *Congress of Tanzania Trade Unions (COTTU);*

4. *Institute Social Work*;

5. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu. Mnamo tarehe 20 Agosti, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika Ibara zinazoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### *2.1 Utangulizi*

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *[The Social Security Laws (Amendments) Act, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu Nne (4) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu (3) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheri hizo kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

(a) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamiili, Sura ya 50 (*The National Social Security Fund Act, Cap. 50*)

(b) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371; (*The Public Service Social Security Fund Act, Cap.371*)

(c) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263; (*The Workers Compensation Act. 263*)

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

***2.2 Sheria zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake.***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu unaofanya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Hifadhi ya Jamii. Kwa kiasi kikubwa Kamati imeridhishwa na maudhui ya Muswada huu kwakuwa yamezingatia maslahi mapana ya Wanachama wa Mifuko hii, na hivyo kuleta chachu ya maendeleo ya sekta ya Hifadhi ya Jamii, aidha ni wito wa Kamati kwa Serikali kuendelea kufanya maboresho ya Sheria kwa mtazamo wa kuongeza tija na ukuaji wa sekta mbalimbali nchini

**2.2.1** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamiili, Sura ya 50 (*The National Social Security Fund Act, Cap. 50***. Sehemu hii inahusu Ibara ya 3 hadi 35 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni Matumizi ya misamiati mahususi katika tasnia ya hifadhi za Jami, kumwongezea mwajiri wajibu wa kutunza kumbukumbu za mwajiriwa, kuruhusu watu waliojiajiri katika sekta binafsi kuchangia kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii na kumpa Waziri mwenye dhamana wajibu wa kutunga Kanuni zitakazoanisha utaratibu wa uchangiaji na viwango kwa watu waliojiajiri katika sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine yaliyojitokeza katika mapendekezo ni utaratibu wa mtu aliyeajiriwa na zaidi ya mwajiri mmoja kuchangiwa kwenye Mifuko na Waajiri wote.

Aidha Mapendekezo haya yanalenga kupunguza faini kwa mwajiri anayechelewa kuwasilisha michango ya mwajiriwa wake kwenye Mfuko kutoka faini ya asilimia tano mpaka asilimia 2.5. Halikadhalika Bodi imepewa mamlaka ya kusamehe faini kwa

mwajiri aliyechelewa kuwasilisha michango ya mwanachama kwenye Mfuko. Limejitokeza pia suala la kumpa Mkurugenzi Mkuu wajibu wa kuhesabu kwamba kiwango cha michango ya mwajiriwa kimekamilika hata kama Mwajiri alimkata mwajiriwa lakini hajawasilisha kwenye mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Mwanachama kulipwa mafao yake hata kama mwajiri hajawasilisha michango yake kwenye Mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo lingine ni ruhusa kwa michango inayowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi miaka sabini kuzingatiwa katika ukokotoaji wa malipo ya mafao ya pensheni kwa mwanachama ambaye amefikisha umri wa kustaafu lakini hajakidhi vigezo vya kupata pensheni. Mengine zaidi ni ongezeko la kiwango cha malipo wanayolipwa wategemezi pale ambapo mwanachama anafariki na ruhusa ya mwanachama kutumia sehemu ya mafao yake kuweka dhamana kwa mikopo ya nyumba.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 (*The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371*).** Sehemu hii inahusu ibara ya 36 hadi 54 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Katika sheria hii yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kubadilika kwa marekebisho ya sheria inayopendekezwa, mambo hayo ni pamoja na kuongeza maafisa masuhuli wa taasisi ambazo mishahara yao hailipwi na Hazina kuwa na wajibu wa kuwasilisha michango kwenye Mfuko, Kuipa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko uwezo wa kuondoa au kupunguza faini za michango iliyochelewa kutoka kwa mwajiri.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine ni kuweka utaratibu wa mamlaka za idhini za Menejimenti, Bodi na Waziri katika kuandaa, kupitisha na kuridhia Bajeti ya Mwaka ya Mfuko. Na pia kuweka masharti kuhusu utekelezaji wa matokeo ya tathmini katika urejeshwaji wa hali ya uhimilivu wa Mfuko katika kulipa mafao.

**2.2.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 262 (*The Workers Compensation Act, Cap. 263*).** Sehemu hii inahusu ibara ya 55 hadi 64 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga kuipa Bodi ya wadhamini mamlaka ya kusamehe baadhi ya masharti ya kulipa fidia ili kulinda haki ya fidia kwa wanachama, kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kupokea madai yaliyowasilishwa na mwajiriwa ndani ya muda.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine ni ukomo wa miezi 12 wa kuwasilisha madai yanayotokana na kifo kilichotokea nje ya nchi ihesabiwe kuanzia tarehe ya kifo, kuondoa ukomo wa malipo ya pensheni kwa mwajiriwa aliyerejea kazini au kwa aliyeanza kupokea malipo ya pensheni ya uzeeni. Na kuweka masharti ya kuwezesha Mfuko kurejesha kwa waajiri michango iliyolipwa kimakosa.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Isipokuwa baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1 Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii, Sura ya 50 (The National Social Security Fund Act, Cap. 50

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 iinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 kinachohusu Tafsiri ya Maneno. Muswada unapendekeza kufanya tafsiri ya neno "*Member*" ambapo katika tafsiri hiyo limetumika neno "*Employee***"** na "*Worker*". Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka kuwa neno "*worker*" lifutwe kwenye tafsiri ya neno "*Member*" kwakuwa neno "*worker*" halijatolewa maana katika sheria na halitofautiani na neno "*employee*". Aidha Sheria ya Ajira na

Mahusiano kazini na Sheria ya Taasisi za Kazi hazijatoa ufafanuzi wa neno "worker". Maboresho haya yanalenga kuondoa mkanganyiko katika kufanya tafsiri ya neno hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 9 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 11A kinachohusu usajili wa watu waliojiajiri. Mapendekezo haya yanalenga kuweka masharti kuwa mtu aliyejiajiri akitaka kuwa mwanachama wa Mfuko atatakiwa kuchangia kila mwezi na endapo atashindwa kuchangia kwa miezi sita mfululizo bila kueleza sababu ya msingi basi Mkurugenzi Mkuu atadhibitisha uanachama wake na atabadilishwa kuwa mwanachama wa Mfuko wa Ziada (Supplimentary Scheme). Aidha Kifungu hiki kimempa mamlaka Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni zitazoweka utaratibu wa kuchangia na viwango.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishauriana na Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya watu waliojiajiri. Kamati ilikuwa na maoni kuwa Kanuni zitazotungwa na Waziri ziruhusu wanachama kuchangia kwa mkupuo lakini mchango wake uweze kufidia miezi ya mbele kwa kugawa kulingana na uchangiaji wake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu waliojiajiri vipato vyao vinabadilika na pia hutegemea msimu hivyo utaratibu huu utasaidia mwanachama kumudu uchangiaji kwa masharti yaliyopendekezwa. Serikali ilikubaliana na Kamati na kueleza kuwa Kanuni zitakazotungwa na Waziri zitaanisha mazingira ambayo yatamfanya mtu aliyejiajiri kutolazimika kuchangia kwa mfululizo iwapo uchumi wake utabadilika kwasababu zitakazotajwa kwenye Kanuni na kulipa kulingana na malimbikizo anayodaiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 12(c) inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14(3) cha Sheria kinachohusu mamlaka ya Bodi kusamehe faini. Muswada unapendekeza kuipa Bodi ya Wadhamini mamlaka ya kuondoa au kupunguza faini zinazotokana na michango iliyocheleweshwa na Mwajiri kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Kamati ilishauri kuwa Bodi kabla ya kusamehe faini ipate idhini ya Waziri mwenye dhamana. Lengo ni kumfanya Waziri kuwa sehemu ya Mchakato wa

kusamehe tozo kwakuwa mamlaka yake ndiyo itakayotekeleza maamuzi hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 28 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 74A kinachohusu haki ya kufanya utetezi wa mashauri ya madai ya michango ya wanachama. Kifungu hiki kinaweka masharti yanayomtaka mdaiwa kuweka dhamana mahakamani ya kiwango cha michango anayodaiwa pindi anapoomba ruhusa ya kujitetea katika kesi ya michango mahakamani. Kamati ilishauri Kifungu hiki kiboreshwe kwa kuanza na maneno *"Notwithstanding with the provison of Order XXXV Rule 3…* ili kuonesha ulazima wa malipo ya dhamana. Marekebisho haya yanalenga kuondoa mgongano wa vifungu vya sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai na Sheria hii. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kufanya maboresho katika Kifungu hiki kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 32(b) inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 87(4) cha Sheria kinachohusu watu watakaohusika katika ukaguzi. Kifungu hiki kinalenga kumpa mamlaka Mkaguzi kushirikiana na Maafisa wa Taasisi nyingine za Serikali katika kufanya ukaguzi ambapo Afisa wa Polisi ni miongoni mwa Maafisa hao. Katika majadiliano baina ya Kamati na Serikali ilikubaliana kumfuta Afisa wa Polisi. Lengo la ushauri huu ilikuwa ni kuondoa uhasama utakaoweza kujitokeza baina ya Mfuko na Waajiri ikiwa mchakato ungemhusisha Afisa wa Polisi.

### 3.2 *Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371* (The Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371)

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 43(b) inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 19 cha Sheria kinachohusu mamlaka ya Bodi ya Wadhamini kusamehe faini. Muswada unapendekeza kuipa Bodi ya Wadhamini mamlaka ya kuondoa au kupunguza faini zinazotokana na michango iliyocheleweshwa na Mwajiri kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Kamati ilishauri kuwa Bodi kabla ya kusamehe faini ipate idhini ya Waziri mwenye

dhamana. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama iliyopendekezwa.

**3.3 Marekebisho ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 (The Workers Compensation Act, Cap. 263).**

Sehemu hii inahusu ibara ya 55 hadi 64 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 62(b) ya Muswada inaweka sharti la Mfuko kuweza kurejesha kwa waajiri michango iliyolipwa kimakosa. Kifungu kinachorekebishwa kimetumia neno "may". Katika majadiliano na Serikali, Kamati ilishauri neno "May" liondolewe na badala yake liwekwe neno "Shall" ili kulazimisha malipo yaliyolipwa kimakosa yarudishwe kwa mwajiri. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kulingana na mapendekezo ya Kamati. Lengo la ushauri huu ni kulinda fedha ya Mwajiri iliyolipwa kimakosa ili iweze kumsaidia kufanya shughuli nyingine za uendeshaji.

**3.4 MAONI NA USHAURI WA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na Hifadhi za Jamii nchini kama ifuatavyo;

a) Serikali ihakikishe inalinda maslahi mapana ya Wanachama pindi itakapotunga Kanuni kwenye vifungu ambavyo Waziri amepewa dhamana kwa ajili ya uendeshaji kwa mujibu wa Marekebisho yaliyofanywa.

b) Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii (NSSF) ihakikishe inaweka mpango wa motisha mbalimbali ili kuwavutia Wananchi waliojiajiri kwenye sekta binafsi kujiunga kwa wingi kwenye Mfuko.

c) Kuna umuhimu wa Bodi za Wadhamini kuzingatia sababu za msingi za kufuta faini kwa waajiri waliochelewesha michango ili kuhakikisha kuwa waajiri

wanazingatia sheria na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

d) Serikali ihakikishe inaboresha Mifumo ya TEHAMA ili Wanachama waweze kupata taarifa za michango yao kutoka kwa waajiri kila mwezi kwenye simu zao za kiganjani ili kuondoa tatizo la wanachama kutolipwa mafao kwa wakati kutokana na kutopelekwa kwa michango yao kwenye Mifuko.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 *Shukrani*

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohammed Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
13. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
16. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
18. Mhe. Neema Kachiki Lugangira, Mb.

19. Mhe. Khamis Yussuf Mussa, Mb
20. Mhe. January Yussuf Makamba, Mb
21. Mhe. Khadija Shaban Taya, Mb

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Paschal Patrobass Katambi (Mb) Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 5.1 *Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja*

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**

29 Agosti, 2024

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa kusoma Maoni hayo ya Kamati ili yaweze kuliongoza Bunge kufanya maamuzi. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu

ama kwenye hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na Mheshimiwa Athuman Almas Maige ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa kupata nafasi hii, lakini awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupatia uhai.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa King, keti kidogo. Samahani.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine pengine wangependa kutoka baada ya kutangazwa. Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo:-

Tunao wanafunzi 92 na walimu nane kutoka Shule ya Awali na Msingi Markaz iliyopo Ukonga, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 32 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari *DCT* Mvumi, Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali King, endelea.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na uzima na leo hii kuja kuangalia Sheria ambayo itakuja kuwasaidia wastaafu kule mbele.

Mheshimiwa Spika, kuna neno moja ambalo linasemwa sana, lakini Muswada huu umekuja kulipunguza nguvu lile neno. Kuna msemo unasema fainali uzeeni. Hili neno linatisha sana. Maana yake unaamini kwamba, matatizo au ugumu wa maisha utakuja kukukuta uzeeni, lakini ujio wa marekebisho haya ya sheria yamepunguza maeneo makubwa sana ya ile fainali uzeeni. Kwa maana hiyo, imepunguza makali ya neno fainali uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii sheria imejikita katika upelekaji wa taarifa, michango na ulipwaji wa wastaafu ambayo kwa sasa hivi

ni kwamba, mstaafu hata kama mchango wake kule haujafika, lakini maelezo yapo anaweza akalipwa. Tunaondoa kile kitu cha mwajiriwa kuanza kutafuta taarifa zake kuzipeleka katika mifuko ya hifadhi. Kwa hiyo, hicho kimeondoka, ina maana kwamba, hilo neno la fainali uzeeni limeondoka au limepungua.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuingizwa kundi la watu waliojiajiri, ina maana kulikuwa kuna watu tulitarajia uzeeni wangeenda kupata matatizo makubwa sana, lakini kwa sasa hata waliojiajiri wenyewe wanao uwezo wa kuingia katika mifuko, wakachangia na baadaye uzeeni wakanufaika. Kwa maana hiyo, inapunguza ukali wa neno hili fainali uzeeni.

Mheshimiwa Spika, pia hii inafanyika Kenya na *South Africa*. Kama ilivyopendekezwa na Ibara ya 9 kwamba, Kifungu 11(a) kimeingizwa kwa ajili ya kufanya hicho kitu.

Mheshimiwa Spika, pia kuongezeka kwa kundi la watu walioajiriwa na zaidi ya mtu mmoja, kuna watu wanafanya kazi kwa nguvu sana, wanatumia muda mwingi sana kufanya kazi, lakini wakishafika uzeeni hawapati kipato kwa mujibu wa kazi ambayo waliifanya. Pengine alikuwa anafanya kazi zaidi ya eneo moja. Kwa maana hiyo, kwa sheria hii imekuwa kama ni mwarobaini. Kwa hiyo, ile fainali uzeeni kidogo itakuwa imepungua. Hii Uganda na Ghana wanafanya.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukitazama watu, mtu wa miaka 60 unaweza ukaangalia kwamba kweli ana uwezo wa kuendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, imetoa fursa nyingine ya miaka 61 – 70 mtu anaweza akachangia katika mfuko na akaja akapata mafao yake baada ya kutimiza umri wa miaka 70.

Mheshimiwa Spika, pia kingine kilichokuja ambacho ni cha faraja ni kama mtu amepata ajali nje ya mfumo wa kazi. Amepata ajali au dharura yoyote ndani ya mfumo wa kazi huwa analipwa na hawa *WCF,* lakini *NSSF* itakuwa inawalipa wale ambao wamepata ulemavu au wamepata matatizo nje ya sehemu ya kazi ambapo pia inaenda kuwanufaisha na kupunguza makali ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ni wategemezi sasa watalipwa kutoka miezi 33 mpaka miezi 36. Pia, waajiriwa wataruhusiwa kutumia dhamana ya michango yao kukopa mkopo wa nyumba. Hili ni jambo la faraja na ni jambo la kuungwa mkono. Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kuweka hiki kitu ambacho kitawanufaisha wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nizungumzie maeneo matatu kwa kutoa ushauri. Tulisema kwamba, *registration* au *self-employed person*, mtu ambaye atakuwa amejiajiri yeye mwenyewe atakuwa anawekewa *scheme* ya kufanya kama Ibara ya 9 ya Muswada ilivyotaka kwa kuongeza Kifungu cha 11.

Mheshimiwa Spika, faida ya hapa ni kwamba kule mbele ilikuwa tuwe na wategemezi wengi, lakini sasa wale wategemezi watapungua baada ya kwamba mtu amejichangia yeye mwenyewe kule mbele anapokwenda. Ila, uhalisia wa mazingira ya watu waliojiajiri binafsi kwamba ni mazingira pekee, wengine wapo kwa msimu na wengine kipato kitakuwa hakijanyooka. Kwamba, kila mwezi kitakuwa kinaingia kile cha ziada, ila sheria hii ilisema inampa nguvu Waziri kutengeneza Kanuni.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi hofu yangu ni hapa kwenye kutengeneza kanuni ambazo zitaendana na mapato halisi, maana mambo mengi tukishatoka hapa baada ya sheria, kanuni itakapokuja pengine tafsiri yake isiwe vile kama tulivyolenga katika kupitisha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Waziri amepewa uwezo huu wa kutengeneza kanuni, basi akatengeneze kanuni kwa mujibu wa mazingira ambayo tunayo. Mtu ambaye ana uwezo wa kupata kwa pamoja labda anaweza hata akalipia mbele, kuna wengine wafugaji, wakulima, wavuvi na wafanyabiashara ndogo ndogo. Tukaangalia haya mazingira na kipato chao kinavyokuwa, ili tutengeneze hiyo Kanuni, basi iwe tumeishona kwa mujibu wa mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nilishauri ni Ibara ya 12 ya Muswada, imefanyia mabadiliko Kifungu cha 14(3)

ambapo tumepunguza kile wanasema *addition contribution*, mchango au tozo ya ziada. Tozo ya ziada imepunguzwa kutoka asilimia tano mpaka asilimia mbili na nusu kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ingawa tumejadiliana na Serikali, tumekubaliana na hili jambo, lakini nizungumze kitu kimoja kwamba hoja ilizozitoa Serikali ni sahihi. Moja, ni kwamba, kwa mwaka inakuwa ni 60% kwa sababu kila mwezi ni asilimia tano ambayo ni sawa, lakini ni mzigo mzito kwa mwajiri, anashindwa kulipa madeni ambayo ilikuwa awalipie wale waajiriwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hili *okay,* tunakubaliana. Hoja nyingine unasema kwamba, Rwanda wao wanakwenda katika asilimia tatu. Tunakubaliana sasa asilimia tatu ni sawa, lakini kuwavutia wawekezaji kama ilivyopendekezwa katika *blue print* ni sawa, ila ni angalizo, kwa asilimia hii twende kwa kipindi cha kuangalia, cha mpito, ili tukifika kule mbele kama yale malengo hayajafikiwa, basi turudi *at least* twende tu karibu na Rwanda kwa sababu, inawezekana.

Mheshimiwa Spika, ukitoa *penalty* nje ya boksi huku katika boksi watu watashikana sana maana umepunguza ile adhabu. Kwa hiyo, naiomba Serikali tuangalie katika kipindi maalum.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nalichangia la ujumla ni kwamba, huu Muswada mzima ukiutazama tunazungumzia taarifa, ufikishwaji wa michango na ulipwaji wa pensheni. Ina maana tunazungumzia sana *information* na utagundua kwamba, upatikanaji wa mfumo kwa wadau wote utakuwa siyo mzuri. Ina maana tungekuwa na mfumo wa kielektroniki au mfumo wa kompyuta ambao utawezesha hawa wadau wote wakawa katika mfumo mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati tuna *strength* ya mkongo wa Taifa ambao utawezesha kufanyika hiyo kazi kirahisi. Pia tuna *Data Center* pale Kijitonyama. Ina maana kila mtu akishakuwepo katika *Data Centre* tunaweza tukaitumia *Data Centre*. Sasa hivi vile vile tuna vijana wengi waliosoma na wanaweza kutengenza mifumo ikawa inakubalika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijaribu

kupitia hizi taasisi za Hifadhi ya Jamii, kuwaunganisha watu iwe sasa hakuna kwenda kudai taarifa hii haijafika au mchango haujafika.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye uchambuzi wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii Na. 3 ya mwaka 2024. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia wasaa huu wa kuweza kutoa mawazo yangu katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona haja sasa ya kutuletea marekebisho haya ya sheria ambayo yatakwenda kutibu matatizo mengi ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hiyo, hongera sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyoweza kutufafanulia na kufanya nao kazi vizuri kwa pamoja mpaka mwisho kwa kumaliza leo Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati yetu pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii. Sisi sote

tulishirikiana kwa pamoja kuhakikisha tunafanya kazi kwa umahiri mkubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu natarajia kuchangia katika kifungu Na. 14, 17, 57 na 43 kwa Sheria ya *PSSSF* na 45 kwenye *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Kifungu Na. 17, Kifungu hiki kinaruhusu wale ambao walichelewa kuanza kazi au wale ambao walikuwa wana umri mkubwa kuweza kuchangia katika mfuko huo na kupata mafao. Katika nchi yetu ya Tanzania na nchi nyingine, sote tunajua changamoto ya ajira kwa vijana. Vijana wetu wamekuwa wakitafuta kazi kwa muda mrefu sana, mpaka wanafikia katika kipindi cha umri wa miaka 40 au 45 hawajapata ajira. Sasa, anapokwenda kwenye kupata pensheni muda wa uchangiaji wake unakuwa mfupi mno kiasi kwamba anaweza amalize wakati wa kazi na kustaafu na hajawa katika eneo la pensheni, yaani hajaingia kwenye mfumo wa pensheni.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sheria hii inayoenda kuboreshwa na kurekebishwa, itamruhusu mchangiaji yule ambaye umri wake, kama ameanza kazi miaka 45 au 50 basi atakapokwenda hadi 60 sasa mfuko utamruhusu kuendelea mpaka hata kufikia umri wa miaka 65 au 67 na kupata pensheni yake vizuri sana. Hilo ni jambo kubwa katika nchi yetu, tunajua changamoto hizo zinawakuta wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, hata watu wazima wapo ambao hawakupitia kwenye mfumo huo, lakini wamejiajiri wenyewe. Sasa katika kujiajiri wenyewe hata kama amevuka umri anaweza akachukua kiasi kidogo akahifadhi kwenye mifuko na baadaye akafaidika kwa kupata pensheni. Ni jambo kubwa lililofanywa na Serikali, nawapongeza mno kwa kuliona hilo. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitaangalia kwenye kifungu cha 57, *WCF* kuongeza muda wa fidia wa mwaka mzima sasa. Wafanyakazi wengi walikuwa wanapata ajali mbalimbali wakiwa kazini. Wanapata ajali mbalimbali ndani ya kazi, nje ya kazi,

wanapata *accident* huko njiani na nini, lakini kuna wengine wanakwenda wanakaa, muda unapita, hajui hata anatakiwa afanye nini. Anakuja kushtukia mpaka anapona zaidi ya mwaka au mwaka umefika. Akienda kwenye ku-*claim* malipo yake anaambiwa muda umepita na hustahili tena.

Mheshimiwa Spika, sasa sheria hii inakwenda kulirekebisha hilo. Wametoa muda mrefu sana karibu wa mwaka mzima mfanyakazi aliyeumia, ataugua, Mungu atamjalia atapona labda hata baada ya miezi sita, sasa ataomba mafao yake ya kufidiwa kwa ajili ya ajali au kitu chochote ambacho kimempata. Ni jambo kubwa ambalo Serikali yetu inaenda kufanya, na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, pia kifungu cha 14 *NSSF* na 43 *PSSSF* kuhusu Bodi kushauriana na Mheshimiwa Waziri kutoa msamaha wa tozo; kifungu cha 14 kinaelekeza kupunguza tozo kutoka asilimia tano iliyokuwepo hadi 2.5%. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa wawekezaji wetu na tunajua dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha wanawaweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika vitu ambavyo vinaonesha vilikuwa vinawatesa wawekezaji wetu ni pamoja na tozo zilizozidi. Tozo hii ilikuwa inazidi, mtu anaposhindwa kupeleka michango yake kwa wakati, anawekewa tozo lakini leo Serikali kwa maboresho haya inataka kuipunguza tozo hii ili iwe rafiki na mlipaji wa tozo hiyo. Mlipaji atalipa hiyo tozo, kama ataonesha pia ana matatizo, Bodi inaweza ikakaa yeye akapeleka maombi yake. Bodi kwa kushauriana na Mheshimiwa Waziri wakaona jinsi gani wanaweza kuiondoa au kuiacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwani kuna watu kama wahandisi wanafanya kazi za ukandarasi maeneo mbalimbali. Hawa wana wafanyakazi wengi sana, lakini utakuta hajalipwa fedha zake za ile kazi ambayo ameifanya. Sasa jambo hilo litamfanya yeye ashindwe pia kupeleka ile michango. Sasa kama huyu naye atachukuliwa na kupewa adhabu kubwa itakuwa ni mtihani kwa sababu yeye mwenyewe pia mafao yake

anategemea kupata katika eneo fulani anakuwa hajayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Sheria hii inakwenda kurekebisha kifungu cha 14 na 43 *PSSSF* kupunguza hiyo asilimia tano kuja asilimia mbili. Naipongeza sana Serikali kwa kuangalia mazingira haya, mazingira wezeshi kwa hawa wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mkoa wa Dar es Salaam, una uwekezaji mkubwa wa viwanda na mambo mbalimbali. Sasa hii sheria inaenda kuwasaidia wale wawekezaji wetu. Siyo kwamba tunawaambia wafanye makusudi ili wafutiwe tozo, hapana. Wanapopunguziwa, basi waweze kulipa zaidi, hata mbinu ya ujasiriamali wanakwambia punguza bei, uza sana. Sasa hawa nao wanapunguziwa ili walipe kwa wakati na walipe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna Kifungu cha 45 mwanachama anapokuwa gerezani anaweza akaridhia au akam-*assign* mtu ambaye anaweza kumchukulia mafao yake. Serikali imeweka jambo hili katika Muswada huu katika kurekebisha. Ni jambo jema, ni jambo zuri, kwa sababu tumeona, mtu anapata matatizo na matatizo ya gereza yanampata mtu yeyote, hujaamka, hujafa, hujaumbika, huwezi kujua utaenda kuishia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mtu anaweza akaenda Mahakamani akaambiwa anatakiwa alipe faini, anaambiwa faini ya shilingi milioni moja wakati ana mafao ya shilingi milioni 100, akaingia jela kwa sababu hana, lakini atakapokuwa gerezani, kwa kufuata utaratibu wa kisheria mwanachama huyu atam-*assign* mtu ambaye atakwenda kuchukua mafao kwa ajili yake. Mafao haya yataisaidia familia yake na hata yeye mwenyewe kama *issue* ya kuhaulisha makosa, anatakiwa labda alipe fedha fulani ili aepuke adhabu kubwa, basi anaweza akafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema na ni jambo zuri, naishukuru sana Serikali na ninaipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria hii ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024. Sheria hii itakuwa mwarobaini, inasaidia sana na Serikali tunaishukuru sana kwa kuwakumbuka wafanyakazi wake na wazee waliohudumia nchi hii kwa miaka mingi. Wamekuwa wakipata tabu sana kufuatilia pensheni zao, lakini sheria hii imekuja kurahisisha upatikanaji wa pensheni kwa watu wote wanaodai mafao yao ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu hali hii ilikuwa ngumu sana, watu wametembea kutoka mikoani kufuata pensheni, wengine wamefariki hawajalipwa pensheni zao. Sheria hii imewakumbuka watu wote ambao kwa kweli walikuwa na dhiki hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea vifungu vile vya 5C, 12C, 28, 32B na 43B vya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa sekta binafsi pamoja na *NSSF,* yaani Sura ya 50 na vilevile *PSSSF* Sura ya 371. Marekebisho katika Sheria hizi zote mbili za Hifadhi ya Jamii zinalenga kuwapa nafuu wastaafu waliokuwa wakichelewa kupata mafao yao, lakini wengine kutolipwa kabisa mafao hayo kwa sababu waajiri hawakuchangia michango yao kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wengine wameshindwa kuchangia michango yao kwa sababu ya tozo ambayo ilikusudiwa kwamba ilikuwa ni kubwa sana kutoka asilimia tano ya mchango wa kila mfanyakazi au kila mwanachama wa Mfuko. Sheria hii inapunguza tozo kutoka asilimia tano ile mpaka asilimia mbili nukta tano kwa Mfuko wa *NSSF* na kuachia Mfuko wa *PSSSF* asilimia moja nukta tano. Hii imechukua nafasi zote mbili, kwanza hapo nyuma mwajiri alikuwa anashindwa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa sababu zozote zile hakulipwa kwa miezi tisa kwa kazi aliyoifanya kama mwajiri, labda mkandarasi, ana wafanyakazi 200, amefanya kazi ya barabara, hakulipwa miezi tisa na kuendelea. Ameshindwa kupeleka michango kwa waajiri, lakini baadaye akapata hela, akalipwa na Serikali au mkandarasi aliyempa kandarasi, sasa anaangalia anatakiwa alipe asilimia tano ya tozo *(penalty)*, anashindwa kupeleka kule.

Mheshimiwa Spika, akishindwa kupeleka ile tozo, hata akilipa michango ya wanachama, lakini wanachama wale hawawezi kulipwa kwa sababu hajalipa tozo. Wanachama wakienda kudai pensheni zao kule wanaambiwa mwajiri wenu sawa ameleta michango, lakini hamwezi kulipwa kwa sababu hajaleta tozo na tozo ni kubwa. Sasa baada ya Serikali kuleta Muswada huu tozo itapungua.

Mheshimiwa Spika, iko mifano mizuri, wakati ule tunahangaika na *SDL* ilipokuwa kubwa sana, waajiri kulipa michango ilikuwa ngumu sana, lakini baada ya kupunguza *SDL*, waajiri wanalipa. Pia iko mifano mizuri, Serikali imekuwa inatangaza kuondoa tozo kwa malipo ya viwanja au ardhi na wananchi wengi wanaenda kulipa.

Mheshimiwa Spika, pia marekebisho yanapunguza tozo kwa Mfuko ule wa Serikali na kuacha ikawa asilimia moja nukta tano na tozo hii itakuwa nzuri na inaweza kulipika sasa. Mapendekezo ya sheria hizi yanawapa nguvu Bodi kupunguza au kufuta kabisa tozo kwa waajiri ambao kwa isivyo bahati sana walishindwa kulipa na wana sababu. Hii itafanya waajiri walipe michango ya wanachama na mifuko iweze kuwalipa wanachama wazee wanaodai pensheni zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi katika Miswada hii inayohusu Mifuko ya Hifadhi, lakini pia imekusudiwa kuboresha kwa mfano, wanachama ambao hawakuwepo kwenye mfumo huu wa kupata pensheni kwa kujiwekea wenyewe. Tumeona hapa katika sheria hii yametokea marekebisho kwamba kumbe watu binafsi wanaweza wakajiwekea michango na baadaye

wakalipwa pensheni, lakini kulikuwa na ugumu wa wanachama ambao wameanza kazi wakiwa wana miaka 40 au wana miaka 35, wakafikia mpaka umri wa kustaafu na ikaonekana kwamba hawawezi sasa kuchangia. Italazimu iweje? Wastaafu wasilipwe pensheni.

Mheshimiwa Spika, sasa Muswada huu umeruhusu sasa wanachama hawa ambao walianza kazi wamechelewa, wakafikia umri wa kustaafu, wakaweza kuchangiwa. Wanapofika miaka 69, 70, Mifuko itakokotoa pensheni zao na kufikiria michango waliyotoa ili waweze kulipwa pensheni.

Mheshimiwa Spika, liko suala lingine ambalo lilikuwa huko nyuma halifanyiki, kwa mfano, mwanachama ana uwezo wa kwenda kujilipia, wanasema, wewe bahati mbaya mwajiri wako hajakuchangia na kwa sababu hajakuchangia, huwezi kulipwa. Baadhi ya hawa wastaafu wamekuwa wakienda kukusanya hela mahali fulani, kukopa hela, waje walipie kwenye Mifuko, walipe ile tofauti ya mishahara ya waajiri ili waweze kulipwa. Hili jambo limefutika. Mkurugenzi atafikiria sasa tu mwenyewe kwamba kwa kujua waajiri wote wamewakata hela wanachama hawa na hawakupeleka hela, awalipe wanachama halafu yeye atajuana na waajiri wake. Hili limekuwa jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, kiufupi marekebisho haya katika Miswada hii yameleta mwarobaini wa matokeo ya tabu zilizokuwa huko nyuma kwa watu wanaodai pensheni walipwe malipo yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mheshimiwa Katani Ahmed Katani ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika miswada hii. Namshukuru Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri

wake na watumishi wote, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, wamefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete karibu sana kwenye Wizara yako na kwenye Kamati yetu. Namshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Kamati nzima ya Ustawi wa Jamii, wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, vifungu na sura zote zimetajwa, mimi nilitaka kuchangia katika Mfuko wa Hifadhi ya *WCF* kwenye *Cap* 263 kifungu cha 39. Ilikuwa wakati mtu amepata ajali akiwa mtumishi, akichelewa kupeleka maombi yake ya kulipwa na Mfuko huu, kwa sababu inawezekana kama alikuwa amelazwa au alikuwa nje ya nchi, amechelewa kupeleka maombi, hayapokelewi kutokana na vifungu vilivyokuwepo. Kwa hiyo, tumeondoa vile vifungu vilivyokuwa vinamzuia mtu kupeleka maombi nje ya muda, na tumeongeza muda maana yake yanaweza kupokelewa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyo wazi ni kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapata ajali humu ndani na wakati fulani wanakuwa wanaenda kutibiwa nje (India na nchi nyingine), akija katika Mfuko huu unakuta amechelewa hawapokei. Kwa hiyo, kwa sasa watumishi wote waliopata ajali wanaruhusiwa kupokelewa maombi yao nje ya muda kama tulivyoeleza kwenye hicho Kifungu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48(16) kinahusu walemavu ambao walikuwa wanalipa pensheni kwa kipindi fulani. Kwa hiyo, tumesema mlemavu au walemavu wa kudumu waliopata ajali, walipwe pensheni yao hata kama wakistaafu na baada ya kustaafu katika maisha yao yote walipwe pensheni yao. Kwa hiyo, kifungu kimeruhusu walemavu waliopata ulemavu wa kudumu waendelee kulipwa katika maisha yao yote ya uhai.

Mheshimiwa Spika, katika Sura ya 50 Mfuko wa *NSSF*, inahusu watu binafsi kuweka mapato yao na kupata pensheni yao. Sisi wafugaji na watu wengine binafsi tumekuwa hatuna pensheni yoyote. Mfano unaweza kuwa una maduka yako makubwa tu lakini ukifika miaka 60 au miaka mingapi huwezi kufanya ile biashara unawaachia watoto wafanye na wewe unakuwa hauna

kitu chochote. Kwa hiyo, tumeruhusu wale wafugaji wetu mtu anakuwa na ng'ombe 1,000, ng'ombe 2,000, 4,000, inafika mwisho huna ng'ombe hata mmoja. Tumeweka vifungu vya wenyewe kuchangia katika mfuko huu na wenyewe wapate pensheni kama walivyo wafanyakazi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 14(3), tulikuwa na asilimia tano ya tozo ya faini kwenye Mfuko wa *NSSF*, kwa hiyo tumepunguza mpaka asilimia mbili nukta tano kuwaruhusu waajiri waweze kulipa hizo faini zao ambazo walikuwa wanaweka.

Mheshimiwa Spika, pia katika kifungu hiki tumeongeza Bodi. Tulikuwa tunaangalia nini? Tulikuwa tunaangalia kwamba inawezekana mtu anayedaiwa faini, amechelewa kupeleka makato ya wafanyakazi, siyo kwa sababu yake tu binafsi. Inawezekana kulikuwa hasa watu wanaofanya kazi na Serikali, Serikali inachelewa kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, sasa inapochelewa kuwalipa na wenyewe hawana uwezo wa kulipa, wanalipa yale makato ya wafanyakazi lakini bado wanadaiwa faini ya asilimia tano. Kwa hiyo, tumepunguza mpaka asilimia mbili nukta tano. Pia tumeweka Bodi ya kuchunguza kama kulikuwa na athari ya jambo hilo, walichunguze vizuri waweze kuwaachia hiyo faini ili mtu asipate adhabu ambayo hakustahili kupata.

Mheshimiwa Spika, katika Mfuko wa *PSSSF* Sura 371, tumeweka Bodi ya kufuta 1.5%. Nataka nizungumze hili, watumishi wa Serikali hasa Watendaji wa kata na Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Mitaa, kuanzia mwaka 2006 kurudi nyuma mpaka leo kuna watu hawajapata pensheni yao. Wakienda *PSSSF* wanaambiwa waende wakalipe mafao yao ambayo hayakupelekwa yale makato yao. Mbaya zaidi, Mfuko hausemi wewe nenda kalipe, unamwandikia Mkurugenzi aende akawalipie wapate mafao yao.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi halipi, mtu anaona kama anadaiwa shilingi 2,000,000 au shilingi 3,000,000 anajilipia mwenyewe, lakini ile barua inaonesha kwamba yeye

aliyeandikiwa ni Mkurugenzi. Kwa hiyo, ukiuliza kwenye Mfuko wa *PSSSF* kwamba jamani mnawaandikia watu wajilipie wanasema sisi hatujaandika, lakini ukienda kuangalia unakuta watu wamepewa *control number* na wamelipa wanapata pensheni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watumishi wengi kama Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji na wa Mitaa na wengine wengi ambao makato yao hayakwenda *PSSSF*, hawajalipwa mpaka leo na umetupa nafasi ya kuchunguza hili jambo mpaka mwezi Februari. Nataka nikwambie kwamba nafasi uliyotupa pengine utuongezee nguvu zaidi kwa sababu tulivyoona, matatizo ni makubwa kuliko ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba katika hili suala, mifuko hii, nami nilikuwa natamani, sijaona hicho Kifungu, wanasheria mtatusaidia. Sijaona kifungu ambacho kinasema hivi kwamba mfanyakazi wa Serikali aliyetumikia Taifa hili miaka 40 au miaka 30 amestaafu, akienda kudai madai yake wanamwambia makato yao hayajaletwa na mwajiri wako nenda katafute.

Mheshimiwa Spika, hatujaona Kifungu hicho humu ndani cha kuzuia hayo makato, mtu anayemwambia mfanyakazi nenda kalete makato yako ili ulipwe mshahara au ulipwe mafao yako. Kwa hiyo, nafikiri wanasheria watusaidie tupate Kifungu cha namna hiyo kwa Mfuko wa *PSSSF* ili tuweze kuondoa adhabu ambayo wafanyakazi wanaipata.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yameelezwa sana, mambo ni yale yale tuliyoeleza, lakini tunakushukuru sana kwa kutupa nafasi ya kufuatilia masuala haya. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo ajiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu unaopendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria za Hifadhi

ya Jamii. Kwa kweli haya mabadiliko ni mazuri na ni muhimu sana, yamekuja kwa wakati. Hivyo basi, nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake yote kuona umuhimu wa kuleta marekebisho ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, nawapongeza sana kwa kazi nzuri. Nawapongeza Wajumbe wa Kamati hii muhimu ambao wamechambua vizuri sana, vilevile Watendaji wote wa Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo moyo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo la Watumishi wa nchi yetu. Hakuna ubishi tumeona jinsi ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameona umuhimu na amezingatia sana matakwa yote yanayohusu maslahi ya watumishi wa Tanzania. Nasema haya kwa sababu nimekuwa *site* katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, watumishi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameendelea kujali maslahi ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kidogo kwenye masuala ya mafao, lakini bado wameendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais jinsi ambavyo alichukua hatua ya haraka sana kuboresha masuala mazima ya mafao. Ameendelea kuwa msikivu katika maeneo yote ya utumishi, wanaamini ataendelea kuboresha zaidi kwa jinsi ambavyo mifuko itaendelea kuboreka na kuhifadhi katika mitaji ambayo ina tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na maboresho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, katika Muswada huu maboresho ni mengi. Wenzangu wametaja vifungu mbalimbali, lakini mimi nasema kifungu Na. 18 kwenye hii Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Sura Na. 371.

Mheshimiwa Spika, sheria hii sasa hivi tumeona inaenda kurekebisha na kuweka bayana Afisa atakayewajibika kisheria, atakayehusika kuwasilisha michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya

Jamii hasa kwa wale watumishi ambao malipo yao hayalipwi na Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha. Kumekuwa na changamoto kote nchini, kwa wale watumishi ambao mafao yao yanapelekwa na taasisi husika au na ofisi husika.

Mheshimiwa Spika, sasa sheria imeletwa vizuri, imebainisha wazi, Afisa atakayewajibika kisheria kupeleka hii michango kwenye mifuko yetu. Naipongeza sana Serikali, ni kilio cha muda mrefu. Sasa kuna mtu atawajibika, afisa maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, katika kifungu cha 45 cha sheria hii, wamezungumza wenzangu, nami kidogo naongelea hapo hapo kuhusu suala zima la watumishi wenzetu ambao katika namna moja au nyingine wamekutwa na adha ya kuingia Magerezani. Tunaona sasa sheria imekuja ambapo akiwa kule gerezani atakuwa na uwezo wa kusaini na kutoa ridhaa kwa mnufaika mwingine achukue mafao yake. Hii ndiyo sera ya hifadhi ya jamii na hii ndiyo Katiba ya nchi inayoitaka Serikali itunze hifadhi ya jamii ya Watanzania, ndiyo nia thabiti.

Mheshimiwa Spika, hapa inaonekana wazi kwamba sasa Serikali inaendelea kusimamia sera yake ya Hifadhi ya Jamii, kusimamia Katiba ya nchi ili kutunza au kuhifadhi jamii ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye marekebisho ya sheria ya fidia kwa wafanyakazi, wamezungumza wenzangu, lakini kikubwa sana, lazima niseme kwa sababu mimi nakwenda kule nakutana nao, watu wengi walikuwa wanalalamikia sana malipo ya fidia ya matatizo yanayotokea kazini, kwa maana ya Mfuko huu wa Fidia kwa wafanyakazi. Suala zima la ukomo lilikuwa tatizo kubwa sana na muda, wengine maskini wa Mungu hata hawajui hizo taratibu na kweli wameumia kazini, anakwenda anakutana na sharti la muda. Ni kilio kikubwa cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine wanapata ajali hawapati fahamu hata mwaka mzima, akizinduka yuko nje ya muda, lakini jinsi ambavyo Serikali ya Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwajali watumishi wa Tanzania, imeona umuhimu

wa kuleta sheria hapa. Kwa kweli naipongeza sana Serikali. Naamini watumishi wamefurahi sana na nikienda nitazungumza nao tena. Jambo hili naipongeza Serikali kuwajali kwa kiwango cha hali ya juu watumishi na wale wanaoenda kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura Na. 50, naipongeza sana Serikali kwani kifungu Na. 14 wamesema wenzangu na wamepongeza kuhusu mapunguzo ya tozo. Nakubaliana nao, pia naamini Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo muda wote imekuwa ikisikiliza na kutenda kutokana na jinsi ya uwezo wa mfuko wake na jinsi ya wakati na mambo yanavyoruhusu, ninaamini katika suala zima ambalo limezungumziwa katika kifungu cha 33, kuzungumzia kuongeza mafao kutoka miezi 33 hadi 36 ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, naamini tutaendelea kuishauri Serikali kupitia wafanyakazi wenzangu, watumishi wa Tanzania, kwamba baadaye jinsi ambapo mifuko itaendelea kuwekeza kwa tija, kama ambavyo Mheshimiwa Rais tumemsikia akizungumza, jamani mifuko ikawekeze kwa tija sasa, tukajiongeze.

Mheshimiwa Spika, pia tunaamini itafikia wakati miezi 33 itakuwa zaidi ya hiyo kwa sababu kiuhalisia watumishi wanazungumza kwamba miezi 36 kwa mtu kupata mafao yake ni michache na ukizingatia Marehemu hataendelea kupata ile *pension* kila mwezi. Kwa hiyo, nasema kwa niaba ya watumishi kwamba tunaamini Serikali ya Mama yetu Samia ni sikivu sana na jinsi ambavyo itaendelea kuboresha mifuko hii na kuwa yenye tija lazima hapo baadaye itaendelea kuboresha eneo la Kifungu cha 33.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Kifungu cha 52. Nazungumza kwa niaba ya wafanyakazi kwamba, tunaipongeza Serikali, tunaamini mafao haya, pesa hizi ni kama dhamana pia ndiyo maana imekuja na sheria nzuri sana. Kwanza mtumishi anaweza akakopea kwa maana ya kuweka dhamana kwa masuala yanayohusu mambo ya nyumba na makazi.

Mheshimiwa Spika, wanazungumza hii ni dhamana, wakati mwingine mtumishi anapata changamoto kubwa sana ambayo anaamini kimfaacho mtu chake, anaamini anayo kidogo hifadhi mahali, pengine nyumba tayari anayo, lakini amepata tatizo kubwa la ugonjwa yamkini ambalo pengine imeshauriwa aende mbali zaidi. Kwa hiyo, tunaamini Serikali ya Mama Samia ni sikivu sana, itakuja kupanua huu uwanda wa dhamana ya hii hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache napongeza sana Muswada huu, naipongeza sana Serikali, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza hususan Mjomba wangu, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Ridhiwani Kikwete na rafiki yangu Wakili Msomi, Patrobas Katambi. Nawapongeza sana Mawaziri hawa kwa maboresho ambayo wamekuja kuyaleta kwenye Sura ile ya 50 ya Mfuko wetu wa Hifadhi ya Jamii. Ukitizama maboresho yale kifungu cha 11(a) wameleta mapendekezo ya watu wanaotoka kwenye sekta binafsi kujiunga kwenye Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, ukisoma sheria ile, imemtaka huyu mwanachama ambaye anachangia, achangie ndani ya miezi sita. Sasa 99% ya watu wangu ni wakulima wa korosho. Wakulima hawa wanategemea mazao ya msimu na wenyewe wanatamani kujiunga na mfuko.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwa sababu ipo *room* ya Mheshimiwa Waziri kutunga kanuni, uende sasa kuwajumuisha

wanachama hawa wapya ambao tunaweza kwenda kuwashawishi walipe kwa wakati mmoja badala ya kuchangia ile miezi sita. Hawa wana uwezo na ni wakulima wengi wa Taifa hili ambao wanategemea mapato yao kutoka msimu mmoja, lakini ukiwaambia wachangie miezi sita; kila mwezi wachangie wanaweza wakashindwa kuchangia. Kwa hiyo, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri wakati umepewa *room* hiyo ya kanuni, basi hawa wakulima wa korosho na wengine waweze kuchangia *in lumpsum* ili waweze kupata mafao kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo ukisoma kifungu cha 15 kimempa *DG* uwezo wa kulipa mafao pale tu inapothibitika kwamba mwanachama amechangia ila mwajiri amechelewa kupeleka michango ile kwa wakati. Sasa wakati *NSSF* wanafanya haya, tunao Mfuko mwingine ambao wenyewe sasa waajiriwa wanaotoka Serikalini wanachangia.

Mheshimiwa Spika, natamani sana kifungu hiki ambacho kimebadilishwa, mtazame mnavyoona mnaweza kufanya na watu wa *PSSSF* na wenyewe sasa itakapojiridhisha kwamba mwajiriwa ameshachangia, amekatwa fedha zake, lakini mwajiri amechelewa kupeleka kwenye Mfuko wa *PSSSF* na wenyewe walipwe mafao yao halafu wao wa-*deal* na mwajiri. Itasaidia sana kuondoa *double standard* kwenye mifuko yetu hii.

Mheshimiwa Spika, kipo kifungu cha 52 na 76 kinachoruhusu mwanachama ambaye hajafikisha umri wa kupata mkopo wa dhamana ya nyumba. Hii ni fursa sasa kwa vijana wengi ambao wameweza kuajiriwa kwenda kujiunga na *NSSF* ambayo imetoa *room* hiyo ya vijana ambao ndoto zao kubwa ni kuwa na majumba mazuri, kuwa na magari, siyo nyumba tu hata magari kama michango yake itatosha, basi aweze kupewa na mkopo wa nyumba, hata gari kutokana na dhamana yake.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kwenye *WCF* ambako wamefanya maboresho kwa watu waliopata ajali kupewa fursa *DG* na Bodi kuona namna gani watu hawa wanaweza kufidiwa. Mimi ni mhanga kwenye hili, nilipata ajali nikashindwa kutoa taarifa ndani ya miezi 12 ya kisheria. Baada ya miezi mitatu,

baada ya kumaliza miezi 12 nilipowaendea wakaniambia uko nje ya muda.

Mheshimiwa Spika, sasa ajali ni kitu ambacho kiko *documented,* ukienda hospitali kuna taarifa, ofisi kama ya Spika inakuwa na taarifa, Mbunge akipata tatizo kubwa, ukienda kwenye Mfuko kwa sheria ya zamani ilikuwa huwezi kupata stahiki zako, kwa sababu umepeleka taarifa nje ya muda. Sasa hivi wamekuja kubadilisha sheria wameenda vizuri kwamba *DG* ana uwezo baada ya kujiridhisha na taarifa zako kwamba anaweza kulipa.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kwa uwezo huu ambao tunakuja kuitunga sheria kama itafaa, kwa wale waliopata ajali na taarifa zao zinajulikana vizuri, basi wafidiwe na mfuko.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo tu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ni mfupi sana. Kilichonisukuma nichangie ni wakati ambapo tulikuwa tunajadili dira ya mwaka 2050, huko kwetu Mkoani Mara, wachangiaji wengi, watu wa kawaida wanatoa mawazo, wanasema na wao wawekwe kwenye *pension.*

Mheshimiwa Spika, sasa tukaanza kujadili, wataingiaje? Kwa hiyo, nimeona kwamba kwanza naunga mkono marekebisho yote haya yanayokuja kuboresha. Isipokuwa mimi labda niongelee ya huko mbeleni na tumwombee kijani wetu Ridhiwani Kikwete awepo miaka 30 - 40 kwenye hii Wizara azidi kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza kabisa ni watu binafsi wameeleza na sehemu nyingine duniani watu binafsi wapo, lakini kwa bahati nzuri labda wenzetu wameendelea sana. Hii *pension* matatizo tunayoyapata hapa wanaofuatilia sana Ujerumani

yamewakumba, Ufaransa yamewakumba, *pension schemes* na fedha zake zinakuwa zina matatizo.

Mheshimiwa Spika, ninachopendekeza kwa siku za usoni ni kwamba tuwe na *pension schemes* nyingi ambazo zinaweza kumchukua mkulima, mfugaji na mvuvi akawa na *scheme* yake, hii ya kuweka wote pamoja ni nzuri, lakini tunavyozidi kwenda lazima wakulima, wavuvi, wafugaji wapate *scheme* yao. Nchi nyingine wana *schemes* zaidi hata ya 2,000 hadi 3,000 kwenye *pension* zao, siyo mbili au tatu. Kwa hiyo, hilo ni pendekezo langu la siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tena ambalo ningependa kuongelea na wewe mwenyewe, nadhani sijui wale walikuwa ni waalimu wako wale wa *law* na wengine walikuwa wametutangulia, hata mimi wangeweza kunifundisha. Nikiongea nao *pension* zao zinasikitisha kweli. Wapo Maprofesa ambao hawavuki shilingi milioni moja na wengine wamekaa mle muda mrefu. Kwa hiyo, inamaanisha kwamba haya maboresho tunayoyafanya, bado yanahitaji marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwa sababu huyu mtu amechangia mafao yake, na hiyo *investment* yake iko *revolving,* kama kuna mtu ameenda amechukua fedha, amekopa akafanyia biashara, lakini huyu aliyechangia haiwezekani anachopokea kila mwezi kwa miaka atakayokuwa bado anaishi kiko hapo hapo. Nadhani hapo tunahitaji kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano ni kwamba kama mtu anastaafu *pension* yake wamempigia hesabu labda ni shilingi 1,100,000, basi kwa miaka yake ya uhai anabaki huko kwenye shilingi 1,100,000, lakini tunajua kwamba shilingi inapoteza nguvu, na inapata nguvu. Kwa hiyo, hii *pension* nilikuwa nadhani iendane na wakati. Maboresho yote tunayoyafanya yaendane na (labda sijui wataalam wa Kiswahili lakini nilimsikia *CEO* wa *CRDB* anajua sana Kiswahili; *living wage* ni nini) *living wage,* si ndiyo! Mzee unaandika vitabu hapa, *living wage* ni nini?

Mheshimiwa Spika, yaani iendane na hali halisi, kwamba ikiwa wengine; siyo vizuri kutolea mfano haujafikia umri wa kustaafu, lakini utakapofikia nadhani utachukua *percent* fulani ya Spika atakayekuwepo wa wakati huo, nadhani ndiyo mpangilio, sasa na *pension,* nayo tuiangalie hivyo. Maana yake huyu mtu ametoa fedha zake wamechukua, wamekopa, wameweka kwenye uzalishaji, fedha imerudi, halafu wamerudi tena wamekopa. Kwa hiyo ile anayopokea kama mafao, haiwezi kuwa imeganda pale pale. Haiwezi kuwa *static. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine cha mwisho ambacho sijui tutaenda huko, mimi nakumbuka huko sehemu nilikokuwa nafanya kazi niliulizwa, Profesa hivi ukitaka *pension* yako tuifanyeje? Nikamwambia mnieleze sasa. Ikaonekana kuna vipengele ambavyo pesa yako ikichukuliwa faida ya yule aliyeichukua, ile *interest rate* wakati anairudisha na wewe unapata kidogo. Hilo nalo ni pendekezo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo hilo la kusema, kama fedha za watu waliostaafu zinakopwa zinafanyiwa kazi, kwa hiyo, kile wanachopata, ile faida, yule aliyezikopa na anayemkopesha, basi ampatie na huyu mwenye fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni huo, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtoa hoja, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Hifadhi ya Jamii Mwaka 2024 *[Social Security Laws (Amendments) Act, 2024]*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza, nami naomba radhi kidogo mbele ya Bunge lako kwa kuchanganya madesa hapa,

kwa kumpa nafasi Mheshimiwa Almas Maige ambayo hakuwa nayo wala hakustahili. Namwomba radhi sana Mheshimiwa Riziki Lulida, pia naliomba radhi Bunge lako maana Mheshimiwa Almasi Maige huyu nimekutana naye kabla sijaanza kuhutubia hapa, nahisi kuna jambo la Kinyamwezi kalifanya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Maige namtambua kama Mjumbe na nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni ya Mheshimiwa Riziki Lulida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchana wa leo, jumla ya Wajumbe saba kwa maana ya Wabunge wamepata nafasi ya kuchangia, bahati mbaya sikupata michango ya maandishi, lakini waliochangia wote nimewasikia. Yapo baadhi ya maeneo ambayo wametoa maoni yao, pia yapo baadhi ya maeneo wametuelekeza nini cha kufanya. Nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru sana kwa kuunga mkono hoja ambayo tumeileta hapa leo.

Mheshimiwa Spika, nataka kwa kipekee kabisa niwashukuru sana Wabunge kwa michango yao mizuri. Kwa niaba ya Wizara na kwa niaba ya Serikali nakiri tumepokea maoni yao mazuri ambayo yanalenga kuboresha Muswada wetu pia kuweka sheria zikae vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la sheria hii tuliyoileta Mezani kwako ambayo ina lengo la kuboresha, kurekebisha na kuweka umadhubuti sheria ya kusimamia Mifuko ya Hifadhi, imegusa jamii yetu na hivyo jamii kupitia Bunge lako imeendelea kutetewa na kusimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja, nataka nieleze katika maeneo machache. Kwanza nataka nianze katika ushauri wa mwisho ambao umetolewa na Mheshimiwa Prof. Muhongo. Kwa kweli ushauri wake ni mzuri hasa katika eneo hili la kwamba kwa kuwa wanachama hawa wanachangia Mifuko na sisi tunakwenda kutumia fedha hizo kwa ajili ya uwekezaji na shughuli nyingine, ni vyema tukaangalia katika mazingira hayo ili wanufaika nao wale wanachama waendelee kunufaika.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue hili jambo, tutakwenda kuliangalia pamoja na wenzangu na kulifanyia *valuation* nzuri ili tutakapoleta jambo hapa mbele ya Bunge lako, basi liwe jambo ambalo limeandaliwa vizuri na siyo jambo ambalo litakwenda kutikisa mifuko yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba pensheni hizi zinaangaliwa thamani yake kwa ustahimilivu wa uwezo wa pensheni hizo kulipika. Hapa nakusudia kuzungumzia *actuarial evaluation* ambazo zinafanyika mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba haya tunakwenda kuyaangalia mara kwa mara kuweza kujua ustahimilivu wa Mifuko yetu na uwezo wa kuweza kulipa hayo yote ambayo ameyasema, hasa hapa nakusudia sana alipozungumzia jambo ambalo hata mimi mwenyewe linanigusa kwa sababu wako baadhi ya watu walionifundisha Chuo Kikuu na pensheni zao, kwa kweli ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ndiyo athari za sheria na sisi tuliopo ambao tumepewa majukumu haya, kazi yetu ni kuangalia na kwa sababu tunatambua michango yao, basi nadhani tunalo jukumu la kuangalia ili tuweze kuwasaidia walimu wetu waliotufanya leo hii napata hata nguvu ya kusimama mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kutumia nafasi hii pia kuwatoa wasiwasi. Nimesikia michango ya Wajumbe wako na hasa katika eneo hili, nataka nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Getere ambaye amezungumzia sana jambo lile linalohusu wale Watendaji Kata ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa hawafurahii sana pensheni zao wanazolipwa. Nataka nimkumbushe na nimrudishe katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, tatizo lile ulilonalo wewe na mimi ninalo hapa la sheria hizi kuzitaja kwa Kiswahili wakati ziko kwa

Kiingereza. Hata hivyo, hapa nakusudia kuizungumzia Sheria ya *PSSSF section* ya 20 inatoa Mamlaka kwa Mkurugenzi Mkuu pale ambapo ataridhika kwa ushahidi kwamba huyu Mtumishi wa Umma amefanya kazi na mishahara yake ilikuwa inakatwa hizo pensheni zake kupelekwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, basi kama ikithibitika kwamba hilo jambo limefanyika, Mtumishi huyu atakuwa katika nafasi ya kulipwa pensheni zake.

Mheshimiwa Spika, tumeeleza katika sheria kwamba sasa hivi katika sheria tunachokihitaji ni ushahidi kwamba huyu mtu alikuwa anafanya kazi na alikuwa anapata makato. Kama huyu anayetakiwa kulipa alikuwa halipi, hilo linakuwa ni kesi baina yake na taasisi husika na siyo kwa yule mwanachama au mwananchi wetu ambaye amehudumia nchi yake kwa jasho kubwa, wakati mwingine kuvuja damu halafu mwisho wa siku anakuja kukosa ile thamani ya jasho ambalo amevuja kwa ajili ya nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, Serikali kupitia sheria tuliyoiweka leo hapa, imeeleza wazi kwamba maisha ya mwanachama wetu ni msingi mkubwa wa mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niwahakikishie Wajumbe wengine wakiwemo Mheshimiwa Ali King ambaye alizungumza kwa sauti kubwa sana, akieleza wasiwasi wake juu ya kanuni ambazo zitatengenezwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ali King, mimi ni Mbunge, pia kama alivyo yeye, mimi naongoza watu, pia ninao wazee, ninao vijana lakini pia ninao watarajiwa na mimi mwenyewe pia ni sehemu ya watarajiwa wa pensheni hizo.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwenda kutengeneza sheria ambayo itakwenda kuvunja na kufinya haki za watu. Tutatengeneza sheria ambayo inakwenda kuangalia maslahi mapana ya watu, lakini sheria ambayo inakwenda kuangalia maslahi makubwa ya wale ambao wanavuja jasho kwa ajili ya mama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ambayo tumeleta mbele yako inathibitisha kwa lugha nyingine kwamba inakwenda kusimamia haki za watu. Tumeeleza kupitia sheria kwamba sheria hii moja ya jambo kubwa ambalo tunaenda kuongeza ni kwanza, muda wa wanachama kulipwa. Kwa mfano, wameeleza Wajumbe wengi na mimi nataka niweke nukta katika jambo hilo, lakini pia kuliwekea msisitizo kwamba kama alivyozungumza Mheshimiwa Katani kwamba sheria hii sasa hivi inafungua wigo siyo tena kubanwa kwamba ndani ya miezi 12 lazima ulete taarifa ili uweze kulipwa na *WCF*.

Mheshimiwa Spika, tunatambua katika changamoto za utendaji kazi, ziko baadhi ya mazingira ambayo yanamfanya huyu Mtumishi wa Umma anayehudumia umma wake kushindwa kupeleka taarifa mapema. Kwa mfano, kwa wenzetu ambao wanafanya huduma ya ulinzi wakati mwingine anaweza akavamiwa, akapigwa akaumia vibaya. Huduma yake kuhudumiwa inaweza ikachukua zaidi ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, pia wako wengine ambao wanafariki. Jeshi la Polisi linaweza likaamua kwamba wale ambao wamefanya ujambazi huo na kuua wakamatwe. Sasa hatuwezi kusubiri wajane na wanufaika wasubiri kesi ile ambayo inaunguruma zaidi ya miaka minne iishe ndiyo wao wafaidi kwa jasho la mzazi wao au kwa jasho la mlezi wao. Sheria hii kwa kutambua mchango wa mtu huyu, inakwenda kutoa *lee way* ya kuhakikisha kwamba yule mtumishi aliyeumia akiwa kazini anaenda kuangaliwa na kufaidi matunda hayo hayo ya utumishi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niendelee kuwatoa wasiwasi. Sheria hii pia inakwenda kuondoa baadhi ya watumishi ambao kwa namna moja au nyingine wangeweza kugongana kimaslahi na utekelezaji wa Sheria hii. Kwa mfano, yako baadhi ya mambo ambayo yanatokea kwa mfano katika maeneo ya kazi, unahitaji mtu wa *OSHA* yeye aje kufanya *assessment* lakini mtu akiumia hapo hapo wanataka taarifa ya *OSHA* pia ije kumsadia yule mwajiriwa. S

Mheshimiwa Spika, sheria hii imeondoa watu hao, sasa inaeleza juu ya nani ambaye anatakiwa kwenda kusimamia juu ya kuhakikisha kwamba mtu huyu anapata haki. Pia, kuhakikisha kwamba siyo haki tu inapatikana lakini haki hiyo ionekane ikitokea.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaenda kuheshimu pia Mamlaka ya vyombo vingine. Wajumbe wako wa Kamati walizungumza juu ya kuhakikisha kwamba majeshi kama Polisi siyo linaingia moja kwa moja katika utekelezaji wa jambo hili, lakini pia liingie kupitia utaratibu mwingine. Bahati nzuri nchi yetu katika kuhakikisha kwamba hiyo haki inatokea, imeweka pia chombo kama Mahakama ambacho kama mtu atahitaji msaada wa Mahakama ili aweze kuwatumia Jeshi la Polisi, basi atapata *Order* ya Mahakama ili aweze kwenda kufanya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tumekubaliana na hilo kwa sababu tunatambua kwamba moja ya msingi mkubwa wa Serikali hii ya Awamu ya Sita ni kuheshimu utawala wa kisheria na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan analifanya hili kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaelekeza kuhakikisha kwamba haki ya wananchi au wanachama inapatikana hasa kwa wale ambao wamepata kazi au wana ajira zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, wako watu ambao wanafanya kazi zaidi ya moja. Unakuta mtu anafanya kazi labda Hospitali ya Aga Khan au akitoka hapo anakwenda kufanya kazi Hospitali ya Benjamini Mkapa. Sasa katika mazingira haya tumempa nafasi huyu mwanachama aweze kuchagua mchango upi uende? Kama akitaka yote ili uonekane mchango ni mkubwa uweze kutafsirika katika pensheni yake, nayo pia tumempa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inampa nafasi ya mwananchi kuweza kupata fungu analolitaka. Kwa maana nyingine maana yake hata kama akihama nalo pia sheria hii inamtaka yule mwajiri wa kwanza aweze kutunza zile taarifa zake na kule anapohamia

taarifa ziende ili kuhakikisha mwanachama huyu hapotezi kumbukumbu za michango yake katika Mifuko yetu ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niwahakikishie kwamba Serikali yenu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imejizatiti kuhakikisha kwamba wanachama ninyi mnapewa kile ambacho mnastahili. Sheria inawataka wanachama wapewe michango yao ndani ya muda uliotajwa lakini pia michango hiyo iendane na ile haki yao inayotaka.

Mheshimiwa Spika, ya kusema yako mengi, lakini nataka nirudie tena kukushukuru wewe kwa kutupa nafasi ya kuleta hoja yetu hapa. Pia kwa ujumla nieleze tena maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili na ni jambo endelevu. Ndiyo maana mara kwa mara Serikali yenu imekuwa inaleta Miswada hii ili kuifanyia marekebisho, kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendelee na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba kutoa hoja, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 (*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024*)**

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 12 kina marekebisho ya Serikali. "*If upon approval by the Minister.*" Mheshimiwa Waziri, haya marekebisho yana nia njema, lakini hili jambo ambalo mnataka kumpa kazi Waziri, mbona siyo jambo kubwa sana? Yaani Bodi haiwezi kumalizana na ile *additional assessment*? Yaani, kwa nini mnampelekea Waziri? Maana Muswada mwanzoni mlileta ili Bodi ifanye? Kwa nini sasa hivi mmeamua kupeleka kwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulivyopeleka mara ya kwanza mbele ya Kamati tulikuwa na andis kwamba jambo hili likamalizwe na Bodi. Kamati kwa kuangalia *sensitivity* ya jambo lenyewe wakasema kuwaachia wao wenyewe peke yao wakaliamua bila Waziri kujua na wakati Waziri ndio msimamizi wa Sekta, *then* inaweza ikasumbua. Kwa hiyo, wakaona tulipeleke jambo hili kwa Waziri, na sisi kwa sababu nia njema ni kufanya kazi za umma, tukaona hatuna shida nalo. Ndiyo maana tumelileta kwako katika mabadiliko haya ambayo tunayapendekeza.

**MWENYEKITI:** Haya kama ni Kamati ilisema hivyo, basi liende hivyo lakini siyo jambo kubwa kubwa kwa kweli kwa sababu unazungumzia ile riba ambayo ni aidha ifutwe ama isifutwe. Sasa hutarajii kwamba watakuwa wanachelewa. Sasa sijui kuna Kampuni moja mkandarasi kachelewa mpaka iende kwa Waziri ndiyo ije ibadilishwe, yaani ndiyo wasamehewe! Siyo jambo kubwa sana, lakini madamu limeamuliwa na Kamati, twende nalo haya.

Lingine hili ni la Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hii lugha, "*if it thinks fit,*" sheria huwa haina mambo andi-*think*. Kwa hiyo, kile Kitengo chako cha andishiw a Sheria, hii siyo lugha ya kisheria. Uzuri hapa imeshatoka kwa kuingiza haya maneno ya Waziri, lakini litazamwe hili jambo mtakapokuwa mmeanza utekelezaji muone yale maombi yanakuja kwa wingi kiasi gani na kwa ukubwa upi ili kuipa Bodi mamlaka ya kufanya hivyo badala ya kusubiri Waziri afanye.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 13

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 13, kinahusu *treating unlimited contributions and as remitted.* Hili ni jambo ambalo kwa kweli ni zuri sana lakini hapa limeandikwa kwamba *where the Director General is satisfied that an employee's contribution has been deducted from his wage*. Kama haikuwa *deducted,* hili ni tatizo la mwajiriwa kweli! Si ni la mwajiri! Sasa huyu kujiridhisha kwamba mwajiri alikata, haya kwa mfano amejiridhisha mwajiri hakukata, huyu mtu hatolipwa pensheni? Ndiyo kifungu hiki kitamaanisha hivyo? Kwamba michango yake yaani mwajiri hajawahi kupeleka na huyu kajiridhisha kwamba siyo tu hakupeleka, hata kumkata mfanyakazi hakumkata. Je, ni tatizo la mwajiriwa?

Sasa hii sehemu ya kwanza tunamsaidiaje huyu? Kwa sababu nia ya hiki kifungu ni kutibu lile jambo ambalo lilijitokeza kwa ukubwa sana hapa Bungeni mpaka tukaelekeza Kamati ikafuatilie, ambalo Serikali kwa kweli imefanya jambo zuri la busara na kubwa sana. Ukishamwekea huyu tena mwajiriwa, hili jukumu kuna shida hapo.

Ehe, tusaidiane jamani, maana hili linakuja kutibu ile changamoto iliyojitokeza sana kwa wapigakura kwamba wanachanga wao michango ili waweze kulipwa; lakini tuko kwenye *NSSF* sasa hivi, hatujafika bado kwenye *PSSSF*. Ni mimi peke yangu ndiyo nasoma hii au wote tunaiona? Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo hiyo hiyo kwamba ajiridhishe? Ajiridhishe kwamba mwajiri alikata halafu hakupeleka? Sasa kama hakukata ni shida ya nani? Si ni shida ya mwajiri bado?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa mimi mwajiriwa naingiaje hapa? Kwa sababu tunasema ili aweze kulipa lazima ajihakikishie kwamba mwajiri alikata, lakini hakupeleka. Hata kama hakukata, si bado ni kosa la mwajiri! Hebu tusaidiane.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, *spirit* ya *provision* hii ni sahihi kwamba waajiri wana wajibu wa kisheria ambao ni *statutory obligations* kulipa michango ya mwanachama na inapofika wakati wa kulipa mshahara, maana yake ni kwamba ataandaa *payroll*. Kwenye ile *payroll* moja ya *deductions* kutakuwa kuna *Pay As You Earn* ile fedha ya kodi, lakini pia kutakuwa na kipengele cha kulipa hii kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mazingira ambayo yanatokea kwamba mwajiri sio tu kwamba hajapeleka michango, hata mishahara halipi. Kwa hiyo, mshahara kwenye *circumstance* ambayo hakuna mshahara, kwa hiyo hata *evidence* ya *payroll* ya mwezi huo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kinachofanyika ni pale ambapo kuna waajiri ambao unakuta mishahara yao hawalipi, labda hawajalipwa miezi sita. *Issue* hapa inakusa sasa ina-*originate* kama *issue* ya kikazi, lakini zaidi kupitia Kamishna wa Kazi na Utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, kwa hiyo, inakua ni kesi ambayo inaweza ikaenda pia *CMA* na *legal course* zikachakuliwa kabisa kwa *procedure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa ilikuwa tu ni mazingira, siyo kwamba yule ambaye mwajiri atakua haja-*deduct* kwamba bado atakuwa amekwepa. Bado kisheria atakua na wajibu wa kuweza kudaiwa fedha hiyo, lakini kwa *context* ya jinsi ilivyokuwa *crafted* na hii *drafting,* nadhani tunahitaji tu ku-*fine tune* ili iweze kuleta *context* ya kile kilichokusudiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna *rewording* kidogo inabidi tufanye.

**MWENYEKITI:** Maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kweli ndivyo kifungu kinavyosema hapa, lakini nia ya kifungu cha mwanzo kabisa ni kuhakikisha huyu mtumishi au mwajiriwa hapati athari kwa makosa ya mwajiri.

Nimekusikiliza hapa ukasema pengine hakuna hata mshahara, sasa hili la mshahara sidhani kama mfanyakazi ataweza kulivumilia kiaso hicho. Kwa hiyo, lazima litakuwa limeshaeleweka huku. Ila nawaza, mimi kama nimeambiwa mshahara wangu shilingi 300,000 na ninalipwa shilingi 300,000, sheria inamtaka mwajiri ndiye anikate, naye hajakata. Umefika muda, nimefika zangu miaka 60, nataka nilipwe. Naambiwa kwamba huyu mtu wako bwana hakuwahi kukukata mshahara na kifungu hiki namna kilivyo kwa kweli wewe haumo. Sasa mimi nakuwa nimelindwa vipi na kifungu hiki?

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kwa ngazi hii kwa sababu nia ya Serikali ilikuwa ni hiyo ya kwamba huyo ambaye mishahara yake imelipwa na kukatwa amekatwa, kwa maana ya kwamba amelipwa pungufu ndiye awepo hapa. Nafikiri tuwapatie muda ili wakalifanyie kazi na hili. Kwa nini? Kwa sababu ni muhimu sana. Kazi ya mwajiriwa ni kutoa huduma yake ile aliyoajiriwa siyo haya mambo mengine.

Wewe hukukata *Pay As You Earn,* mimi nahusikaje? Wewe hukukata hizo za *NSSF,* mimi nahusikaje? Kwa sababu kisheria ni wewe, lakini kwa mazingira haya tukisema tuibadilishie hapa, kwa sababu kuna hoja hapa nyingine zitakuja za mahesabu na nini. Kwa hiyo, mwende nayo hii kwa nia ile ile mkaitafakari, mje na mabadiliko. Kwa nini? Kwa sababu nia ni kumlinda mfanyakazi, na yeye hausiki popote kujikata yeye haya mambo kwa sababu fedha zinatoka kwa mwajiri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama mwajiri hakulipa mshahara, hilo sisi tusiende lakini kwamba mwajiri hakukata ilhali anamjua kabisa huyu ni mwajiriwa wake, hili ni shughuli yake, na huko maofisini watu wanalipwa mishahara. Si kuna watu wanaitwa sijui *Labour Inspectors,* sijui kitu gani! Si ndizo shughuli zao hizi jamani! Kwa hiyo, huyu mwajiriwa tumwondoe kabisa kwenye hili jukumu, ila mkalifanyie kazi.

Hili lipo kwenye upande wa *NSSF*. Upande wa *PSSSF* hiki kifungu kule hakipo Katika utungaji wa sheria, kwa sababu hawa wote mwishoni ni wastaafu, hakuna cha binafsi wala huku

kwingine. Kwa hiyo, inabidi katika utungaji lazima wawe sio sawa kwa maana ya kiasi wanacholipwa, lakini sawa kwa maana ya yale mazingira yao yasiwe tofauti kwa maana ya sheria. Nimeeleweka?

Mtakapoenda kukifanyia kazi ili kule tusilazimike kukijadili tena, mtakifanyia kazi upande huu na upande ule mwingine. Sasa ili tumalize hapa kabisa haya maneno, kuna kifungu kipo upande ule, ama tutakapokifikia ili tusichanganye mambo. Kwa hiyo, hiki cha 15, Bunge leo litakipitisha hivi kilivyo, lakini kwa sababu ya ile nia ya kumlinda mwajiriwa, mwende mkakifanyie kazi ili mtakapokuwa mmeshafanya na hesabu na mpo tayari, tuleteeni marekebisho ili kwa kweli mwajiriwa alindwe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, naona umesimama.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniruhusu kabla hatujaondoka kwenye hiki kifungu, nilikuwa nataka tu Mwanasheria Mkuu atusaidie hasa *drafters*. Naona matumizi ya *his* yanaendelea, sasa ni *generic,* tutumieje? Maana hapa inaonekana sisi wengine haituhusu. Maana yake ni *his, his wage, his employer* tunafanyaje? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ipo wapo hiyo? Mbona imenipita. Ipo sehemu gani Mheshimiwa?

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, ni kwenye hii kifungu cha 15, kwa mfano inaongelea *employer from his wage, his employer, is he, he, he, he,* kwa kweli hiyo…*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa, hiyo acha nimsaidie. Ile Sheria ya Tafsiri ya Sheria ikisema *he* inasema pia *she*, lakini hoja yako imeeleweka kwa maana ya kwamba, inabidi tuitazame ile sheria inayohusu tafsiri inayosema kwamba *he includes she*. Ile ndiyo inabidi tuirekebishe ili hapa pia tuweze kurekebisha isije ikaonekana kuna watu tena wanaanza na mambo mengine. Ngoja tusiende huko yasije yakaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, lakini hoja ya Mheshimiwa Mbunge imeeleweka, inabidi tuitazame ile sheria inayohusu tafsiri. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 17 haya ni mambo ya *drafting* Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *subject to the provision of these act retirement pension shall be payable to a member*. Hii "*who*" kwa sababu imejitokeza kwenye vifungu vyote, "*who*" inasimama pale juu halafu maneno mengine yote yanafuata. Yaani "*who*" inakuwa hairudiwi kwenye kila kifungu, ndiyo uandishi wa sheria. Sijui umenipata? Kwa hiyo, hii mtaifanyia hayo marekebisho ya kuondoa hizi "*who*" zilizotawanyika kwenye kifungu.

Waheshimiwa Wabunge, hili ni jambo la kiuandishi wa sheria. Kwa hiyo, watafanya marekebisho. Kifungu cha 23 kinaafikiwa?

Samahani ni Kifungu cha 23 kwenye Sheria, na ni kifungu cha 17 kwenye Muswada.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila madadiliko yoyote)*

Kifungu cha 28

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 28 kina marekebisho ya Serikali ambapo wamekifuta hiki kifungu.

Waheshimiwa Wabunge, wamekifuta kabisa Kifungu cha 28, kwa hivyo kinaondolewa. Tunaafiki kuondolewa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Madadiliko yoyote)*

Kifungu cha 35

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 35 kinahusu mabadiliko ya *one-year* kwa ajili ya Makamu Mwenyekiti wa Bodi. Sasa mmesema

itoke kwenye *one-year* iende *three years*. Mmebadilisha tu *three years*, ile *re-election?* Yaani, atakuwa na *three years* na *re-election* ama ni *three years* akimaliza basi? Kwa sababu mwanzoni ilikuwa ina *re-election* kwa sababu anapewa mwaka mmoja. Sasa tunakusudia kusema miaka mitatu *re-election* iendelee?

Haya, Mwenyekiti anaruhusiwa mara mbili, siyo! Mwenyekiti anaruhusiwa? Naam.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara mbili.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, na huyo mara mbili? Haya, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila madadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 43 pamoja na marekebisho ya Serikali. Hiki ni kimojawapo cha kwenda kutazama utekelezaji. Hapana hiki siyo cha *drafting,* hiki ni cha utekelezaji wa lile jukumu lililotolewa bodi kuelekea kutaka *approval* ya Waziri.

Haya ahsante. Tuendelee, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila madadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 52 *restoration of funding position of the fund* kipo huku kwenye nini?

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, kwenye *NSSF*.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza. Hii siyo *NSSF,* tumeshaingia *part three* ambayo inahusu *PSSSF*. Hakipo kwenye *NSSF,* hiki kinachohusu *restoration of funding position of the fund,* kule kwenye *NSSF* hakipo. Kwa hiyo, mtatazama *gist* ya hiki kifungu ili muone na kule kikae namna gani kwa sababu hiki kilichoandikwa hapa ni muhimu na wao wafanye, si ndiyo?

Kwa hiyo, mtatazama pamoja na yale mengine ambayo tumeyazungumza. Hili litasaidia kwenye lile ulilokuwa unasema Mheshimiwa Waziri wakati ukihitimisha hoja hapa kuhusu hoja aliyoisema Mheshimiwa Profesa Muhongo ya mafao kutokusimama sehemu moja wakati mifuko inaendelea na uwekezaji, kukopesha na kupata faida, ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 62

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 62, marekebisho ya Serikali mmeondoa neno "*may*" mmeweka "*shall.*" Sasa, hoja ni kwamba kwenye ile sheria yetu ya tafsiri neno "*may*" lina-*include shall,* lakini *shall* haliwezi ku-*include may*. Hapa hiki kifungu kilivyoandikwa ni tofauti na kilivyoandikwa kile cha kwenye *NSSF,* wakati vyote vinataka kuzungumza kitu kimoja. Ile *drafting* ilivyoandikwa hapa ni tofauti na kule *NSSF*.

Sasa, mambo mawili; la kwanza, kule kwenye *NSSF* mmesema kwamba *Director General* anaweza; yaani hii fedha ambayo imezidi inaweza ikatumika kwenye kufuta madai mengine ambayo yanaweza kuja baadaye ama kitu kama hicho nafikiri. Ngoja nikitazame kifungu hicho. Kipo wapi? Nanyi kitazameni ni cha ngapi maana nimekiona mahali hapa.

Kifungu cha 14 kwenye Muswada, ambacho ni Kifungu cha 16 kwenye sheria kinazungumzia, *"refund of contributions remitted in error."* Cha *NSSF* kinasema, *"where the Director General is satisfied that any amount has been remitted to the fund as contribution as a result of an error, the amount remitted in error shall be refunded or used with the consent of the person who remitted it to offset any current liability."* Sawa, huku imetumika neno *"shall."*

Sasa, ukija hapa inasema; *"any money paid to the fund in error or in excess of the amount in which an employer is liable in respect of the assessment payable to the specific period, may be refunded."* Sasa hivi mmesema iandikwe *"shall"*. Haya, *"shall be refunded to the employer in such a manner as the Director General may determine."* Huyu kwa nini akilipa za ziada asi-*offset?* Ama kwa sababu huku hakuna binafsi, kule kuna binafsi? Maana kule mmesema *person* na *person* wote tunajua *interpretation* yake. Yaani hivi vifungu vinataka kusema jambo moja, lakini uandishi umetofautiana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMEVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli lakini msingi wake ni kwamba moja ya mfuko *(NSSF)* una-*deal* na *private sector* na huu mwingine *PSSSF* una-*deal* na Serikali.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Serikali lazima irudishiwe ila huyu mwenye kampuni binafsi siyo lazima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMEVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hapana ni lazima. Hoja inakuja kwamba, huku katika upande wa Serikali inapotokea kama kuna malipo ambayo yamelipwa ya ziada, kuna *procedure* nyingi kidogo za kufuata kwa sababu kuna hiyo *demand* ya *procedures* ambazo ina-*involve* zaidi ya mtu mmoja kufanya *internal auditing* na kuweza kufanya hizo *procedures.* Hata kwenye mashtaka mfumo wa Serikali tuna *government proceeding* zake inahitaji *at least* utoe taarifa…

**MWENYEKITI:** Ngoja usianze kutuchanganya Mheshimiwa. *(Makofi)*

Usianze kutuchanganya kwa sababu kama aliyelipa na yeye ni mwajiri na huu ni utungaji wa sheria, tunarudi pale pale unatunga sheria. Sasa huyu unataka umrejeshee, huyu mwingine unamgomea. Kwani Serikali huwa haidaiwi na mifuko? Si na

yenyewe pia huwa inadaiwa? Je, mfuko ukiona ile fedha ikibaki wanaenda kuwekeza haraka? *Anyway…*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMEVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaliangalia ni *internal arrangement* za upande wa Serikali kwa sababu taasisi zote kwa upande huo...

**MWENYEKITI:** Tena umeeleza mwenyewe kwamba, mlolongo wa kwenye Serikali utakuwa mrefu kweli, yaani kurejesha hizo fedha mpaka zifike kule mwezi mwingine utakuwa umeshafika. Kwa hiyo, afadhali wangeziacha kabisa.

Sasa tunarudi pale mwanzo nilipokuwa nimesema nitakupatia nafasi Mheshimiwa Ali King, kwenye ule uandishi wa vile vifungu vinavyofanana. Hebu jaribuni kutazama kwa sababu mwisho wa yote huyu wa *NSSF,* sawa inashughulika na watu binafsi, lakini huu sio mfuko binafsi. Sijui kama tupo pamoja?

Huu si mfuko binafsi! *This is also a public fund.* Pamoja na kwamba wapelekaji fedha huko ni binafsi, lakini huu nao ni *public fund* unaoshughulika na *public servants,* na huu ni ni *public fund* unaoshughulika na *private sector.* Siyo *private fund.* Kwa hiyo, lazima...

Mheshimiwa Ali ulitaka kusema kitu gani?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, hapa tumekusudia mfuko unaotajwa hapa ni *WCF* siyo *PSSSF.*

**MWENYEKITI:** Sawa, tumepitiliza.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ni *WCF* ambao *contributors* ni wafanyakazi wote wa umma na binafsi.

**MWENYEKITI:** Ngoja tuone. Kumbe tumeshapitiliza, *part three.* Tupo *part four* kumbe, Sawa. Sasa umesikia, *this is even more serious.* Kwa hiyo, maelezo yako Mheshimiwa Waziri haya-*justify* hiki kifungu. *(Kicheko)*

Hayaendi hapo kwa sababu kweli tulifikiri kipo pale kwenye Serikali. Naona huku kwenye Serikali ndiko hakipo kabisa. *Anyway,* kakitazameni muone kama na kwenyewe kunahitajika kifungu hiki, lakini kwa sasa hapa namna kilivyo hiki cha 62(6) kinachorekebishwa kweli ni cha *WCF* na siyo *PSSSF*.

Kwa hiyo, kile kifungu kilichopo 14, *page nine*, nafikiri chukueni hizo sekunde 30 tazameni kama hii 16 na hii sita iliyoandikwa hapa vinalenga jambo moja, ili tutumie maneno yale ya kwenye 14 hapa. Hebu tujiridhishe kama vinazungumza jambo moja.

Waheshimiwa nimeangalia hii sheria ama hiki kifungu, hakipo kabisa, ni kifungu kipya kinaletwa. Kwa sababu ni kifungu kipya, kama mmesoma hapo mmeona *spirit* inafanana na ile nyingine, kile cha *NSSF* kimeandikwa vizuri zaidi kuliko hiki kwa sababu kinazungumzia *paid to the fund in error or in excess,* na hiki cha huku kinazungumzia *refund of contributions remitted in error*.

SKwa hiyo, kile cha kule *NSSF* kimeandikwa vizuri zaidi kuliko hiki, si ndiyo? Kwa sababu vinazungumzia jambo moja, basi Kifungu cha 62(6) kichukue Kifungu cha 14 cha Muswada. Hebu kitazameni hapo, kinakuwa kimekaa sawa? Badala ya kuwa Kifungu cha *sub,* kwa sababu ya ile *marginal notes*, vinakuwa haviendani. Yaani kikichomekwa hapo kinakuwa kama kiko *out of place*. Kwa hiyo, kwa sababu ni kifungu kipya, pale kilipochomekwa kinakuwa hakijakaa vizuri, ukichukua yale '*opening*' ukaweka hiki Kifungu cha 16 pale, kinakuwa hakina mtiririko mzuri wa uandishi wa sheria.

Kwa hiyo, kiingie kama 75(A), Kifungu kipya kabisa na kiwe kinahusu *refund of contribution remitted in error* ama *in excess, whatever*, *minor in error* tu itakuwa inatosha. Ama mnaonaje? Mmekiona vizuri lakini? Isije ikawa, tena unaona huku maneno yameongezwa vizuri, "*Any amount paid to the fund in error or in excess of their amount, in which an employer is liable to ...*"

*Attorney General*, naona huku kwenye hiki kifungu tunachotaka kuondoa kina maneno "*in excess of the amount*"

siyo *error* peke yake. Kile cha 16 kinazungumzia *error* peke yake. Sasa, hii '*error*' na '*in excess*' vinaweza kuwekwa pamoja au tutakuwa tumechanganya mambo hapo?

Haya, nyie mko vichwa vitatu ama mko vichwa vingi, mmeona tunaweza kuongeza kule kwenye 14 yale maneno '*in excess*' ama ni viwili vitengane hivyo hivyo, viwe peke yake peke yake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulikuwa tunafanya *consultation* pia na wataalamu wetu wa Mifuko naona wako *comfortable* kuichukua ile *Clause 14* kuipeleka katika 62 kama ambavyo mwanzo tulikuwa tumeiona.

**MWENYEKITI:** Sasa tukishaipeleka, kwa sababu huku hii *14* imesema tu kuhusu *error*, haijazungumza (A), kwa hiyo, labda Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapa kwenye *error* yawe *merged* na yale ya *assessment error or* ili kifungu kiwe *robust*, si ndiyo. Kwa hiyo, hii *16* ndiyo itaenda kwenye haya mabadiliko yaliyoko kwenye 62 lakini sasa kwenye uandishi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa namna Kifungu cha 14 kinasomeka ili kilete maana vizuri kwenye *WCF*, inabidi kikae kama 75(A) ili kiwe na *marginal note* yake, lakini yale maneno yaliyoko kwa sasa kwenye *62(6)*, yale yanayohusu "*in excess of the amount*" na kuendelea huko iingie pale ili Kifungu kikae vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hatuwezi kufanya uandishi sasa hivi hapa na kama nilivyokuwa nimesema, haya kwa sababu anaunganisha maneno ambayo sisi wote tumekubaliana hapa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataiweka vizuri halafu tutapata taarifa.

Tulikuwa Kifungu sitini na ngapi? Kwa hiyo, tumeshaelewana hii 62 namna itakavyokuwa? Haya.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 62

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Sasa sisi tumesema ndiyo kwenye kuongezeka 75 (A) na haya kuwa *merged* yale kuja huku. Ahsante sana.

Kifungu cha 63
Kifungu cha 64

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *renumbering* ya *Clause 28 – 64 to 28 – 63*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaafiki mabadiliko haya ya namba?

*(Mapendekezo ya Mpangilio wa Namba za Vifungu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi, mtoa hoja taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni

ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Tolea la Mwaka 2023, ninapenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendment Act, 2024)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendment Act, 2024)* kama ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima sasa ukubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana na sasa nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja, ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kufanya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa Lengo la Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mifuko *(A Bill for an Act to Amend the Social Security Laws with the View to Make Better Provisions for the Administration and Management of Social Securities Schemes)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu umeshasomwa mara ya tatu. Kwa hiyo, tumeshamaliza kazi yetu kama Bunge na tutaupeleka kwa Mheshimiwa Rais ili naye aweze kuufanyia kazi kama ambavyo Katiba inamtaka.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, natumia nafasi hii kutangaza kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendment Bill, 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua hizi ambazo zimeshachukuliwa na Mawaziri ambao wako chini ya ofisi yake; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko haya, mengi ni yale ambayo katika michango yenu mmekuwa mkipendekeza hapa na pale kwenye changamoto za utekelezaji wa sheria hizi na sasa Serikali imesikiliza maoni yenu na imeleta mabadiliko haya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, natumia nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuwa sikivu kwenye Mawazo wanayoyatoa Waheshimiwa Wabunge na mpaka tumefika sehemu ambapo kwa kweli wastaafu wanaweza kupata haki zao. Hata kama bado kuna changamoto, tutaendelea kuzifanyia kazi, lakini hatua zilizochukuliwa kwa sasa kuweka mambo haya kisheria ni hatua ambazo zinapaswa kupongezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawapongeza sana na kuwashukuru kwa ushirikiano mnaoutoa. Wakati huo huo tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mmeahidi kupitia Muswada huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia naishukuru Kamati yetu, kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana. Kamati hii ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imefuatilia jambo hili kwa karibu sana na yako mambo mengine ambayo bado wanayafanyia kazi, lakini kwa kupitishwa kwa Muswada huu sasa nafikiri mengine yanaweza kuwa yameshapata majibu hata kama utekelezaji, utakuwa unasubiri sasa kibali cha Mheshimiwa Rais, ikiwa ni pamoja na Mifuko yetu hii ya Hifadhi kuanza kulipa wastaafu bila kusubiri kama yule mwajiri alikamilisha malipo ama hakukamilisha, maana lilijitokeza kwa ukubwa sana hapa ndani ambapo

waajiriwa wakawa wanatakiwa wao wachangie ili Mfuko uweze kulipa. Sasa kwa sababu hilo limeondolewa na sheria, Kamati yetu itajaribu kupima kama hoja bado ipo ama imeondoka baada ya kufikia hatua hizi ambazo Serikali imefikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa kweli tunawashukuru sana, lakini na Wabunge wote kwa sababu Mawazo haya huwa yanatoka humu ndani halafu Kamati fulani ndiyo huwa inapewa kwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wote ahsanteni sana kwa ushirikiano mzuri ambao mmekuwa mkiutoa na tunaamini tutaendelea kushirikiana hivyo ili kuhakikisha haki za Watanzania zinalindwa katika maeneo yote ikiwa ni pamoja na hili eneo la mafao yao kutochelewa wala mafao yao kupunjwa ama wao kutakiwa kufanya chochote cha ziada zaidi ya kazi waliyoifanya katika kipindi chao cha utumishi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, leo ratiba yetu tulikuwa na Muswada huu na tumeumaliza kwa muda huu, tumevuta kidogo muda. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa uvumilivu, lakini ilikuwa ni muhimu tumalize kwa sababu mtoa hoja alianza kuhitimisha kabla, na kanuni zetu zinataka tukikaribia kuhoji basi tumalize. Kwa hiyo, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo mara baada ya kusitisha Bunge hapa, Wabunge wanawake tutakutana Ukumbi wa Spika ghorofa ya tano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.55 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Agosti, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*